SUPA JACKPOT
TZS. 1,034,905,195
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## MGOGORO NCCR Mageuzi bado ngoma mbichi


Ukurasa 16
UCHUMI WA BLUU KILWA
Inaweka rekodi Bara Afrika, pweza kuvuliwa kwa kigezo elektroniki, kutua soko kimataifa

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 30, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Machinga Dodoma wafika mwisho mtaani, kuhamia maisha ya sokoni
Ukurasa 18

Wanakijiji Magu wachoshwa, wajenga daraja lenye kiwango, TARURA yabariki

Na Anthony Gervas, MAGU

"MATESO ya miaka mingi bila kupata ufumbuzi wa kutatua kero hii ya kuvuka Mto Nyalali, unaotenganisha kata za Bujora na Kisesa wilayani Magu mkoani Mwanza,hatimaye sasa wananchi tumepata dawa ya kuondoa kero hii bila kusubiri Serikali," sauti ya wananchi wakisema.

Wananchi na wadau wa maendeleo katika vitongoji vya Iseni A,B na Ng'wang'alanga A katika kata hizo, wameamua kujitolea kuchangia kujenga daraja dogo, baada ya kuchoshwa na changamoto ya kuvuka maji katika mto Nyalali unaozitengenisha kata hizo.

Ni uamuzi mgumu wa kujenga kwa nguvu zao wenyewe bila kusubiri fedha za Serikali,kutokana na mto huo kuwatesa kuvuka kwa miaka mingi pasipo na ufumbuzi ,ambao wakati wa mvua na mafuriko hulazimika kuzunguka umbali wa takribani kilomita tatu kupata huduma zao.

Hofu yao ilikuwa ikitokea wakati mvua za masika zinapoanza kunyesha na kusababisha kukatika mawasiliano rahisi, hivyo baada ya kukamilika kivuko hicho kitawezesha kupita hata magari madogo ya mizigo,watembea kwa miguu na vyombo vingine vya usafiri.

Wananchi hao, Kanisa la Pentekoste (FPCT) na wadau wamechanga vifaa vya ujenzi, fedha tasilimu, mawe ,saruji, mchanga nondo, mawe tripu 30 kufanikisha ujenzi huo kugharimu kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 15 kukamilika daraja.

Wanakijiji na mafundi wao wakiendelea na kazi ya kujenga daraja, huku Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini wilayani Magu (TARURA), Mhandisi Wawa Nyonyoli ( wa kwanza kulia mwenye jaketi la kijani) akiwashuhudia. PICHA: ANTHONY GERVAS.

Wanasema watoto na wanafunzi walikuwa kupita kwenda shule na kuwasababishia adha kubwa wazazi wao kuingia gharama za usafiri wa bodaboda kuzunguka mto huo.

Kaulimbiu yao ni kuondoa kero zinazowakabili muda mrefu, ikiwemo kutengeneza barabara za mitaa,ambazo ni changamoto kubwa hadi sasa.

KINAMAMA.

Jenifa Masanja, ni mwanamke anayewashukuru kukubaliana kufikia uamuzi huo wa kuondoa changamoto iliyowasibu muda mrefu, watoto na wanafunzi kupata shida kubwa.

MWENYEKITI KAMATI

Shaban Kumalija, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Daraja, anaeleza kuwa wananchi na wadau wamejitolea kuchangia ujenzi huo, kuondokana na kero hiyo inayowaumiza kichwa kila siku kutafuta namna ya ufumbuzi.

Kumalija anasisitiza kujengwa kwa miundombiu hiyo katika ubora unaotakiwa bila kufanyika udanganyifu wa aina yeyote katika fedha zitakazotumika, wakikusudia kukamilisha mwezi ujao,Oktoba.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ng'wangh'alanga Mwenesho Malago, anasema ilibidi yeye na wadau kuibua wazo hilo la ujenzi, kutokana na wananchi wao kila kukicha wanalalamika kuhusu uvukaji mgumu katika mto huo hasa nyakati za masika.

Malago anasema hivi sasa ndoto yao imetimia na kuepuka shida iliyokuwa ikisababisha hata maafa ya wananchi na watoto kusombwa na mto, akimshukuru meneja wa tarura Wilaya ya Magu kufika katika ujenzi na kukagua daraja lao pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam.

Anasema hatua hiyo itasaidia vitongoji vyote hata kurahisisha huduma muda wote katika kipindi cha mavuno mazao ya wananchi kupita na magari.

Hata hivyo Mwenyekiti wa kijiji cha Wita, Michail Migeke anaipongeza jamii na wadau hao kuhusu mchango wao wa hali na mali kuhakikisha wanatatua kero hiyo,badala ya kusubiri serikali kwani haikuwa rahisi kuchukua hatua za kutatua changamoto hiyo.

DIWANI KATA YA BUJORA.

Diwani wa Kata ya Bujora, John Bunyanya, anaeleza kuunga mkono juhudi hizo za maendeleo, lakini wasimamizi wake wafuate taratibu na sheria za ujenzi kuanzia ngazi ya vitongoji,vijiji hadi kwenye kata kama walivyokubaliana katika vikao vyao, ili kuondoa migogoro inayoweza kutokea baadaye.

"Kama tulivyokubaliana kwenye kikao,ili hata likitokea jambo diwani asiingie mkenge kwamba alikubali wakati mimi sijaona barua yao kama mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya kata," anasema.

MENEJA TARURA

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini wilayani Magu (Tarura), Mhandisi Wawa Nyonyoli, anapongeza juhudi za wananchi na wadau waliojitolea kuchangia maendeleo, wakitumia nguvu zao wenyewe kuwa hata serikali iko nao bega kwa bega kuhakikisha ujenzi unafanyika katika kiwango chenye ubora unaotakiwa.

Mhandisi Nyonyoli anasema, daraja litakalojengwa linatakiwa kudumu zaidi ya miaka 30 likitoa huduma kwa wananchi, yakiwemo magari na vyombo mbalimbali vya usafiri, akiwaomba kuboresha barabara zinazounganisha huduma hiyo.

Katika upande wa barabara, anashauri ziwe na upana wa mita nane, mitaro na sehemu ya kupitisha huduma za miundombinu mingine kama vile nguzo za umeme na mabomba ya maji.

Anataja kuwa zipo aina tatu za barabara ambazo ni pamoja na makusanyo yenye upana wa mita 40 ikiwemo hifadhi yake, barabara mlisho ikiwa na ukubwa wa mita 30 pamoja na mita 25.

Anaeleza kuwa kama barabara inayounganisha daraja hilo itatengenezwa vizuri kwa kufuata vipimo vya kitaalamu,tarura itaangalia uwezekano wa kuweka bajeti na kuingiza katika mtandao wa barabara, ikiwa hivi sasa haiko rasmi kwenye mtandao huo.

UKURASA 13

Nipashe
Ijumaa Septemba 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581084
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Magonjwa moyo sasa janga zito

**TAKWIMU** kwa siku, mwezi zatisha, Janabi abainisha mzigo gharama za matibabu...*Endelea ukurasa 2*



Timu ya madaktari bingwa wa moyo wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa kushirikiana na wa Shirika la One New Heart, wakifanya upasuaji kwa watoto wenye matatizo ya moyo, jijini Dodoma jana, katika kambi ya siku tano ya upasuaji bure ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Samia: Hakuna mkataba bila Mwanasheria Mkuu

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akibonyeza kitufe cha kompyuta kuzindua rasmi Chama cha Mawakili wa Serikali, baada ya kufungua mkutano mkuu wa mawakili hao, jijini Dodoma jana. Wengine ni Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (wa pili kushoto) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wazee walilia pensheni kama ilivyo sasa kwa wenzao Zanzibar

UKURASA 3

UKURASA WA 4



### MRADI UWEKEZAJI KANDA MAALUM WAZINDULIWA

SERIKALI imezindua mradi wa uwekezaji katika kanda maalum ya kiuchumi wa Mkinga mkoani Tanga na kuahidi kuwaunga mkono wawekezaji wa ndani na nje...

UKURASA WA 4

### KAMATI YATAKA SERIKALI KUONA FURSA DAMPO PUGU KINYAMWEZI

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imeishauri serikali itumie dampo la Pugu Kinyamwezi kama fursa inayoweza...

UKURASA WA 5

### DAKTARI AWAPA NENO WENYE TATIZO UVIMBE

MRATIBU wa Afya ya Kinywa na Meno Taifa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, amewataka wenye uvimbe mdomoni, badala ya kuzunguka mitandaoni kuelezea waende hospitali...

UKURASA WA 5

### TANZANIA KUNUFAIKA MABILIONI YA JAPAN



TANZANIA ni moja ya nchi za Afrika zitakazonufaika na fedha za Mfuko wa Kukuza Uwekezaji barani Afrika kutoka serikali...

UKURASA WA 7

### WAHARIRI WANAWAKE AFRIKA WANG'ARA TUZO WIN

TAASISI inayosaidia vyombo vya habari duniani WAN-IFRA Women in News (WIN), imewatunuku tuzo za umahiri wa uongozi bora wanawake viongozi katika vyombo vya habari.
Kati ya wanahabari hao walioutunukiwa tuzo hizo jana...

**MICHEZO** SIMBA YAMJIA JUU DEJAN UK. 32

**KABWELA** UK. 7



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (kulia), akitoa maelekezo baada ya kukagua shamba la kimkakati la mkonge la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kikosi cha Mgambo 835 KJ, Kabuku, wilayani Handeni juzi, linalolimwa na vijana wakujitolea kwa mujibu wa sheria. Wengine ni Mkuu wa JKT nchini, Meja Jenerali Rajabu Mabele (kushoto), Mkuu wa kikosi hicho, Kapteni Raymond Mwanri (wa pili kulia) na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Seriel Mchembe. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Magonjwa ya moyo sasa janga zito

**Na Waandishi Wetu**

UGONJWA wa moyo unaonekana kuwa tatizo kubwa nchini kwa sasa baada ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa, Dodoma kuweka bayana ongezeko la wagonjwa wanaopokewa kupata huduma.

Jana, JKCI ilisema inapokea wastani wa wagonjwa 300 hadi 500 kutoka 30 hadi 40 kwa siku, huku Benjamini Mkapa ikipokea 1,300 hadi 1,500 kutoka 150 hadi 200 kwa mwezi.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya JKCI, Muhimbili jijini Dar es Salaam, kwa kaulimbiu ya 'Tumia Moyo kwa Kila Moyo', Mkurugenzi wa Matatizo ya Moyo wa JKCI, Dk. Tatizo Waane, alisema kati ya wagonjwa hao, 120 wanabaki wodini kwa matibabu.

Dk. Waane alisema kati ya wagonjwa hao, asilimia 30 wanagundulika kuwa na shinikizo la juu la damu, asilimia 35 uzito mkubwa na asilimia 26 wana kiwango kikubwa cha lehemu (cholesterol) katika damu.

Alisema tatizo hilo linaongezeka nchini siku hadi siku ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka kadhaa liyopita.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa JKCI, Dk. Samweli Rweyemamu alisema kuna uhusiano mkubwa wa ugonjwa wa moyo na shinikizo la damu na kwamba magonjwa hayo hayana dalili za moja kwa moja bali huonekana kwenye shinikizo la damu huku wengi huishia kwenye vifo vya ghafla.

Dk. Rweyemamu alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni mwili kuchoka, kuumwa kifua hasa mtu anapotembea, kupanda mlima au kufanya kazi ngumu, kukosa hewa akiwa sehemu finyu na sehemu ya wazi au akiwa usingizini, kuvimba miguu, tumbo na mapigo ya moyo kwenda mbio isivyo kawaida

.

**BENJAMINI MKAPA**

Jana, Hospitali ya Benjamini Mkapa kwa kushirikiana na One New Heart walifanya upasuaji wa moyo kwa watoto sita waliotoka mikoa mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamini

Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, alisema watoto hao wamefanyiwa upasuaji huo kifuani na

wanaendelea vizuri chini ya uangalizi wa karibu wa madaktari.

"Magonjwa ya moyo yameonekana kuongezeka siku hadi siku na hii inatokana na jamii kutofuata maelekezo ya wataalamu hususani katika suala la mazoezi pamoja na vyakula wanavyokula," alisema Dk. Chandika.

Alisema gharama za matibabu ya upasuaji wa watoto hao ni zaidi ya Sh.milioni 30 na aliwashukuru wadau walioshiriki kugharamia matibabu.

Pia alisema katika hospitali hiyo wanaoongoza kwa maradhi ya moyo ni wenye shinikizo la damu, ugonjwa unaochangia kwa kiasi kikubwa kutanuka kwa moyo kutokana na mfumo wa maisha kama kunywa pombe kupita kiasi na uvutaji sigara.

Kadhalika, alisema kimeanzishwa kitengo hospitalini hapo ili kupunguza mzigo kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kwamba matatizo ya moyo ni asilimia 91 na kati yake asilimia 68 wanabainika kuwa na tatizo hilo.

Naye Mkurugenzi wa Habari na Maendeleo wa The

One New Heart Tanzania, Godfrey Maro, aliipongeza Benjamin Mkapa kwa huduma nzuri na kuitaka jamii kufuata ushauri unaotolewa na wataalam.

**GHARAMA KUBWA**

Akizungumza jijini Arusha, kwenye maadhimisho ya siku ya moyo kitaifa, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema gharama za kuzibua mishipa ya moyo ni Sh. milioni sita, kuweka betri katika moyo Sh. milioni 10.5 na kutoa mshipa kwenye mguu kuweka kwenye moyo ni Sh. milioni 32.

**MADAKTARI FEKI**

Katika hatua nyingine, Dk. Rweyemamu aliwataka Watanzania kutambua kuwa hakuna huduma ya moja kwa moja kutibu moyo duniani kote bali kuna tiba endelevu ambazo mtu atatumia maisha yake yote.

Pia alisema kwa sasa kuna wimbi la madaktari feki mitaani wanaodanganya umma kwamba wanaweza kutibu moyo huku wengine wakiwaambia unywaji maji mengi unaponyesha jambo ambalo si kweli kitaalamu.

"Matatizo haya hasa yanasababishwa na ulaji mbaya, mitindo ya maisha vinachangia kukua kwa matatizo haya kwa watanzania walio wengi,"alisema daktari huyo.

LISHE

Kwa upande wake, Ofisa Lishe wa JKCI, Husna Faraji, alisema ulaji mbaya wa chakula ndio chanzo namba moja kinachopelekea kuongezeka kwa magonjwa hayo ya moyo.

"Katika utafiti uliofanyika Watanzania wanatakiwa wabadilike katika suala zima la ulaji na hii itasaidia kupunguza au kuondoa wimbi la ongezeko la magonjwa hayo, kila mtu anatakiwa kujua anapaswa kula chakula gani, wakati gani," alisema.

**Imeandikwa na Renatha Msungu (DODOMA), Pilly Kigome (DAR) na Golden Kisapile (TUDARCo)**

# Samia: Hakuna mkataba bila AG kuhusishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza kuanzia sasa hakuna mkataba serikalini utakaoingiwa bila kushirikisha ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ili kuepuka mizozo inayoweza kujitokeza.

Aidha, amewaagiza mawakili wa serikali kusimamia haki wanapochezesha vifungu vya sheria ili wasiwanyime wanaostahili kupata haki.

Pamoja na hayo, Rais Samia ameagiza kuangaliwa sheria ya kulinda uwekezaji nchini kwa kuwa bado ni kikwazo na imekwamisha miradi mikubwa mitatu au minne yenye fedha nyingi kuwekezwa nchini.

Akifungua Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali jana jijini hapa, Rais Samia alisema kuna tatizo la baadhi ya mikataba kuingiwa bila kushirikisha ofisi ya AG na unapoibuka mzozo, wanarudi kwake ili awasaidie.

"Mliingiaje mikataba kama AG hajui? Pengine aliyeingia mkataba ule alishastaafu au hayupo duniani, kwa hiyo kupata chanzo inakuwa ngumu. Huu ni wito kwa serikali nzima sasa hakuna mkataba utakaoingiwa bila kushirikisha ofisi ya Mwanasheria Mkuu," alisema.

Pia alisema nchi inaingia mikataba mikubwa kwa sasa na wawekezaji kutoka nje na sheria zinataka inapotokea mzozo, mwekezaji atumie sheria za ndani ya nchi.

"Kama mtu anakuja na fedha yake kubwa anaiwekeza ndani ya nchi, tunakwenda na uwekezaji ule, mzozo unapotokea unamwambia mimi nitakuhukumu. Nadhani halileti sura nzuri sana kwa wawekezaji. Wengine wanatukimbia kwa sababu hiyo.



"Nina mifano hai mkononi. Kuna miradi mikubwa mitatu au minne hivi wawekezaji wanakuja na fedha nyingi sana, lakini tumejadiliana tumefika katikati mwekezaji anasema unapotokea mzozo twende kwa mtu wa tatu usije kwangu nisihukumiwe na wewe twende kwa mtu wa tatu, sisi tunasema hapana unapotokea mzozo mimi mwenyewe nitakuhukumu.

"Sasa wewe umekula fedha yake amekupa ajira uwekezaji upo kwako kisha ukitokea mzozo unasema mimi nitakuhukumu. Tuwe wa kweli jamani kuna haki hapo? Pamoja na kwamba tunasema tuna sheria ya kulinda uwekezaji, AG tuitizame vizuri," alisema.

Rais alisema kuna mashauri inawezekana kufanyika nchini lakini kuna mengine ambayo mwekezaji makini akipewa kipengele hicho atakimbia.

"Sekta zinarudi kwangu zinasema tumekwenda vizuri lakini tumekwama hapa. Nikicheki upande wa pili wanasema hapana hatuji kuwekeza fedha hizo zote halafu ikitokea mzozo nyie ndio mtuhukumu. Haiwezekani, hatuwezi kuja ndivyo wanasema. Nadhani mlitizame vizuri nyie ndio wataalamu wa sheria," alisema.

"Ili kuendelea na uwekezaji mzuri na mkubwa utakaokuza uchumi wetu lazima mawakili wa serikali muwe makini sana kuharakisha kusikiliza migogoro hii. Nimefurahishwa na hili ulilolisema Mwanasheria Mkuu kwamba mnajipanga kusikiliza migogoro kabla ya kufika mahakamani ili kupunguza kupelekana mahakamani na wawekezaji wetu au wafanyabiashara wetu wakubwa.

"Haya hayatagusa masuala ya kodi. Haya ni kwa upande wa sheria za uwekezaji, sheria za biashara. Niwasihi sana kujiweka vizuri katika hili, tukilinda uwekezaji unaowekezwa Tanzania. Tunakwenda kupanua wigo mpana wa kukuza uchumi," alisema.

**ABAINI MGONGANO**

Rais pia alisema amebaini kuwapo na mgongano kati ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwamba atakutana nao ili kuangalia suala hilo.

Kuhusu utendaji haki, Rais Samia alisema mawakili wamekabidhiwa sekta ya haki, hivyo waifanye kwa uadilifu. Alisema kabla ya mabadiliko katika sekta ya sheria, haki ilikuwa ikiikukwa sana, mlundikano wa wafungwa au mahabusu ulikuwa mkubwa kwa sababu haki haifanyiki, haisimamiwi, hivyo wakasimame kwenye haki kwa uadilifu na uaminifu.

"Ninyi ni mainjinia (wahandisi) wa kucheza na vifungu vya sheria. Mtu anakosa mnacheza na vifungu anaachiwa au asiye na kosa akatiwa hatiani, sasa hiyo engineering (uhandisi) haiwapeleki pazuri, fanyeni yale yatakayowasimamisha kwenye haki,' alisema. Awali, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dk.Damas Ndumbaro alisema Mawakili hao ndio watekelezaji wa majukumu na askari na wapiganaji katika mfumo wa utoaji haki, masuala ya mikataba na usuluhishi wa migogoro.

Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Hamis Juma, alisema bado kuna sheria ambazo ni kikwazo kwa maendeleo, uwekezaji na biashara huku akidai kuwa hakuna sheria ya masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, nishati mbadala na kushauri maeneo hayo yaangaliwe.

## HABARI KITAIFA

# Wazee walilia pensheni kama wenzao Zanzibar

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MTANDAO wa Mashirika ya Kuhudumia Wazee Tanzania, umependekeza utaratibu wa kuwalipa pensheni wazee unaofanyika Zanzibar, ufanyike kwa Tanzania Bara kutokana na umuhimu wao kwa taifa.

Akizungumza jana jijini hapo kwenye mjadala wa kitaifa kuhusu masuala ya wazee ulioandaliwa na Shirika la HelpAge kwa kushirikiana na Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Mwenyekiti wa mtandao huo, Cotilda Kokupima, alisema serikali ya Zanzibar inatekeleza hilo, hivyo ni muhimu Tanzania Bara kuweka utaratibu huo ili kuwasaidia wazee ambao miongoni mwao wamelitumikia taifa kwa uaminifu.

Kuhusu bima ya afya, alishauri utaratibu wa bima ya afya kwa wazee usilenge wasio na uwezo bali kipengele kirekebishwe iwe kwa wazee wote.

"Mzee anakwenda kwenye kituo cha afya anapanga foleni hadi mwisho anaambiwa dawa hakuna nenda ukanunue, hilo ni tatizo atanunua na nini? Maana yake aende nyumbani akafe, lakini dawa pia hazipatikani kama shinikizo la damu na kisukari," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema hayo ni magonjwa makubwa ya wazee ni muhimu dawa kupatikana bure kwa kuwa hawana uwezo wa kununua kwa Sh.30,000 kwa mwezi.

Kadhalika, alisema ulinzi wa wazee bado ni tatizo kwa kuwa wanauawa na wengine kuzikwa wazima huku wengine wakifanyiwa ukatili na wakinyang'anywa mali zao.

Awali, akifungua majadiliano hayo, Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alishauri kuwapo na utaratibu wa pamoja wa kuwatunza na kuwaenzi wazee.

Alisema nchi nyingi duniani wazee wamekuwa wakitunzwa isipokuwa kila nchi ina namna yake ya kuwatunza wazee hao kulingana na mila, desturi na tamaduni pamoja na hali ya kiuchumi za nchi zao.

"Hata hiyo ilionekana kwamba ingefaa kuwe na utaratibu madhubuti wa kuwatunza na kuwaenzi katika kuchughulikia changamoto zao, wenye kulingana na namna fulani kimataifa na kikanda, hivyo ungekuwapo ingekuwa vizuri sana," alisema.

Dk. Shein alitaka jamii kupinga fikra potofu ambazo baadhi ya watu katika jamii hasa vijana wanazo dhidi ya wazee.

Alisema takwimu zinaonyesha idadi ya wazee ni asilimia 4.5 na kwamba matokeo ya sensa iliyofanyika hivi karibuni itatoa idadi kamili itakayosaidia kuwekwa mipango mizuri ya kuwasaidia.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alisema ni muhimu kusimamia utu na kuhudumia watu bila ubaguzi.



# Mgogoro NCCR- Mageuzi bado ngoma nzito

**Na Elizabeth Zaya**

MGOGORO ndani ya Chama cha NCCR-Mageuzi, bado ni ngoma nzito baada ya upande unaomuunga mkono Mwenyekiti James Mbatia, anayedaiwa kufukuzwa uanachama, kuwomba Jaji Kiongozi kuingilia kati.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Saalam, Mkuu wa Idara ya Uenezi na Uhusiano wa Umma wa NCCR-Mageuzi, Edward Simbeye (anayemuunga mkono Mbatia), alisema wameamua kuomba msaada wa Jaji Kiongozi kwa sababu wanaona haki yao imekiukwa.

"Tulipeleka kesi namba 150 ya mwaka 2022, ambayo ni maombi ya malalamiko ya kikao (cha upande wa Katibu Mkuu wa chama hicho, Martha Sambo) kilichofanyika Mei 21 na kulikuwa na ombi dogo namba 384 la kuomba zuio la mahakama la vikao walivyokuwa wamepanga kufanya Septemba 24 mwaka huu, mpaka ombi la msingi litakapotolewa uamuzi vilifanyika," alisema Simbeye.

"Tumeamua kumwomba Jaji Kiongozi kwa kuwa ndiye anayesimamia majaji wote kwa hiyo ana uwezo wa kuwaita wakakaa vikao vyao vya kinidhamu vya kijaji. Tunaamini atafuatilia kesi na kuona zuio tulilolitoa na namna ambavyo halijafanyiwa kazi," aliongeza.

Simbeye alitoa wito kwa wanachama wote wanaomuunga mkono Mbatia kuwa watulivu na kwamba atatoka hadharani wakati wowote kuzungumza nao.

"Tunaweka mazingira sawa ili mwenyekiti wetu (Mbatia) atoke hadharani na kuzungumza na wanachama wetu wakati wowote. Kwa hiyo tunaomba uvumilivu wao kidogo. Lengo ni kutaka tuondokane na dhuluma hizi ambazo tunaziona ni za wazi katika taifa letu," alisema Simbeye.Kwa muda kidogo, kumekuwa na mgogoro ndani ya chama hicho ambacho kinaonekana kugawanyika pande mbili, upande wa Mbatia na wa Sambo.

Pande hizo mbili, kila mmoja una wafuasi wake na unajiona ndio wenye mamlaka na chama hicho na kila mmoja umekuwa ukiitisha mikutano yake na kutangaza kumfukuza mwenzake.

Septemba 24, mwaka huu, upande unaomuunga mkono Sambo (Katibu Mkuu), uliitisha mkutano wa dharura uliofanyika jijini Dodoma na kutangaza kumvua uanachama Mbatia na wanachama wengine.

Siku iliyofuata, Mbatia naye aliibuka na kuitisha mkutano na waandishi wa habari ambao ulizuiwa na watu wasiojulikani katika hoteli aliyokuwa ameomba kufanyia, lakini alilazimika kuzungumza pembezoni mwa barabara karibu na hoteli hiyo iliyopo Mikocheni, Dar es Salaam.




# Mradi uwekezaji kanda maalum wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imezindua mradi wa uwekezaji katika kanda maalum ya kiuchumi wa Mkinga mkoani Tanga na kuahidi kuwaunga mkono wawekezaji wa ndani na nje kutumia fursa za uzalishaji kutumia teknolojia ya hali ya juu ya viwanda ili kuzalisha bidhaa.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mradi wa Mkinga na kuongeza kuwa, "Mradi wa Mkinga ni muhimu sana katika kuzalisha ajira nyingi kwa Watanzania hivyo unaenda sambamba na sera ya serikali ya kuboresha maisha ya watu wake."

Alisema katika mradi huu Mradi wa Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Mkinga Mkoani Tanga ambao utatekelezwa katika awamu tano, unaotarajiwa kuzalisha ajira zaidi ya 3,000 katika awamu ya kwanza ya utekelezaji.

Aidha, aliwapongeza wawekezaji hao kwa kuziona fursa zilizopo mkoani Tanga na kisisitiza kuwa serikali itawaunga mkono kwa kuwezesha uwekezaji huo kuwa na tija, kwa kuwa sekta binafsi ni moja ya sehemu kubwa katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakua.

"Serikali inatarajia uwekezaji huu kuwagusa moja kwa moja wananchi wa wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga na Taifa kwa ujumla kwani hiyo ndio itakuwa njia sahihi ya kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na hivo kuleta tija katika uchumi wa Taifa," alisema Kigahe.

Alisema wajibu wa serikali ni kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji kufanya kazi na kuweza kuwavutia wawekezaji wengi zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA), Charles Itembe, amesema kampuni ya Mkinga imepata leseni ya kubuni, kujenga na kusimamia viwanda vitakavyojengwa katika eneo hilo.

"Nawapongeza Kampuni ya Mkinga kwa kujitoa kwao na namna ambavyo wameionyesha dunia kuwa mradi huu unaweza kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa na sekta binafsi," alisema.

Aliongeza kusema, "Tunategemea kuwa mradi huu utakuwa moja ya miradi makubwa ya maeneo maalum ya kiuchumi kutekelezwa na sekta binafsi, lakini ukiunga mkono sera ya serikali ya kuvutia wawekezaji wa sekta binafsi katika uendelezaji wa miundombinu ya viwanda na kuvutia uwekezaji zaidi katika viwanda."

Alisema mradi wa Mkinga una mahusiano ya karibu na kampuni ya Misri, nchi ambayo imepiga hatua kubwa katika kuvutia uwekezaji kutoka nje hivyo kwa hatua hii itaweza kuifaidisha mradi huu pamoja na nchi kwa ujumla.

"Ili kuonesha kwa kiasi gani wawekezaji wa mradi wa Mkinga wapo makini, tayari kampuni hii imepata ekari 3,000 za ardhi ambazo zitaendelezwa kwa awamu tano ambapo kila awamu itakuwa na ekari 50 ambazo zitaendelezwa kwa gharama ya shilingi za kitanzania zaidi ya bilioni 115,"alisema.

Kwa kuanzia tayari kampuni hii imeshavutia wawekezaji 20 ambao wameonyesha dhamira ya dhati kuwekeza katika mradi wa Mkinga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa mradi wa Mkinga Special Economic Zone, Ally Kassim, alisema lengo la mradi huo ni kutekeleza maagizo ya serikali katika kuhakikisha uwekezaji nchini unaongezeka ili kuleta usawa wa kiuchumi katika maeneo yatakayofanyiwa uwekezaji husika.

Aidha, alisema wawekezaji hao wamethibitisha kuwa hadi sasa jumla ya wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali ikiwamo Brazil, Misri, Tunisia, Bulgaria, GCC, Ufilipino na India wameonyesha nia ya kuwekeza katika mradi huo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile (wa pili kulia), akishauri namna ya kuzichakata taka na kuwa malighafi, ili kutunza mazingira, walipofanya ziara katika dampo la Pugu, jijini Dar es Salaam juzi. Wa tatu kulia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Khamis Hamza Khamis. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC amaliza mgogoro wa shamba Mkalama na Singida

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amemaliza mgogoro wa shamba la mbegu lenye ukubwa wa ekari 456.82 lililo kati ya kijiji cha Mpambaa Wilaya ya Singida na kijiji cha Kinampundu wilayani Mkalama kwa kuagiza wananchi wagawiwe shamba hilo mara moja.

Serukamba alitoa agizo hilo jana akiwa na viongozi wa wilaya za Mkalama na Singida wakati akizungumza na wananchi wa vijiji hivyo ambao tangu mwaka 2020 wamekuwa na mgogoro huo huku kila upande ukidai una haki ya kumiliki shamba hilo ambalo lilikuwa chini ya serikali ya mkoa wa Singida.

"Naagiza shamba lote ekari 456.82 lenye mgogoro ligawanywe kwa wananchi wa Halmashauri za Wilaya ya Singida na Mkalama kwa kuzingatia mipaka iliyoainishwa kwenye GN (Gazeti la Serikali)," alisema.

Serukamba alitoa mchanganuo kuwa ekari 222.5 ambazo ziko upande wa Mkalama, zigawiwe kwa wananchi na ekari 234.32 zigawiwe kwa wananchi wa Singida.

Kufuatia uamuzi huo, mkuu huyo wa mkoa alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mlagiri na Sophia Kizigho wa Mkalama, kusimamia ugawaji wa mashamba hayo ili wananchi wanufaike kwa kuendeleza kilimo, ufugaji na shughuli zingine za uzalishaji mali.

Alisema vijiji vilivyoko eneo la mashamba haya, vipewe kipaumbele cha kuandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuepuka mgogoro mingine ndani ya utawala wa vijiji.

Pia aliagiza kuwekwa alama za mipaka (beacons) maeneo ya karibu mita 100 hadi 200 kwenye maeneo ya mpaka na wananchi wapewe elimu walipo na pia halmashauri na serikali za vijiji zihakikishe watakaopewa mashamba wanayalima na sio kuyaacha kuwa mashamba pori.

"Tusisubiri mgogoro kama hii inaibuka na kufika mpaka ngazi ya mkoa, wizara na ofisi za viongozi wa kitaifa ilhali sisi hatuna taarifa, tuishughulikie kwa kadri ya uwezo wetu ili tuitatue na wananchi waendelee na shughuli zao za kila siku za kujenga nchi," alisema.

Kuhusu historia ya mashamba hayo, alisema mkoa wa Singida ulianzisha mashamba makubwa mawili, shamba A na shamba B ambayo yalikuwa maalum kwa ajili ya kuzalisha mbegu.

Alisema shamba moja lilikuwa upande wa Singida na lingine lilikuwa upande wa wilaya ya Iramba na wilaya ya Singida iliamua shamba A kulipima na kulitolea hati, hivyo likabaki mali ya Singida lakini shamba B halikupimwa wala kupewa hati na wananchi waliendelea kulima bila utaratibu wowote.

Serukamba alisema mgogoro ulianza mwaka 2012 baada ya serikali ilipoanzisha wilaya mpya ya Mkalama na shamba B wananchi wa wilaya ya Singida na wa Mkalama walianza kugombania kila upande ukisema ni lake.

"Kwa kawaida ndugu wananchi tukiunda wilaya lazima wilaya iwe na mpaka wake. Lazima tutoe GN ili kila wilaya ijue mipaka yake kwa hiyo Iramba ikasogezwa mbali na ilipochorwa ramani kutengeneza mpaka shamba B likawa katikati ya Singida na Mkalama.

Alisema kutokana na mgogoro wa wananchi wa pande zote mbili, serikali iliunda tume kuchunguza suala hilo na kuja na majibu kuwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida wagawiwe ekari 234.32 na wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama wapewe ekari 222.5 ili kumaliza mgogoro huo.

"Utatuzi wa migogoro ni suala ambalo lazima tuangalie sheria, kanuni na miongozo inasemaje na sio suala la kukurupuka," alisema Serukamba.

Kutokana na uamuzi huo, wananchi kila upande walipongeza na kusema mgogoro huo sasa umefikia tamati wanachokisubiri ni wataalamu kwenda kuwapimia ili waendelee na shughuli za kilimo.

## Kamati yataka serikali kuona fursa dampo Pugu Kinyamwezi

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imeishauri serikali itumie dampo la Pugu Kinyamwezi kama fursa inayoweza kuiingizia mapato kwa kurejeleza taka hizo na kuibua fursa mbalimbali ikiwamo gesi na mbolea.

Dampo hilo lenye ukubwa wa eka 65 linachukua takataka zote za Mkoa wa Dar es Salaam na kwa sasa limezidiwa kutoka na wingi wa takataka zinazofikishwa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, David Mwakiposa, alitoa ushauri huo wakati kamati hiyo ilipotembelea dampo hilo jana kuangalia athari za mazingira ikiwa na maofisa wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

"Serikali ifikirie uwezekano wa kurejeleza zile takataka, kwa mfano tunapaswa kujiuliza hivi haiwezekani kuzichakata zile taka na tukapata mbolea, je, hatuwezi kuzichakata zikatuzalishia umeme, au haziwezi kuzalisha gesi. Lazima tuanze kufikiria mambo kama haya tuione hii ni fursa na kupunguza uchafuzi wa mazingira," alisema.

Alisema kamati imeishauri serikali kuja na mkakati wa kuwalinda wananchi wa jirani na maeneo hayo kwani kuna hewa yenye vimelea vyenye sumu inayotoka maeneo hayo ambayo ni hatari kwa afya.

Alisema hali ya dampo hilo siyo nzuri kutokana na wingi wa takataka hizo hivyo alishauri Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam kuangalia uwezekano wa kutafuta maeneo mengine ya kumwaga taka hizo.

Mbunge wa Bunda (CCM), Mwita Gitere, alishauri serikali ijenge ukuta mkubwa kuzunguka dampo hilo ili kulinda usalama na afya za wananchi wanaoishi jirani na eneo hilo kwani hali ya sasa ni mbaya na hatarishi kwa umma.

Alisema kamati imetembelea eneo hilo na kukuta watu wanakula na kulala eneo hilo likiwa na uchafu ambao hauvumiliki na viongozi wa Jiji wamekuwa wakitembelea na kuona lakini hawachukui hatua zozote.

Alisema kama serikali imeweza kujenga ukuta wa Mirerani kwa mabilioni ya fedha haiwezi kushindwa kujenga ukuta kwenye dampo hilo kwani imekuwa ikikusanya mabilioni ya fedha kwa taka zinazoletwa.

"Hivi shida ni nini hasa mpaka tunashindwa kujenga ukuta mrefu pale Pugu Kinyamwezi, tunaogopa nini kujenga ukuta pale mpaka tunawaacha wananchi wanaathirika kwa kiasi kile, wananchi wanatembea pekupeku wanakanyaga vitu vya hatari sana mle," alisema.

"NEMC nyinyi mmekuwa mkifungia fungia watu kwa kushindwa kutimiza masharti ya utunzaji wa mazingira sasa mnashindwaje kulifungia lile dampo. Mimi sijaridhika nataka turudi tena pale na vyombo vyote vya habari tuiambie dunia kinachoendelea pale," alisema.

Gitere alisema kamati hiyo inawajibu wa kutoa tamko zito kwa serikali ili ichukue hatua ya kurekebisha mazingira ya eneo hilo na wajumbe wa kamati hiyo wanapaswa kurudi kila baada ya miezi mitano kuangalia hatua zilizochukuliwa kurekebisha hali hiyo.

# Tanzania kunufaika mabilioni ya Japan

Na Mwandishi Wetu

TANZANIA ni moja ya nchi za Afrika zitakazonufaika na fedha za Mfuko wa Kukuza Uwekezaji barani Afrika kutoka serikali ya Japan zitakazotolewa kuanzia Machi, mwakani.

Mwenyekiti wa Timu ya Afrika ya KEIZAI DOYUKAI (Japan Association of Corporate Executives), Mutsuo Iwai, alisema hayo jana wakati akizungumza na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ofisini kwao, Marunouchi, Chiyoda-ku, jijini Tokyo, Japan.

"Ifikapo Desemba, mwaka huu, tutazindua kampuni ya kusimamia mfuko huu wa uwekezaji wenye manufaa barani Afrika na utekelezaji utaanza Machi, 2023. Tunataraji ifikapo Machi, 2024 tutakuwa tumetoa Dola za Marekani milioni 100 kwa kampuni za vijana wanaochipukia ili kuwajengea ubia, kujifunza teknolojia mpya na kubadilishana ujuzi," alisema.

Alisema fedha hizo za uwekezaji kwenye mitaji ya kuanzisha biashara (start-ups) zimelenga kukuza biashara ambazo zitatatua changamoto za kijamii zikiwamo sekta za afya, kilimo, nishati na kuimarisha uhifadhi wa mazingira.

Utolewaji wa fedha hizo ni utekelezaji wa ahadi ya Waziri Mkuu wa Japan, Fumio Kishida aliyoitoa Agosti 27, mwaka jana, kwenye Mkutano wa Nane wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaohusu Maendeleo ya Japan na Afrika (TICAD 8) uliofanyika Tunis, Tunisia.

Kishida alisema Japan imelenga kukuza uwekezaji ambapo safari hii wamelenga kuwainua vijana wanaoanzisha makampuni kwani hatua hiyo itawapa fursa vijana wa Afrika na wa Japan kufanya kazi kwa karibu.

KEIZAI DOYUKAI ni taasisi binafsi iliyoanzishwa Aprili 30, 1946 yenye wanachama 1,500 ambao ni watendaji wakuu na wamiliki wa kampuni kubwa za Japan wanaojihusisha na utoaji suluhisho kwa masuala ya kisera yanayohusu maendeleo ya nchi yao na dunia kwa ujumla.

Waziri Mkuu pia alikutana na wawakilishi wa Shirikisho la Wafanyabiashara wa Japan (KEIDANREN) ofisini kwao Otemachi, Chiyoda-ku, jijini Tokyo, ambako Mwenyekiti wa Kamati ya nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Hajime Kawamura, alimweleza shirikisho lao linavyojihusisha na miradi ya maji, barabara, nishati, mawasiliano utengenezaji wa kemikali na ununuzi wa mazao.

Wawakilishi wa kamati hiyo wanaotoka makampuni ya Sumitomo, Marubeni, Toshiba, Komatsu na Mitsubishi walimweleza Waziri Mkuu nia yao ya kuwekeza kwenye miradi ya nishati ikiwamo uzalishaji wa umeme kwa kutumia jotoardhi, usambazaji wa umeme, usambazaji wa gesi (LPG), huduma za mawasiliano na TEHAMA.

KEIDANREN (Japan Business Federation) jumuiya ya kiuchumi iliyoanzishwa Agosti 16, 1946 yenye wanachama 1,494 ambao ni wawakilishi wa makampuni ya Kijapani, ina vyama 108 vya wenye viwanda na taasisi 47 za kiuchumi kutoka mikoa yote.

Waziri Mkuu aliwaeleza wafanyabiashara wa makundi yote mawili kwamba Serikali ya awamu ya sita iko tayari kufanya kazi na wawekezaji na ndiyo maana iliamua kuboresha miundombinu ili kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu.

"Utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, utulivu na amani vilivyoko nchini, hali nzuri ya hewa, ujenzi wa bandari, reli na barabara, umeme na maji unawahakikishia wawekezaji uhakika wa mitaji pindi mnapoamua kuwekeza nchini Tanzania," alisema.

Waziri Mkuu aliwahamasisha waje nchini kuwekeza kwenye sekta ya utalii ikiwamo ujenzi wa hoteli za nyota tano na kuanzisha michezo ya majini kwenye fukwe za bahari Zanzibar na Bara.

"Pia angalieni uwezekano wa kuwekeza kwenye kilimo cha mashamba makubwa na ujenzi wa viwanda. Lengo la serikali hii ni kuendelea kukuza uchumi kupitia sekta mbalimbali ikiwamo viwanda," alisema.



# Daktari awapa neno wenye tatizo uvimbe

Na Romana Mallya

MRATIBU wa Afya ya Kinywa na Meno Taifa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, amewataka wenye uvimbe mdomoni, badala ya kuzunguka mitandaoni kuelezea waende hospitali kupata matibabu ili kuepuka kuondolewa taya.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni Dk. Nzobo alisema kadri uvimbe unavyokuwa ndivyo unavyoharibu taya na mwisho wa siku linaweza kutolewa.

"Mmekuwa mkishuhudia watu wengi kwenye mitandao ya kijamii mtu amewekwa video fupi ana uvimbe mkubwa mdomoni, badala ya kuwahi hospitali kutibiwa afanyiwe upasuaji kuuondoa, anazungumza mtandaoni au kwenda kwa tiba asili.

"Ule ni uvimbe unaoharibu taya linatanuka na kufika mahali kunakuwa na uvimbe mkubwa, wito wetu mtusaidie wanapoona wana uvimbe mbalimbali mdomoni, wawahi vituo vya afya wapate matibabu kabla ya hali haijafika kuwa mbaya."

Alisema mtu akifika hospitali akiwa na uvimbe mkubwa kinachofanyika, taya litaondolewa kwa kuwa hakuna namna nyingine ya kufanya.

"Mtu yeyote akiona tatizo kwenye eneo lake la mdomo aje kwetu matibabu yapo awahi," alisisitiza.

Pia aliwataka wanaokwenda hospitali kwa shida ya meno, wanapomuona mtaalamu wa kinywa na meno wasiseme wamekwenda kung'oa jino bali kutibiwa, ili daktari atumie utaalam wake kuona litapewa matibabu gani.

Kadhalika, aliwakumbusha wazazi na walezi kuwa meno ya utotoni yanayopaswa kung'oka ni 20 na kufanya hivyo kulingana na umri wa mtoto wakati wa ukuaji wake.

"Meno ya utotoni yapo 20 na ya ukubwani yapo 32 kwa hiyo yale 20 ambayo huanza kuota kwa mtoto mwenye umri wa miezi mitano mpaka sita mpaka miaka miwili huota, yote hutakiwa yatoke.

"Mtoto anapoendelea kukua na meno yake akifikisha umri wa miaka mitano au sita meno ya mbele huanza kulegea na gego la ukubwa ndipo huota, magego ya utoto yote yanatakiwa kutoka, lile kuanzia umri wa miaka sita ndilo hubaki," alisisitiza.

Alisema kama jino halijalegea, lile la ukubwa muda wake ukifika litasukumwa na utokaji wa meno ya utotoni huenda mpaka miaka kumi.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rushwa idhibitiwe katika uchaguzi viongozi wa CCM

**HALMASHAURI** Kuu ya CCM Taifa (NEC), juzi ilitangaza majina ya wagombea wa nafasi ya wenyeviti wa chama hicho ngazi ya wilaya katika uchaguzi utakaofanyika mwishoni mwa wiki hii Tanzania nzima. Viongozi watakaochaguliwa katika kinyang'anyiro hicho, wataungana na wengine katika ngazi za mashina, matawi na kata kwa ajili ya kujenga chama hicho.

Kabla ya hatua hiyo, kulikuwa na sarakasi nyingi kuanzia kwenye ngazi za matawi kiasi cha baadhi ya maeneo kutakiwa kurudia uchaguzi huo. Hata katika baadhi ya maeneo uchaguzi ulifutwa na kuagizwa mchakato kuanza upya.

Madai ya kuwapo kwa viongozi walioko madarakani kuwafanyia fitina wanaojitokeza kuwania na wengine kufutwa pamoja na kuwapo kwa tuhuma za rushwa zilitanda katika vyombo vya habari. Hatua hiyo ilisababisha baadhi ya viongozi wakuu wa kitaifa katika ziara zao mikoani kukemea vikali na kuweka bayana kwamba watakaokiuka maadili watachukuliwa hatua.

Pia kukithiri kwa rafu hizo, kuliripotiwa kuwa zaidi ya wanachama 400 wa Kata ya Mahina, Nyamagana mkoani Mwanza, walitishia kurudisha kadi za uanachama kutokana na kasoro mbalimbali za uchaguzi wa mashina 80 na matawi manane. Huo ni mfano mmoja tu ni jinsi gani kulikuwa na rafu katika uchaguzi huo ngazi za awali kabla ya hatua ya wilaya.

Katika kutangaza majina ya walioteuliwa kugombea uenyekiti na nafasi zingine katika ngazi ya wilaya, kumekuwa na mabadiliko makubwa kutokana na baadhi ya waliokuwa wakishikilia nafasi hizo kuenguliwa. Hilo linajidhihirisha kwamba hatua dhidi ya baadhi ya waliojihusisha na ukiukwaji maadili zimechukuliwa.

Hiyo kwa kiasi kikubwa ni dhahiri kwamba inatokana na kauli aliyoitoa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, aliyesema wanafuatilia kwa karibu madai hayo na hatua zitachukuliwa kwa waliokiuka.

Ni imani kwamba chama kilipokea ripoti mbalimbali zilioeleza mazuri na kasoro, hivyo kuchukua hatua ikiwamo kuwaengua wale waliojihusisha na tuhuma za rushwa na upangaji wa safu za uongozi hasa kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka 2025.


Kwa kufanya hivyo, CCM inastahili pongezi na inaonyesha kuwa imedhamiria kwa vitendo kukomesha rushwa na ukiukwaji wa kanuni na maadili ya chama katika kupata viongozi bora kuanzia ngazi ya shina hadi taifa. Pamoja na pongezi hizo, ni vyema CCM ikafanya jitihada zaidi kuanzia sasa hasa kipindi hiki cha uchaguzi wa chama kuanzia ngazi ya wilaya kwa kuwa huko ndiko nguvu ya fedha inatumika zaidi. Kwa mantiki hiyo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), inapaswa kuongeza nguvu zaidi kuhakikisha uchaguzi unaoanza kesho hadi keshokutwa unafanyika kwa uhuru na haki.

Tunasema hivyo kwa sababu kama kutakuwa na rafu kwenye uchaguzi huo, ikiwamo watu kupata uongozi kwa njia za rushwa, kuna uwezekano mkubwa kwa chama hicho ambacho kimejijengea umaarufu ndani na nje ya nchi na kuwa na wafuasi wengi, kupata viongozi wabovu.

Matokeo yake, uchaguzi huo unaweza kuibua mpasuko mzito ndani ya chama, hivyo kusababisha safari ya kuelekea 2025 kuwa ngumu katika baadhi ya majimbo, jambo ambalo litaigharimu CCM wakati huo ukifika.

Bado tunaamini kwamba CCM bado ni chama imara ndani ya Tanzania ndiyo maana imekuwa ikiaminiwa kila uchaguzi unapowadia na kupewa kura za kishindo kuendelea kushika dola. Sifa hiyo isiharibiwe na watu wachache hasa wanaotaka uongozi kwa kutumia fedha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bei hizi za vyakula zinazotisha, hatua zikachukuliwe kudhibiti

Na Sabato Kasika

**MFUMUKO** wa bei za vyakula, ni moja ya mambo ambayo yamekuwa ni gumzo kwa Watanzania, baada ya kushuhudia unga wa mahindi, mchele, maharage na vitu vingine vikizidi kupanda bei kila uchao.

Kupanda bei kwa vyakula katika maeneo mbalimbali nchini, ingekuwa ni vyema kama kungedhibitiwa, kwani vinginevyo mfumuko huo, unaweza kusababisha baadhi kushindwa kumudu milo mitatu kwa siku.

Upandaji bei huo umesababisha mchele kuuzwa shilingi 2,800 hadi 3,000 kwa kilo, huku unga wa mahindi ukiuzwa kati ya shilingi 1,600 hadi 1,800 kwa kilo na maharage shilingi 1,800 hadi 3,000 kwa kilo.

Sio kipindi kirefu miezi ya nyuma, kilo moja ya mchele ilianzia shilingi 1,600 hadi shilingi 2,000 huku unga wa mahindi ukiuzwa shilingi 1,200 kwa kilo, maharage shilingi 2,200 hadi 2,400 kwa kilo.

Bei ni hiyo ninayoielezea kwa baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ikiwamo Mbezi Luis, lakini imepanda, hali inayotishia milo ya watu, hasa kutokana na ukweli kwamba wengi wao ni wale wa maisha ya kawaida.

Ingekuwa ni vyema kama Serikali ingefanya jitihada zaidi kwa ajili ya kudhibiti mfumuko huo wa bei, ili kuwapa Watanzania unafuu wa maisha, ni takriban kila kona ya nchi wanalalamikia upandaji huo wa bei ya vyakula.

Ninajua zipo sababu mbalimbali zinazotajwa kuchangia mfumuko huo, ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, pia baadhi ya wafanyabiashara wa nje ya nchi kuja kununua vyakula na kwenda kuuza kwao.

Kwa mfano, hivi karibuni wananchi mjini Bukoba, mkoani Kagera, walikaririwa na vyombo vya habari wakidai kuwa kuna wafanyabiashara kutoka nchi jirani wanaingia mkoani humo na kununua mazao yote.

> **Bei ni hiyo ninayoielezea kwa baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ikiwamo Mbezi Luis, lakini imepanda, hali inayotishia milo ya watu, hasa kutokana na ukweli kwamba wengi wao ni wale wa maisha ya kawaida**

Wakadai kuwa kuingia wafanyabiashara hao kutoka nje ya nchi, kumesababisha bei ya vyakula kuwa juu na kuwafanya wawe na wakati mgumu, kwa kuwa hawana uwezo wa kumudu gharama mpya.

Hatua hiyo pia imesababisha hata mamalishe na baadhi ya migahawa kupanda bei ya vyakula, hali ambayo kwa ujumla inaweza kufanya baadhi ya watu kujibana na kula mlo mmoja kwa siku.

Katika mazingira hayo, bado hakujawa na dalili ya bei kushuka, hivyo ingekuwa vyema kama chanzo cha mfumuko huo kingedhibitiwa na kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu, ili Watanzania waondokane na adha hii.

Mtaalamu mmoja wa uchumi anasema, mfumuko wa bei kama huo ambao unaonekana mwiba kwa wananchi, njia inayoweza kutumika haraka kuondoa makali yake ni kuongeza uwezo wa ununuaji wa mtu wa kawaida.

Kwamba hakuna njia ya mkato kwenye mfumuko wa bei, bali ni lazima watu wawe na kipato, kwa kuwa bila kipato, ni vigumu kwa mtu kuweza kununua bidhaa, hasa pale inapopanda bei.

Pia kunaelezwa kwamba, kuna haja kwa serikali kupunguza au uondoaji wa kodi kwenye bidhaa zote muhimu zilizoathirika na bei, hususani ngano, mafuta ya kula na sukari, ili kuwapa unafuu wananchi.

Lingine, Serikali inashauriwa kubana matumizi yake ili kufidia kufutwa kwa kodi au punguzo la kodi katika vyakula, kwa kuwa ni vigumu wananchi kukabiliana na mfumuko wa bei kama hakuna mbinu za kuwanusuru.

Upandaji bei umehusisha pia bidhaa zinazotokana na mazao ya chakula na vinywaji, na bidhaa za viwandani, ambazo siyo chakula. Hivyo kila upande ungetafutiwa ufumbuzi wake, ili kuwapa wananchi unafuu wa maisha.

# DC aelekeza nguvu vita ujangili

**Na Steven William,** IRINGA

SERIKALI wilayani Iringa imesema kuwa inaendeleza mapambano dhidi ya ujangili katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, alisema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari alioongozana nao katika hifadhi hiyo wakati wa ziara ya maofisa tarafa na watendaji wa kata.

Alisema mapambano ni ya kivita kama vilivyo vita vingine kwa kuwa kinachofanyika ni uhujumu wa kiuchumi ambao kama hatua hazitachukuliwa, maendeleo ya taifa na ustawi wa wananchi vitadorora.

Moyo aliagiza suala la ujangili liwe ajenda ya kudumu kwenye vikao vya maofisa tarafa na watendaji kata na kwamba atafuatilia taarifa za ujangili kwenye maeneo yao mara kwa mara kuona kama kuna jitihada wanazozifanya kupambana na vitendo hivyo.

"Ujangili wa sasa ni ujangili wa nyama ambazo zinauzwa kwenye maeneo yenu ya utawala tofauti na hapo awali, hivyo naamini taarifa hizo za ujangili ni rahisi kuzipata kama mtawajibika ipasavyo," alisema Moyo.

Mkazi wa Wilaya ya Iringa, Charles Mhilu, alisema mkuu huyo wa wilaya amekuwa akihamasisha viongozi wa kata na tarafa kupiga vita vitendo vya ujangili katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha sambamba na kutembelea hifadhi hiyo na kujionea maajabu yaliyomo.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi na Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Godwell Meng`ataki, alisema kuna baadhi ya wananchi kwa makusudi wamekuwa na nia ovu ya kumaliza rasilimali za wanyamapori kwa kufanya ujangili jambo ambalo halikubariki kwa jamii.

Meng`ataki alisema hali ya ujangili inazidi kuongezeka kutokana na wanajamii kuendelea kuwaficha wahalifu.

Aisema agenda ya kupinga ujangili iwe kipaumbele kila wakati kwenye vikao vya serikali na visivyo vya kiserikali kwa lengo la kuendelea kutoa elimu ya kupinga vitendo hivyo vinavyofanywa na wananchi wanaoizunguka hifadhi hiyo.

**Meng`ataki alisema hali ya ujangili inazidi kuongezeka kutokana na wanajamii kuendelea kuwaficha wahalifu.**



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, akizungumza na viongozi na wananchi wakati wa makabidhiano ya hundi na kushuhudia utiaji saini mkataba wa uhifadhi mazingira na wanyamapori kati ya Lion Landscapes na Serikali ya Kijiji cha Kitisi, Kata ya Idodi, wilayani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wahariri wanawake Afrika wang'ara tuzo WIN

**Na Mwandishi Wetu,** ZARAGOZA

TAASISI inayosaidia vyombo vya habari duniani WAN-IFRA Women in News (WIN), imewatunuku tuzo za umahiri wa uongozi bora wanawake viongozi katika vyombo vya habari.

Kati ya wanahabari hao waliotunukiwa tuzo hizo jana mjini Zaragoza, Hispania, ni wahariri watatu kutoka Zimbabwe, Lebanon na Philippines.

Mhariri wa Zimbabwe Independent, Faith Zaba, alitangazwa mshindi wa tuzo hiyo ya Laureate kutoka Afrika pamoja na Diana Moukalled, mmoja kati ya waanzilishi wa chombo cha habari cha Daraj kutoka Lebanon, ukanda wa nchi za Kiarabu na Regina "Ging" Reyes, Makamu Rais na Mkuu wa kitengo cha habari ABS-CBN kutoka Philippines.

Tuzo hizo zinazotolewa kila mwaka zinazojilikana kama 'The Annual WIN Editorial Leadership Award', zinatambua mchango wa mfano wa kuigwa wa wahariri wanawake katika vyumba vya habari na mchango wa chombo chake katika uwasilishaji taarifa kwa jamii.

Washindi wengine watatu wa tuzo hizo wa mwaka 2019, 2020 na 2021, walikabidhwa katika sherehe hiyo iliyoambatana na kongamano la 73 la dunia la vyombo vya habari, kutokana na kutokuwapo kwa sababu ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Kwa mwaka 2020, walioshinda ni Mary Mbewe kutoka Zambia, Anna Nimiro (Sudan Kusini), Edyth Kambalama (Malawi), Samia Nakhoul (Lebanon) na Nyein Naing wa Asia Kusini.

Akiwapongeza waliopata tuzo hizo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa WAN-IFRA, Vincent Peyregne, alisema umuhimu wa vyombo vya habari katika utoaji taarifa husaidia kujenga mazingira mazuri katika nchi yoyote duniani.

Waliopata tuzo hizo, alisema wameonesha utofauti katika utendaji kazi wao wakiwa viongozi wanawake kwenye vyombo vyao vya habari. Alisema katika ubora wa uwasilishaji habari ni njia inayoleta afya katika jamii.

"Tuzo hizi ni ujumbe kwa waaandishi wanawake vijana wenye ndoto ya kuleta mageuzi na kujiunga kwenye sekta hii muhimu kuwa hata wao wanaweza kushika nafasi," alisema.

Hata hivyo, alisema mtu lazima ajitume, aonyeshe kujitoa kwake na kukwepa vizingiti vinavyowakwamisha wanawake kusonga mbele.

Akishukuru kwa tuzo hiyo, mmoja wa washindi kutoka Zimbabwe, Zaba, aliwataka waandishi wanawake vijana kutokata tamaa, kwa sababu wanathamani na wanaweza kufanya vizuri wakidhamiria.

Washindi wa tuzo hizo huchaguliwa na wanachama wa WIN kupitia kamati tendaji ambayo huangaliza vigezo kadhaa ikiwamo utendaji katika chumba cha habari kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na kusaidia kizazi kijacho cha uongozi kwenye vyumba vya habari.

## KABWELA



# Mradi wa bil. 699/- kuibua fursa ajira kwa Watanzania

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Mkinga mkoani Tanga wenye thamani ya Sh. bilioni 699 unatarajiwa kutekelezwa na kuongeza fursa nyingi za ajira kwa Watanzania.

Mradi huo unatarajiwa kuleta mabadiliko katika maendeleo ya kiuchumi na ushirikiano barani Afrika.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Siginon Logistics E.A Limited, Ali Mohammed, alisema kampuni hiyo imetengeneza mazingira mazuri na rafiki ili kuruhusu uwekezaji kwa kushirikiana na mashirika ya serikali.

"Katika kipindi cha wiki mbili, mwekezaji mwenye nia ataweza kupata kibali cha kuwekeza katika mradi huu baada ya kuzingatia masharti na vigezo vilivyoko. Tunatarajia kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza, mwanzoni mwa mwaka 2023 na tunawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kutumia fursa hii," alisema.

Pia alisema serikali ya Tanzania itanufaika na uwekezaji huo wa kigeni na kuifanya kuwa miongoni wa nchi zenye maendeleo makubwa ya kiuchumi kwenye nchi za Afrika.

Alisema Mkoa wa Tanga utakuwa na mabadiliko makubwa kwa kupata faida ya ajira na ukuaji wa uchumi vilevile kuwa kitovu cha biashara, baharini na usafiri wa anga.

Mradi huo, alisema una teknolojia za kiwango cha kimataifa kama akili bandia yaani, biashara ya mtandaoni (e-commerce) na biashara ya kidijitali na kuifanya kuwa ya kipekee katika eneo hilo.

"Mradi huu unalenga kujenga miundombinu muhimu kwa Mkinga ili kuimarisha uchumi na kujenga msingi wa maendeleo kwa kuzingatia mikataba kati ya mataifa ya Afrika kama vile AfCFTA, EAC, SADC, AGOA na mikataba mingine mingi," alisema. Alisema hadi sasa jumla ya wawekezaji watano kutoka mataifa mbalimbali wameonyesha nia ya kuwekeza fedha, ikiwamo Brazil, Misri, Tunisia, Bulgaria, GCC, Philippines na India.

Kwa mujibu wa Mohammed, Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 zenye uchumi unaokua kwa kasi barani Afrika na kwa miaka 10 iliyopita, uchumi wa nchi ulikua kwa wastani wa asilimia saba.

"Julai, 2020 Benki ya Dunia (WB) iliipandisha rasmi nchi ya Tanzania na kuwa nchi ya kipato cha kati mafanikio haya yanaweza kuhusishwa na utulivu wa kisiasa na kiuchumi, sera na viongozi wazuri, pamoja na umoja na amani," alisema.

Alisema kwa kutumia akili bandia yaani 'artificial intelligence' (AI), teknolojia ya usambazaji data (Blockchain Technology) itatumika na leseni za biashara za kawaida, kuruhusu kampuni kutoka duniani kote kuungana na kufanya biashara kutokea Dubai.

Alisema kutakuwa na aina mpya ya biashara kupitia mtandao inayojulikana kama 'smart commerce', ambayo hutumia akili bandia na mitandao itakayoendesha uvumbuzi ndani ya minyororo ya ugavi.

Mitandao hiyo, alisema itawezesha kampuni zote za kimataifa na kampuni ndogo na za kati kuanzisha biashara za kidijitali huko Dubai katika maeneo ya bure bila haja ya kuwa huko kimwili kwa kuanzisha kampuni pepe (Virtual Company).




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Emmanuel Mjema (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu harambee ya kuchangisha fedha za ujenzi wa mabweni ya wasichana kwenye kampasi ya chuo hicho mkoani Mbeya, iliyofanyika Jumamosi iliyopita. Kulia ni Mkurugenzi wa Shahada za awali wa chuo hicho, Dk. Shima Banele na Naibu Mkuu wa chuo, Mipango na Fedha, Dk. Emmanuel Munishi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Stanbic yazindua huduma maalum kwa wajasiriamali

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Stanbic Tanzania, imezindua huduma maalumu kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na kati, iitwayo 'Mpambanaji'. Kauli mbiu ya huduma hiyo ni 'Tunakuwezesha Kukuza Biashara Yako' inayolenga wajasiriamali kufikia huduma za benki kirahisi na kupata fursa za uwekezaji nchini, kikanda na kimataifa.

Katika taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari, ilieleza kuwa, uzinduzi huo ulifanyika mkoani Mwanza juzi.

Mpambanaji inajumuisha huduma mbalimbali ikiwamo Akaunti mahususi kwa wajasiriamali (akaunti ya Mpambanaji mmoja mmoja, vikundi, na Saccos), huduma ya kujenga uwezo/kuelimisha, huduma za kibenki bila mipaka, mikopo ya vyombo vya usafiri, huduma za bima, huduma ya kufanya biashara kati ya Tanzania na China, pamoja na huduma mpya ya Wakala wa Benki yenye zaidi ya mawakala 500 wanaoongeza uwapo wa huduma za benki nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara, Fredrick Max alisema:

"Sekta ya biashara ndogo na kati ni zaidi ya asilimia 70 ya sekta binafsi na inatoa ajira kwa zaidi ya watu milioni nne, kwa hiyo ina mchango mkubwa katika kuchangia uchumi wa Tanzania ikiwa zitarasimishwa."

Alisema: "Ndio maana kama taasisi ya fedha tumetambua umuhimu wa kuleta suluhisho ambalo ni zaidi ya usaidizi wa kifedha, kwa kuja na suluhisho ambalo litahakikisha wafanyabiashara wana zana wanazohitaji ili kuanzisha biashara endelevu na zenye faida."

Mkuu wa Kitengo cha wateja binafsi, Omari Mtiga, aliweka wazi kuwa benki itaendelea kutafuta ufumbuzi pamoja na kubuni huduma zitakazokidhi kiu ya wateja wao.

Aliongeza wajasiriamali wanaweza kufungua akaunti ya Mpambanaji kwa kutumia TIN namba pamoja na Kitambulisho cha Taifa (NIDA).

Vilevile, akaunti hii haitakuwa na ada ya mwezi na kupitia akaunti hiyo mteja ataweza kuweka fedha, kutoa fedha na kufanya malipo.

# Ataka usafi endelevu kuepusha magonjwa

**Na Jenifer Gilla**

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Temeke, Dk. Joseph Kimaro, amewataka wakazi wa Keko, Manispaa ya Temeke, kuweka mazingira usafi ili kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitatu kwa kuwa wengi huathirika kwa kuhara kutokana na kula uchafu.

Pia amewataka wakazi hao kuacha kutupa taka katika makaburi ya eneo hilo na kutoa rai ya kujijengea utamaduni wa kusafisha maeneo hayo mara kwa mara.

Dk. Kimaro aliyasema hayo wiki iliyopita, alipowaongoza wakazi hao kufanya usafi katika mitaa yao ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Usafi wa Mazingira Duniani yaliyoandaliwa na Manispaa ya Temeke kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali zikiwamo, TCCI, Mazingira Plus, HUDEFO na ETE Worldwide Solutions. Aidha, alisema amefurahishwa na ushiriki wa wadau mbalimbali katika usafi huo na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa kwenye sekta ya afya kwa kuwa Hospitali ya Temeke imeongezewa vifaa tiba na mashine mbalimbali hivyo huduma zimezidi kuimarika.

Ofisa Habari TCCI Mazingira, Godwin Innocent, alisema ukiacha kufanya usafi wanaadhimisha siku hiyo kwa kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutunza mazingira na kuwahimiza wajijengee utamaduni wa kufanya usafi katika maeneo yanayowazunguka bila kusukumwa.

"Tunataka ifike mahali wakazi wa eneo hili kila ikifika Jumamosi wakusanyike na kufanya usafi katika maeneo ya jumuiya ikiwamo makaburini, kwenye vituo vya daladala, hospitalini na hata pembezoni mwa shule. Hatutachoka mpaka tuone adhima hii imekamilika," alisema.

Mkurugenzi wa Asasi ya Utu na Mazingira, Sarah Pima, alisema maadhimisho hayo ni muhimu kwao kwa sababu yanawakumbusha wajibu wa kutunza mazingira, ili yawe safi muda wote kujiepusha na maradhi ikiwamo kipindupindu.

Alisema hali usafi wa mazingira kwa sasa imeimarika ukilinganisha na miaka ya nyuma kwa sababu ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa mazingira za kuhamasisha utunzaji wa mazingira hayo.

"Hali ya mazingira kwa sasa inaridhisha, ndio maana unaona hata maradhi ya milipuko yamepungua, tunaishukuru sana serikali kwa kutupa nafasi ya kushiriki kwenye uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira yetu sisi kama wadau hatutachoka kutetea afya zetu na watoto wetu zinazoathiriwa na mazingira machafu," alisema Sarah.

## HABARI KITAIFA

## TBS, TMEA zaingia mkataba wa bil. 9/-

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetia saini mkataba na Kampuni ya Trade Mark East Africa (TMEA) utakaogharimu Sh. bilioni tisa kwa lengo la kuhakikisha wafanyabiashara wanawezeshwa kufanya biashara kulingana na viwango vilivyowekwa na kuingia kwenye masoko.

Mkataba huo wa miaka mitatu ulitiwa saini juzi Makao Makuu ya TBS, Dar es Salaam baina ya shirika hilo na TMEA.

Akizungumza baada ya kutiwa saini kwa mkataba huo, Mkurugenzi Mkazi wa TMEA, Monica Hangi, alisema makubaliano hayo yanalenga kurahisisha biashara na kukabiliana na changamoto ili kupunguza vikwazo vya kibiashara na visivyo vya ushuru nchini.

Hangi alisema ni vigumu mtu kuuza bidhaa zake kwenye soko kama hajafikia kiwango kinachotakiwa.

"Kwa hiyo tupo hapa kutia saini huu mkataba katika kuendeleza kazi ambayo tulishaianza na juhudi hizi zinarahisisha biashara na zimewekwa, ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza ikiwamo kupunguza vikwazo vya kibiashara na visivyo vya ushuru nchini," alisema.

Wafanyabiashara walisema bado wanakabiliwa na changamoto za kuzingatia viwango na hiyo kwa kiasi kikubwa inatokana na uelewa mdogo na gharama kubwa, hali inayopunguza uwezo wa kutumia masoko ya kikanda na kimataifa kwa mauzo ya nje.

Alisema pamoja na changamoto hizo, TBS imekuwa mmoja wa washirika wakuu na imeonyesha uwezo wa kuleta matokeo yanayoonekana katika miradi mbalimbali inayoungwa mkono na TMEA.

"Hivyo natoa wito kwa TBS tuendelee kushirikiana kuhakikisha awamu hii ya mradi inaenda kuwa na mafanikio makubwa," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, aliishukuru TMEA kwa juhudi kubwa na msaada unaotolewa, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na utekelezaji wa viwango vyote viwili vya hiari na vya lazima kwa lengo la kuwezesha biashara.

Pia aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa hali ya juu katika utekelezaji wa miradi inayokuja kwa manufaa ya maendeleo ya uchumi wa nchi.

"Miundombinu ya viwango na ubora ina jukumu kubwa kuelekea kizazi cha nne cha viwanda. Kwa hiyo kusaidia shughuli za viwango na ubora wa miundombinu ni kusaidia hatua kuelekea kizazi cha nne cha viwanda," alisema.

# Balozi aonya kampuni kusafirisha wafanyakazi bila kufuata sheria

**Na Jenifer Gilla**

BALOZI wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Mwadini, amesema kampuni zinazosafirisha Watanzania kwenda nchini humo bila kufuata utaratibu wa kisheria, zitachukuliwa hatua.

Pia amesema ubalozi unafuatilia na kuchukua hatua kwa Watanzania wanaopitia matatizo mbalimbali nchini humo, ikiwamo kunyanyaswa na waajiri na kuwataka kutumia kampuni zilizosajiliwa ili iwe rahisi kuwasaidia wanapopata changamoto.

Aliyasema hayo juzi katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika kwa njia ya mtandao kuhusu fursa zinazopatikana nchini humo na kuwataka Watanzania wanaokwenda kufanya kazi kufuata taratibu za ajira. "Kuna watu wanapata fursa hizi kipembeni pembeni (kwa njia zisizo rasmi), ni muhimu ukiipata fursa hii uirasimishe. Nenda TAESA (Wakala wa Huduma za Ajira-Tanzania) kuhakiki kuwa aliyekupa hiyo fursa amesajiliwa, anatambuliwa serikalini na ubalozi. Ili kukulinda wewe lazima tujihakikishie kuwa hiyo kampuni imesajiliwa na serikali na inatambulika," alisema.

Pia alisema ni muhimu wakala wa ajira hizo akasafirisha wafanyakazi walio katika viwango kwa sababu wengi hupitia changamoto hizo kwa kuwa hupelekwa wakiwa nchi ya viwango tofauti na matarajio ya waajiri wao.

"Shida nyingine ni mawakala hao kuwatoza fedha wafanyakazi na kuwapa ahadi zisizo sahihi. Hili pia husababisha tatizo la kisaikolojia kwa sababu akifika hapa anaona kwanza nimetoa pesa halafu mshahara wenyewe sio nilioambiwa," alisema.

Aidha, Balozi huyo alisema Tanzania imewafungilia njia wananchi kupata kazi nje ya nchi kwa kuwajengea uwezo kwa vitendo kupitia vituo vingi vinavyotoa elimu kwa vitendo, ikiwamo Mamlaka ya Elimu na Mafunzi ya Ufundi Stadi (VETA).

"Nimebahatika kutembelea nchi takribani 25 za Kiafrika sijaona vitu vya aina hii kwa nchi nyingi, haya yote yanamtengeneza Mtanzania fursa za nje. Wapo vijana wengi ambao wametumia fursa hizi kujiimarisha kiuchumi," alisema.

Aidha, Balozi Ali alisema nchi hiyo pia ni miongoni mwa wazalishaji bidhaa zinazoongoza katika soko la dunia, ikiwamo nazi, ufuta, karafuu, hiliki, ndizi na bidhaa za madini kama vile dhahabu na kuwataka Watanzania kutumia fursa hiyo kujiongezea kipato.

"Kwa mfano makapi ya nazi yanatumika kutengenezea sabuni, nta au masega ya nyuki nayo ni mali, mabibo ya korosho pamoja na maganda yake ni mali, yanaweza kutengenezea malisho ya mifugo au mafuta wakati sisi tunatupa," alifafanua.

Alisema kuwa Saud Arabia ni nchi ya viwanda hivyo kuna fursa nyingi za kununua bidhaa ikiwamo pembejeo za kilimo na vifaa vya umwagiliaji pamoja na malighafi za kutengeneza vifaa vya plastiki pamoja kuuza asali, maji ya matunda, samaki na nyama.

"Miongoni mwa mambo tuliyofanikiwa katika kipindi hichi cha uongozi wa Rais Samia Hassan ni kufungua tena soko la nyama kati ya Tanzania na Saudi Arabia ambalo kwa takribani miaka 21 lilikuwa limefungiwa na kampuni mbili za Kitanzania zimeruhusiwa kuuza nyama hapa nchini," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya (katikati), akijaribu ubora wa moja ya matrekta yatakayotolewa zawadi kwa washindi wa msimu wa pili wa kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' mahususi kwa wakulima wa zao la korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi, katika uzinduzi mjini Mtwara jana. Wanaoshuhudia ni viongozi waandamizi wa benki hiyo, akiwamo Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo, Elibariki Masuke (wa tatu kulia) na wadau wa zao hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yaanza kampeni kuinua kilimo korosho

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imezindua msimu wa pili wa kampeni maalum kwa wakulima wa zao la korosho mikoa ya Mtwara na Lindi inayofahamika kama Vuna Zaidi na NBC Shambani.

Lengo ni kuunga mkono na kufanikisha adhma ya serikali ya kuzalisha tani 700,000 za zao hilo kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, aliongoza juzi hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo iliyofanyika mkoani humo leo na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa zao hilo wakiwamo viongozi wa kiserikali, viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) na vyama vikuu vya ushirika, maofisa wa Benki ya NBC wakiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo wa NBC, Elibariki Masuke.

Alisema imekuja wakati muafaka kwa kuwa inakwenda sambamba na mpango wa serikali wa kuhakikisha sekta ya kilimo inachangia pato la taifa kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

"Na ndiyo sababu nawapongeza sana Benki ya NBC kwa mkakati huu ambao hapo tu kimasoko bali pia unaunga mkono jitihada za serikali kukuza sekta hii muhimu na pia inalenga kumkomboa mkulima. Wito wangu kwa wakulima wa korosho mkoa wa Mtwara na Lindi naomba sana tuwaunge mkono NBC kwenye hili," alisisitiza.

Akizungumzia zawadi mbalimbali zinazotolewa kupitia kampeni hiyo ikiwamo trekta, maguta (Toyo), baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa simu janja, kanga, mabegi na madaftari, Kyobya alisema zinalenga kuunga mkono jitihada za mkulima katika kuboresha kilimo na uzalishaji hatua ambayo ina tija zaidi kiuchumi katika mkoa huo.

"Msisitizo wangu tu kwa wakulima ni suala zima la nidhamu ya fedha na kutumia vema mafunzo yanayotolewa na Benki ya NBC kuhusu umuhimu wa kujiwekea akiba, matumizi ya bima mbalimbali ikiwamo bima ya afya pamoja na kuwekeza kwenye zana za kisasa za kilimo,"alisema.

Kwa upande wake, Masuke alisema msimu wa pili wa kampeni hiyo ya miezi mitatu ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kujizatiti kwenye kuinua kilimo cha mazao ya kimkakati, ikiwamo zao la korosho kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara.

"Tunashukuru kuona kwamba kampeni yetu ya mwaka jana ilipokewa vizuri sana na wakulima wa korosho katika mikoa hii ya Lindi na Mtwara na zaidi tunajivunia kuona kwamba kampeni ile ilimalizika kwa mafanikio kwa wakulima ambapo tuliweza kukabidhi kwa wakulima zaidi ya 150 ambapo tulikabidhi jumla ya pikipiki 25, pampu za umwagiliaji zaidi ya 60, baiskeli 70, na trekta moja. Ni matumaini yetu mwaka huu mambo yatakuwa mazuri zaidi," alitaja.

Alisema katika kampeni ya mwaka huu wakulima hao pia watakuwa kwenye nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa na zawadi za kifamilia ikiwamo simu janja, kanga, mabegi na madaftari."

"Kwa upande wa vyama vya msingi (AMCOS) vinaweza kujishindia zawadi kubwa zaidi ikiwamo maguta (Toyo) pamoja na matrekta, ili walengwa hawa wote waweze kujishindia zawadi hizi wanatakiwa wafungue akaunti benki ya NBC na wapitishe fedha za malipo yao kwenye akaunti hizo na moja kwa moja watakuwa wameingia kwenye droo ya kujishindia zawadi hizi," alifafanua.

# Bil. 1/- zatengwa ubunifu kwa vijana

**Na Faustine Feliciane**

UBALOZI wa Ufaransa nchini kupitia Mfuko wa Mshikamano wa Serikali ya Ufaransa (FSPI), umetenga Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya miradi ya ubunifu kwa vijana wa Tanzania.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi wa SANAAPRO utakaosaidia tasnia ya ubunifu nchini, Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Nabil Hajlaoui, alisema uamuzi huo unatokana na ahadi ya rais wa nchi hiyo, Emmanuel Macron aliyoitoa kwenye mkutano wa 'New Africa France' uliofanyika Oktoba, mwaka jana kwenye mji wa Montpelier nchini humo.

Rais huyo alizungumzia ubunifu kwa vijana wa Afrika ndiyo maana ubalozi umeona kuna aja ya kuwekeza kwenye tasnia ya ubunifu kuwapa fursa vijana kujipambanua kwa miradi itakayowawezesha kupiga hatua kimaisha.

"Ubunifu umekuwa sekta ya kimkakati ya kuvutia vijana ili kuongeza ushindani, tija, ajira na ukuaji endelevu wa uchumi, mradi huu unalenga kuwainua vijana ambao watabuni mambo mbalimbali yenye tija na kupewa uwezo wa kutekeleza," alisema Hajlaoui.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili 2022-2023 shughuli mbalimbali za mradi huo zitatekelezwa huku walengwa wakiwa mashirika manane ya hapa nchini yatakayofanya kazi na mashirika mengine matano kutoka Ufaransa.

"Mashirika ya hapa Tanzania ni ASEDEVA (Sanaa ya kimaendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika), MUDAFRICA, CAC kutoka Arusha, Tuna-Present Tanzania, AJABU AJABU, DCMA- Zanzibar, Kito cha kiutamaduni cha Ufaransa-Dar es Salaam pamoja na FCS," alisema Hajlaoui.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo kutoka MUDAFRICA, Rachel Kessy, alisema mradi huo utawasaidia vijana wa kitanzania wenye ndoto za kufikia mafanikio kwa ubunifu wanaoufikiria.

"Mradi huu umekuja katika kipindi sahihi kwa vijana, ubunifu wao utawapa mafanikio kwa fedha hizi ambazo Ubalozi wa Ufaransa wametoa," alisema Rachel.

Aidha, Mkurugenzi wa ASEDEVA, Isack Abeneko, alisema mradi huo pia utawahusisha wanawake na watu wenye ulemavu ambao nao watanufaika na mradi huo.

"Tunawashukuru sana wenzetu wa Ufaransa na nafasi hii, ASEDEVA hii ni nafasi kubwa ya kuwafanya vijana kufikia malengo yao hasa wale wenye ubunifu," alisema Abeneko.

Mradi huo ulizinduliwa jana na Balozi Hajlaoui utadumu kwa kipindi cha miaka miwili na kumalizika mwaka 2023.



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James (kulia), akimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Songas, Anael Samuel, wakati wa sherehe ya kutimiza miaka 10 ya Mafunzo kwa Vitendo ya Viwanda (IPT) ya kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam juzi jioni. IPT ilizinduliwa mwaka 2011 ikitoa ujuzi na taaluma kwa vijana 140 katika maeneo kama vile matengenezo, uendeshaji na uhasibu, TEHAMA na ugavi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miaka 40 sheria si rafiki kwa mwandishi wa habari

**Na Jenifer Gilla**

MJUMBE wa Kamati Tendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, amesema ni wakati serikali kubadilisha Sheria ya Habari kwa kuwa imekuwa si rafiki kwa wanahabari tangu mwaka 1979.

Aidha, amesema kwa miaka 40 sheria hiyo ilitoa mwanya kwa mtu mmoja kuamua kufungia chombo cha habari, hata ile iliyotungwa mwaka 2016 imefanya kazi hiyo kwa kuhamisha mamlaka pekee.

Alisema hayo alipozungumza katika kipindi cha redio na kuongeza kuwa Sheria ya Mwaka 2016 ilianza kulalamikiwa kwa kuwa haikuondoa mitego iliyowekwa na Sheria ya Mwaka 1979 hali iliyochangia kudumaa kwa vyombo vya habari nchini.

"Hata Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 ilipotungwa, imefuata mkondo huo huo wa kutoa mamlaka kwa mtu mmoja kuamua kufungia chombo cha habari au la ingawa mamlaka hayo amepewa Mkurugenzi wa Idara ya Habari Malelezo! Katika mabadiliko haya, tumeiomba serikali iondoe kipengele hicho," alisema Meena.

Meena pia alisema baada ya wadau wa habari kupiga kelele, serikali ya awamu ya sita iliona haja ya kukaa meza moja na wadau wa habari ili kupatia ufumbuzi na hatua za awali alizochukua Rais Samia Suluhu Hassan, ziliongeza ari ya wadau wa habari kushirikiana ili kung'oa vipengele hasi vya sheria ya habari.

"Mwaka jana mwishoni mwa mwezi wa sita, tulikutana na rais (Rais Samia) na akasema yuko tayari kushughulikia malalamiko yetu. Hatua zilianza kuchukuliwa kwa serikali kuleta mapendekezo ya maeneo ya kurekebisha, lakini na sisi tuliongeza yetu ambayo wao walikuwa hawajaweka kwenye mapendekezo yao,"alifafanua.

Aidha, mjumbe huyo alisema wadau wa habari wanachopambania ni kuhakikisha inapatikana sheria rafiki kwa wanahabari na wamiliki wa vyombo vya habari nchini. Kama kuna sheria zinazonekana kuwa mbaya na hazijatumika, sheria hizo hazipaswi kuwapo kwa kuwa zinatoa mwanya kwa anayetaka kuzitumia kufanya hivyo.

"Kuna sheria zingine zipo na inaelezwa hazijatumika. Sheria kama hizo hazipaswi kuwapo maana anaweza kutokea mtu mmoja akazitumia na tukawa hatuna cha kusema. Kikubwa katika tasnia ya habari kila mmoja atekeleze majukumu yake, serikali ibaki na majukumu yake na wanahabari kama wanataaluma wabaki na majukumu yao," alisema.

Meena alitoa mfano wa baadhi ya magazeti yaliyolalamikiwa kuandika vibaya lakini hayakuwahi kufungiwa, lakini mengine yalifungiwa kwa kuwa tu sheria ya kufanya hivyo ilikuwapo.

## Bashe aipa jukumu TARI

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo,Hussein Bashe, ameipa miaka mitatu Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania(TARI), kumaliza tatizo la upungufu wa mbegu bora nchini kwa kuanza na mazao ya kimkakati.

Aidha, ametoa mwaka mmoja kwa bodi hiyo kuhakikisha inamaliza tatizo la mbegu kwa zao la mahindi kwa kuwa ni aibu kutojitosheleza na kutegemea kuagiza kutoka nje, ili hali uwezo wa kuzalisha kwa kutumia wataalam wa ndani upo.

Waziri Bashe alitoa agizo hilo hivi karibuni jijini Dodoma,wakati akizindua bodi hiyo wakurugenzi wa TARI chini ya Mwenyekiti Dk. Tausi Kida, aliyeteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Hassan Suluhu huku wajumbe wake wakiteuliwa na waziri huyo wa kilimo.

"Ninawapa pole sana kwa uteuzi mlioupata kwani mna kazi kubwa ya kufanya kwa nchi hii, moja ya kazi yenu kubwa ni kuhakikisha mnamaliza tatizo la upungufu wa mbegu nchini," alisema Waziri Bashe.

Aidha, aliitaka bodi hiyo kuachana na siasa kwakuwa serikali imeamua kulivalia njuga suala hilo la kumaliza tatizo la upungufu wa mbegu kwa kuongeza bajeti kwa TARI kutoka Sh. bilioni 11 hadi Sh. bilioni 40 katika bajeti ya mwaka wa fedha, ili kutatua changamoto za taasisi hiyo.

"Sio lazima kutatua tatizo la upungufu wa mbegu kwa mazao yote kwa wakati mmoja, lakini tunaweza kuanza na mazao ya kimkakati angalau kama 10 ndani ya miaka mitatu na baadae tukamaliza mengine," alisema Waziri Bashe.

Aidha, Waziri Bashe aliagiza bodi hiyo kuhakikisha inasimamia ujenzi wa uzio katika mashamba yote ya mbegu ya vituo vyote 17 vya TARI, ili viweze kuepuka na migogoro ya ardhi, ambayo watu wanaozunguka wanaingia kufanya shughuli za kilimo.

Waziri huyo wa Kilimo alisema imefika wakati sasa kwa TARI kufanya utafiti utakaojibu maswali ya wakulima, ili waweze kuongeza uzalishaji na sio kutoa maelezo ya kisayansi ambayo hayamsaidii mkulima.

Waziri Bashe aliagiza bodi hiyo kukutana mara moja na Bodi ya Wakala wa Taifa wa Uzalishaji wa Mbegu (ASA) na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) pamoja na menejimenti zao kukaa kwa pamoja na kupanga mikakati itakayotoa muelekeo wa kumaliza tatizo la upungufu wa mbegu hapa nchini.

Aidha aligiza TARI kuanza safari ya kuhifadhi mbegu za asili kwa kuzitambua, kuzisafisha na kuzitunza ili mkulima aweze kuchagua ataweza kutumia mbegu, ipi kama ya asili au ya kisasa katika msimu wa kilimo.

Alisema mpango wa serikali kwa ni kuhakikisha inajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yake ya mbegu hekta 800 katika mwaka wa fedha pamoja na ujenzi wa maghala matano kwaajili ya kuhifadhi mbegu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya TARI, Dk. Tausi Kida alisema wamepokea maagizo yote na kuhaidi kuyafanyia kazi mara moja, ikiwemo kumaliza tatizo la upungufu wa mbegu hapa nchini.

Dk Kida alisema kwa hivi sasa kilimo kimekuwa ni biashara hivyo ni lazima kuhakikisha wakulima wanaondolewa changamoto mbalimbali, ili kuweza kufikia malengo yalikusudiwa.

Alisema atahakikisha TARI itafanya utafiti ambao utajibu mahitaji ya sokoni, ili wakulima waweze kuongeza tija kwa kuzalisha mazao yanayohitajika sokoni kwakuwa hivi sasa kilimo ni biashara.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo alisema tayari wameshagundua aina 51 ya mbegu za kisasa ambazo zina uwezo wa kupambana na changamoto mbalimbali za wadudu na mabadiliko ya tabia nchi.



# DC apongeza viboko wakiukaji maadili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Richard Ruyango, amelipongeza kabila la Wameru kwa kuweka adhabu ya viboko 70 kwa wanaovunja maadili ya jamii hiyo, hali inayosaidia kurudisha vijana katika maadili na kushiriki shughuli za maendeleo.

Ruyango alitoa pongezi hizo jana wilayani humo wakati wa sherehe ya makabidhiano ya madaraka ya ulinzi wa jamii hiyo kimila kutoka rika la Kilowio kwenda rika la Oltuwati. Uongozi uliokabidhiwa utakaa katika kipindi cha miaka 12.

"Viboko 70 kama tumekubaliana mkapitisha na nikaona inafaa kurekebisha tabia, sina shida naridhia kwa sababu lengo si kiwakomoa bali kuwafanya watukutu wawe waadilifu. Naungana nanyi na ninawapongeza," alisema.

Katika jamii hiyo, alisema viboko vimesaidia vijana kuachana na ulevi uliokithiri na matumizi ya dawa za kulevya jambo ambalo ni zuri na linapaswa kuigwa na jamii zingine.

Pia alisema matumizi ya dawa za kulevya au ulevi wa kupindukia huchangia kuharibu vichwa vya watoto au vijana wadogo na kusababisha kushindwa kufanya kazi za maendeleo.

Alisema katika jamii hiyo, imekuwa tofauti na maeneo mengine kwa kuwa wao kutumia mila kurekebisha tabia na kuchangia shughuli za maendeleo jambo ambalo ni zuri na linapaswa kuigwa.

Sambamba na hilo, alisema baadhi ya jamii nchini zikijificha katika kivuli cha mila, kwa kufanya unyanyasaji wa kijinsia, hali hiyo imekuwa tofauti kwa jamii ya Kimeru mkoani Arusha, ambao wamekuwa wakipinga vikali ukatili dhidi ya wasichana, watoto na wanawake kwa kutumia mila.

Ruyango pia alipongeza rika la kilowio kwa kuchangia maendeleo mbalimbali ya jamii, ikiwamo kujenga darasa katika Shule ya Sekondari Uwiro, lenye thamani ya Sh. milioni 21 na kutumia sheria za kimila kupinga unyanyasaji wa kijinsia.

Kanaeli Elbariki, mwanarika kutoka Kilowio na Alex Wilfred ambaye ni mwanarika wa Oltuwati, alisema wamechanga Sh. milioni 21 na kujenga chumba kimoja cha darasa kwenye koo hiyo ili kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Walisema pamoja na kuchangishana fedha hizo, pia wajipanga kutafuta fedha za kutatua uhaba wa mabweni.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Uwiro, Remmy Mauki, alishukuru kwa msaada huo ambao licha ya kupunguza msongamano darasani, alisema utaongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, Maria Kitomari alikiri mila za jamii yao zimekuwa msaada mkubwa kwa kuzitumia kupinga vikali suala hilo.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha na Diwani wa Kata ya Laroi, Ojun'gu Salekwa akizungumza katika kikao kazi cha kuutambulisha mradi wa 'Boy's Vac Lab', wilayani Arumeru, mkoani Arusha juzi, unaofadhiliwa na Foundation for Civil Society, wenye lengo la kumjengea uwezo mtoto wa kiume kwa kujitambua, kujithamini ili kupambana na ukatili dhidi yao. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Wanafunzi wafundishwa kujiamini na kujitambua

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

SHULE ya Awali na Msingi Tarangire ya Mchepuo wa Kiingereza iliyoko Wang'waray katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imejipanga kutoa elimu ya thamani endelevu kwa wanafunzi ili wajiamini na kujiandaa kuiongoza nchi miaka ijayo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapo, Mkuu wa shule hiyo, Juma Ama, alisema lengo kubwa ni kuwapatia wanafunzi elimu ya thamani endelevu, ili wawe ni faida kwa taifa.

"Tunaamini tutakapowapa elimu ya thamani endelevu wanafunzi hawa wanaweza kujiamini na kujiandaa kupokea nchi na kuiongoza kwenye miaka ya baadaye," alisema.

Wanafunzi wa shule hiyo, walisema wana uwezo mkubwa wa kujiamini na kujisimamia, hivyo wazazi, walezi na jamii kwa ujumla iwapeleke watoto wakapate elimu Tarangire.

Pia alisema wanafunzi wanajiamini kutokana na elimu ya taaluma wanayoipata shuleni hapo kwani walishatoa madarasa matatu ya darasa la saba kwa ufaulu wa daraja la kwanza.

"Tarangire tuna madarasa 10, mabweni mawili, magari na mabasi sita, wafanyakazi 32 na tuna wanafunzi 400 pamoja na ambao wanaohitimu darasa la saba mwaka huu," alisema.

Alisema kupitia uwapo wa shule hiyo, majirani wa eneo hilo wamepata maendeleo mbalimbali ikiwamo matengenezo ya barabara, nishati ya umeme na maji.

"Pamoja na hayo hivi sasa tunatarajia kuanzisha Usharika wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ili kumtolea Mungu sadaka ya shukurani kwa mema yote aliyotujalia," alisema Ama.

# Wajinoa kuendesha shughuli za posta

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya wakuu 80 wa idara za usalama wa Shirika la Posta Afrika (PAPU) kutoka mataifa 50 barani Afrika, wameanza kujifua kuhusu mbinu bora za kuendesha huduma za kiposta kwa njia za kiusalama.

Mafunzo hayo ya siku tatu, yameandaliwa na Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania na PAPU.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohammed Abdullah, akizungumza jana jijini Arusha wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha huduma za posta zinazotolewa zinakuwa kwenye viwango vya usalama na kujenga uaminifu kwa wateja wanaotumia posta.

"Baada ya mafunzo haya nchi kupitia kwa wawakilishi wao kufaulu ili tupatiwe cheti cha kimataifa kitakachoitambulisha Tanzania kuwa tuko vizuri katika utoaji wa huduma za posta.

"Hatuna upungufu wowote lakini imetubidi kutoa mafunzo haya kwa kuwa dunia kwa kuwa awali tulikuwa tunafanya kazi kwa njia ya usalama wa kizamani na kwa sasa mambo yote yamehamia katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA. Hivyo na sisi tunatakiwa kubadilika na kwendana na kasi hiyo," alisema.


Pia aliwataka watumishi wa posta nchini, kufahamu kuwa kwa sasa dunia imehamia kwenye mfumo wa TEHAMA, hivyo ni lazima wabadilike baada ya kujengewa uwezo kwenye mafunzo hayo.

"Washiriki wanapaswa kuzingatia mafunzo kwa kuwa ni ya msingi na muhimu kwao, kwa kuwa yanawasaidia kuwajengea uwezo na ujuzi wakati wa utendaji kazi," aliongeza.

Awali, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo, alisema mafunzo hayo yatasaidia kutengeneza mazingira wezeshi kwa posta za Afrika kutafuta viwango vya ubora wa huduma za kiusalama kwa shughuli wanazofanya.

"Awali tulikuwa tukitoa huduma kwa njia za kizamani lakini kutokana na mabadiliko ya teknolojia, posta zote za Afrika zinapambana kubadilisha mifumo ya uendeshaji wa kutoa huduma kwa wananchi.

"Sisi kama wadau muhimu tumeona tushiriki katika mafunzo haya ili kujengewa uwezo kwa wataalamu wetu watusaidie kuweka mazingira wezeshi ya usalama katika mchakato wa hatua ya kuwahudumia wananchi," alisema.



# Wapata mafunzo umiliki wa ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

ZAIDI ya wanawake 100 wanaofanya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya Rombo na Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro, wameanza kufundwa kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi na uongozi.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwapa morali ya kutetea haki zao mbele ya jamii, inayoonekana kulipa kisogo suala la haki sawa.

Mafunzo hayo pia yanalenga pamoja na mambo mengine, kuwapa mbinu za kisasa ili kuwasukuma kuwekeza kwa tija katika sekta ndogo ya kilimo mifugo.

Ofisa Biashara na Uwezeshaji Wanawake na Vijana kupitia Mradi wa Mwanamke Imara, unaotekelezwa kwa ubia na Shirika la Kiraia la KWIECO, James Zakaria, alisema jana kuwa wanawake hao pamoja na mambo mengine, wanajengewa uwezo kwenye masuala ya ujasiriamali.

"Kwa sasa tunaangalia namna ya kujikwamua kiuchumi na mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia, ambayo ni janga kubwa hasa kwa jamii ya wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro ndiyo maana Mradi wa Mwanamke Imara, umejikita zaidi kuwajengea pia uwezo wanawake na vijana kuhusiana na masuala ya uongozi, umilikaji wa ardhi na kutambua haki zao," alisema.

Wanawake hao wanatoka katika kata 10 zinazotekeleza mradi huo ambazo kwa Wilaya ya Rombo ni Maida, Katangara Mrere, Motamburu Kitendeni, Mrao Keryo na Kata ya Leni.

Kata za Moshi ni Mabogini, Mamba Kaskazini, Mwika Kaskazini, Mwika Kusini na Kilema Kusini.

Vilevile, wanawake hao kwa sasa pia wananufaika na mafunzo ya ujasiriamali na mikopo ya uwezeshaji kiuchumi.

**Kata za Moshi ni Mabogini, Mamba Kaskazini, Mwika Kaskazini, Mwika Kusini na Kilema Kusini.**

# Ubovu shule wahatarisha usalama wa wanafunzi

**Na Anjela Mhando,** MOSHI

SHULE kongwe ya Msingi ya Uhuru iliyoko katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, inatishiwa uchakavu wa miundombinu yake na uhaba wa vyumba vya madarasa, hali ambayo inahatarisha maisha ya wanafunzi wa shule hiyo.

Hadi kufikia sasa, inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa sita ambavyo huwalazimisha walimu, kuunganisha mikondo miwili ya wanafunzi wa darasa la nne na darasa la saba, wakati wa mitihani.


Hayo yalielezwa jana na wanafunzi wa shule hiyo, walipósoma risala yao kwa Meya wa Manispaa hiyo, Zuber Kidumo.

Akisoma risala hiyo, mwanafunzi wa darasa la saba, Inviolatha Aloyce, alisema pia shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa madawati 120.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Lawrance Kisima, alisema wamewaandaa vyema wanafunzi hao kufanya mitihani ya kuhitimu darasa la saba, wakiwamo wasichana 35 na wavulana 44.

Aidha, Kisima alisema baada ya kutoka katika mitihani ya majaribio, amebaini wanafunzi wake wamefanya vizuri kwa wastani wa wa alama A hadi C na hakuna mwanafunzi aliyepata alama D.

Akijibu risala ya wanafunzi hao, Meya Kidumo alisema tayari Halmashauri ya Manispaa imetenga fedha kwa ajili ya kutatua matatizo yanayoikabili shule hiyo.




Ofisa Mwandamizi wa Programu wa Shirika la Fair Trade Africa -Tanzania, Tumaini Minja (kulia), akizungumza na wadau wa uzalishaji na usafirishaji nje ya nchi wa zao la kahawa na chai kutoka Tanzania na Kenya, katika mdahalo maalumu wa uzalishaji wa mazao bora kwenye mashindano ya ubora wa kahawa yaliyoandaliwa na shirika hilo, yajulikanayo kama 'Kombe la Dhahabu Coffee Quality Contest' yaliyoanza Septemba 26, mwaka huu hadi juzi, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro. **PICHA: JAMES LANKA**

# Dereva basi la shule mbaroni kwa madai ya kumgonga mtoto na kufa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

POLISI mkoani Kilimanjaro, inamshikilia dereva wa basi la Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Valley View, kwa tuhuma za kumgonga mtoto mwenye umri wa miaka mitatu, Aisha Abdalah, ambaye alifariki dunia papo hapo.

Mtoto huyo alipata ajali hiyo juzi, wakati alipokuwa akimsindikiza kaka yake shule.

Kamanda wa Polisi Mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, ingawa hakumtaja jina dereva huyo, alikiri kukamatwa na kushikiliwa kwa ajili ya mahojiano.

"Ni kweli tukio hilo limetokea na dereva huyo anashikiliwa. Hivi sasa tunaendelea kumhoji na upelezi utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo kumfikisha mahakamani kujibu kosa linalomkabili.

"Katika tukio hili, tunaona mtoto alikimbilia puto na dereva kuondoa gari bila kujua. Endapo mtoto yule angelindwa, labda jambo hilo lisingetokea. Wazazi na walezi tuongeze umakini katika kuwalea na kuwatunza watoto wetu," alisema.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, akiwamo Saimon Peter, walisema ajali hiyo ilitokea juzi, majira ya 7:30 juzi, katika eneo la kuchukulia watoto la Kambi ya Magereza lililiko Manispaa ya Moshi.

"Mtoto huyo alikuwa anamsindikiza shule kaka yake, akafika kwenye kituo, kaka yake akapanda gari, yeye alikuwa na puto mkononi, likamponyoka na kukimbilia chini ya gari na dereva bila kujua, akaondoa gari na kumsababishia umauti," alisema Peter.




UCHUMI WA BLUU KILWA

Inaweka rekodi Bara Afrika, pweza kuvuliwa kwa kigezo elektroniki, kutua soko kimataifa

Ukurasa 16

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 30, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Machinga Dodoma wafika mwisho mtaani, kuhamia maisha ya sokoni

Ukurasa 18

# Wanakijiji Magu wachoshwa, wajenga daraja lenye kiwango, TARURA yabariki

**Na Anthony Gervas, MAGU**

"MATESO ya miaka mingi bila kupata ufumbuzi wa kutatua kero hii ya kuvuka Mto Nyalali, unaotenganisha kata za Bujora na Kisesa wilayani Magu mkoani Mwanza,hatimaye sasa wananchi tumepata dawa ya kuondoa kero hii bila kusubiri Serikali," sauti ya wananchi wakisema.

Wananchi na wadau wa maendeleo katika vitongoji vya Iseni A,B na Ng'wang'alanga A katika kata hizo, wameamua kujitolea kuchangia kujenga daraja dogo, baada ya kuchoshwa na changamoto ya kuvuka maji katika mto Nyalali unaozitengenisha kata hizo.

Ni uamuzi mgumu wa kujenga kwa nguvu zao wenyewe bila kusubiri fedha za Serikali,kutokana na mto huo kuwatesa kuvuka kwa miaka mingi pasipo na ufumbuzi ,ambao wakati wa mvua na mafuriko hulazimika kuzunguka umbali wa takribani kilomita tatu kupata huduma zao.

Hofu yao ilikuwa ikitokea wakati mvua za masika zinapoanza kunyesha na kusababisha kukatika mawasiliano rahisi, hivyo baada ya kukamilika kivuko hicho kitawezesha kupita hata magari madogo ya mizigo,watembea kwa miguu na vyombo vingine vya usafiri.

Wananchi hao, Kanisa la Pentekoste (FPCT) na wadau wamechanga vifaa vya ujenzi, fedha tasilimu, mawe ,saruji, mchanga nondo, mawe tripu 30 kufanikisha ujenzi huo kugharimu kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 15 kukamilika daraja.



Wanakijiji na mafundi wao wakiendelea na kazi ya kujenga daraja, huku Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini wilayani Magu (TARURA), Mhandisi Wawa Nyonyoli ( wa kwanza kulia mwenye jaketi la kijani) akiwashuhudia. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

Wanasema watoto na wanafunzi walikwama kupita kwenda shule na kuwasababishia adha kubwa wazazi wao kuingia gharama za usafiri wa bodaboda kuzunguka mto huo.

Kaulimbiu yao ni kuondoa kero zinazowakabili muda mrefu, ikiwemo kutengeneza barabara za mitaa,ambazo ni changamoto kubwa hadi sasa.

**KINAMAMA.**

Jenifa Masanja, ni mwanamke anayewashukuru kukubaliana kufikia uamuzi huo wa kuondoa changamoto iliyowasibu muda mrefu, watoto na wanafunzi kupata shida kubwa.

**MWENYEKITI KAMATI**

Shaban Kumalija, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Daraja, anaeleza kuwa wananchi na wadau wamejitolea kuchangia ujenzi huo, kuondokana na kero hiyo inayowaumiza kichwa kila siku kutafuta namna ya ufumbuzi.

Kumalija anasisitiza kujengwa kwa miundombiu hiyo katika ubora unaotakiwa bila kufanyika udanganyifu wa aina yeyote katika fedha zitakazotumika, wakikusudia kukamilisha mwezi ujao,Oktoba.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ng'wangh'alanga Mwenesho Malago, anasema ilibidi yeye na wadau kuibua wazo hilo la ujenzi, kutokana na wananchi wao kila kukicha wanalalamika kuhusu uvukaji mgumu katika mto huo hasa nyakati za masika.

Malago anasema hivi sasa ndoto yao imetimia na kuepuka shida iliyokuwa ikisababisha hata maafa ya wananchi na watoto kusombwa na mto, akimshukuru meneja wa tarura Wilaya ya Magu kufika katika ujenzi na kukagua daraja lao pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam.

Anasema hatua hiyo itasaidia vitongoji vyote hata kurahisisha huduma muda wote katika kipindi cha mavuno mazao ya wananchi kupita na magari.

Hata hivyo Mwenyekiti wa kijiji cha Wita, Michail Migeke anaipongeza jamii na wadau hao kuhusu mchango wao wa hali na mali kuhakikisha wanatatua kero hiyo,badala ya kusubiri serikali kwani haikuwa rahisi kuchukua hatua za kutatua changamoto hiyo.

**DIWANI KATA YA BUJORA.**

Diwani wa Kata ya Bujora, John Bunyanya, anaeleza kuunga mkono juhudi hizo za maendeleo, lakini wasimamizi wake wafuate taratibu na sheria za ujenzi kuanzia ngazi ya vitongoji,vijiji hadi kwenye kata kama walivyokubaliana katika vikao vyao, ili kuondoa migogoro inayoweza kutokea baadaye.

"Kama tulivyokubaliana kwenye kikao,ili hata likitokea jambo diwani asiingie mkenge kwamba alikubali wakati mimi sijaona barua yao kama mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya kata," anasema.

**MENEJA TARURA**

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini wilayani Magu (Tarura), Mhandisi Wawa Nyonyoli, anapongeza juhudi za wananchi na wadau waliojitolea kuchangia maendeleo, wakitumia nguvu zao wenyewe kuwa hata serikali iko nao bega kwa bega kuhakikisha ujenzi unafanyika katika kiwango chenye ubora unaotakiwa.

Mhandisi Nyonyoli anasema, daraja litakalojengwa linatakiwa kudumu zaidi ya miaka 30 likitoa huduma kwa wananchi, yakiwemo magari na vyombo mbalimbali vya usafiri, akiwaomba kuboresha barabara zinazounganisha huduma hiyo.

Katika upande wa barabara, anashauri ziwe na upana wa mita nane, mitaro na sehemu ya kupitisha huduma za miundombinu mingine kama vile nguzo za umeme na mabomba ya maji.

Anataja kuwa zipo aina tatu za barabara ambazo ni pamoja na makusanyo yenye upana wa mita 40 ikiwemo hifadhi yake, barabara mlisho ikiwa na ukubwa wa mita 30 pamoja na mita 25.

Anaeleza kuwa kama barabara inayounganisha daraja hilo itatengenezwa vizuri kwa kufuata vipimo vya kitaalamu,tarura itaangalia uwezekano wa kuweka bajeti na kuiingiza katika mtandao wa barabara, ikiwa hivi sasa haiko rasmi kwenye mtandao huo.

»»»»»»»»»»»»»»»»»»»

BIASHARA

# Mtihani bugudha, lugha chafu Stendi Kuu Moshi na jibu la wenye dhamana

## • Kila upande unakiri...kitendawili utatuzi



Baadhi ya abiria katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi wakisubiri magari. **PICHA: MARY MOSHA**

**Na Mary Mosha, MOSHI**

MATUMIZI ya lugha chafu (matusi), wizi, ung'ang'anizi wa mizigo, kupandishwa nauli bila ya kuzingatia uhalisia wa gari, vimetajwa kuwa miongoni mwa matatizo yanayowakumba abiria katika Stendi Kuu ya Mabasi mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Aidha, ni matatizo yanayowakumba abiria kutoka kwa baadhi ya wakala wasio rasmi wanaotumia wapigadebe kupata abiria wa kujaza magari, chini ya wakala husika.

Wakala hao wasio rasmi, hasa katika magari yanayoenda mikoani wakiwa na vitabu vya tiketi au nakala za tiketi vya zaidi ya magari saba, jambo ambalo hatambuliki ni mtendaji wa gari gani hasa panapo tokea madhara.

**NAMNA YANAVYOWAKUTA**

Rachel Mmasi, ni miongoni mwa abiria Nipashe iliyemkuta katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi, anasema kumekuwapo na wakala, baadhi wakiwa katika hali ya ulevi, hata wanatumia lugha chafu kwa wateja abiria.

Anasema, wakala hao wasio rasmi huwasumbua wateja kwa kung'ang'ania mizigo yao, hata wapo wanaotumia mwanya huo kuwaibia.

"Mtu anaweza kuchukua pochi yako wakati anajifanya kukuwaishia kwenye gari ambalo amekutafuta au kukupokea na badala yake anatumia mwanya huo kuiba na kwa bahati mbaya zaidi, huna pa kushitaki, inaumiza sana," anasema.

"Wengine tunasafiri na watoto wanasikia lugha hizi, kwa kweli haifai. Pia, hawana mwonekano mzuri (nadhifu), hali ambayo unashindwa kutambua yupi ni wakala yupi ni mwizi, tunaomba serikali ichukue hatua za haraka ili kuwasaidia abiria," anasema Fabian Msele.

Abiria, Nathaniel Frank, anasema katika harakati za kung'ang'ania mizigo yao, wengi hutumia upenyo huo kuwaibia wakala washirikiane na wezi.

"Mimi ni mfanyabiashara wa simu hapa Moshi. Mara nyingi husafiri maeneo mbali mbali ikiwamo Namanga. Nimeshawahi ibiwa simu, mbaya zaidi hakuna msaada, licha ya stendi hiyo kuwa karibu na Kituo cha Polisi Kati Moshi.

"Nyakati za kufungua na kufunga shule, wanafunzi wengi hulizwa hapa. Baadhi yao wanadai kuwa na vitambulisho, lakini hazionyeshi jina wala gari analofanyia. Ikiwa wapo kwa mujibu wa sheria wawe nadhifu watengenezewe vitambulisho na gari wanaofanya hii itarahisisha na kumalidha hali iliyopo kwa sasa, " alisema.

Devota Robert anasimulia kuwahi kufanyiwa matibabu ya huduma ya kwanza na wasamaria wema (gari tumelihifadhi) baada ya kufika stendi na kung'ang'aniwa na mawakala hao, hata akaangukia kuchanwa mkononi na kuvuja damu.

"Niliposhuka kwenye bajaji, naingia stendi walikuja mawakala wengi wakitaka kujua naelekea wapi. Nilipo wajibu walianza kung'ang'ania katika harakati hizo moja kati yao alinichana kwa kucha, ndipo nikapatiwa huduma ya kwanza hapa kutoka kwa msamaria mwema.

"Sielewi juu ya afya yangu, pia wanatupandishia nauli kulingana na utashi wake, unalipa nauli ya daraja la kwanza, gari ni ya daraja la pili, hii inaumiza sana," anasema.

Exaud Oiso, mfanyabiashara wa pesa (wakala kampuni za simu), anakiri fujo hizo akieleza mazingira hayo yamekuwa hatari kwa biashara zao za pesa.

"Mteja anaweza kuja anataka kutoa pesa kwa ajili ya nauli labda na matumizi yake binafsi, wakala zaidi ya sita wameambatana naye, hivyo kama alikuwa atoe laki a naogopa kutibiwa anatoa 50,000.

"Hii inatokana na wakala mmoja ana tiketi za magari zaidi ya kumi, lazima kuwepo na kumkimbilia mizigo ya wateja na kuwashawishi, lakini kutoka na hali ya kilevi hukuta ameshafanya fujo kwa mteja," anasema Oiso.

**WAKALA WAFUNGUKA**

Akizungumza na Nipashe, wakala Witness Breyson, anasema wapo stendi hapo kwa ajili ya kutafuta riziki, licha ya kuwepo matatizo mengi kwa abiria na kwao.

"Ni kweli kuna fujo nyingi, matusi hutokea kutokana na wengi kuwa walevi, udhalilishaji upo hasa kwa wanawake na wengine kubishana na abiria kiasi kumchapa makofi, wengine huibiwa, hatuna ubishi ila ni kutokana na ukosefu wa ajira.

"Vitambulisho tunavyo na tunapaswa kuvitundika shingoni tatizo sasa, wengi wetu hawavai na wengine huchukua na kujiandikia neno 'Wakala' kumbe siye, hawa ndio wanaleta shida, kuhusu usafi ni kweli wengine hawaogi hata wiki, " anakiri Wakala Witness.

**NINI KIFANYIKE?**

Amina Ramadhan, ni mjasriamali wa uji na chai katika stendi hapo, anaiomba serikali kusimamia sharia, taratibu na kanuni, ili kuleta hadhi ya stendi hiyo.

"Uongozi wa stendi wafanye operesheni maalumu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, kuhakikisha kila mtu aliyepo stendi anaoga kila siku, hakuna kufika stendi ukiwa umelewa na ukibainika hivyo fidia shilingi elfu hamsini hadi laki moja.

"Ukionekana umemkimbilia abiria, kuwepo na faini wanaopokea mizigo ya abiria wawe na vigari maalumu vya kuendesha mizigo hiyo kutoka sehemu moja kwenda nyingine na si kubeba kama ilivyo kwa sasa na watakaobainika kutukana kila tusi 20,000-50,000," anasema Amina.

Grace Wilson, anashauri serikali iweke askari kanzu kudhibitu usumbufu huo stendi alifafanua: "Hapa pana vijana wengi ambao hawana ajira wanatafuta riziki na endapo watafukwazwa bila mpangilio wataongeza vibaka mitaani, wadhibitiwe kwa kuhakikisha eneo la stendi linakuwa safi na linafanya ni eneo jema la kila mmoja kufanya kazi. "

Leila Peter, muuza matunda katika stendi hiyo, anasema suala la usafi na unadhifu ni tatizo na anashauri haja ya kuwekwa sheria na askari stendi wasimamie uvaaji sare za magari kwa madereva na utingo wawe wasafi.

"Wamiliki wa magari wasaidie wafanyakazi wenu kupata sare zaidi ya moja na zifanyiwe usafi mara kwa mara ili kuwaweka nadhifu, hawa nazungumzia sana kwenye magari aina ya Costa na Hiace.

"Tumekuwa tukishuhudia tisheti zile zikichomekwa kwenye siti za magari na wakizivaa tu pale wanaoanza safari, hii sio sawa. Pia, utingo wengi hawavai na kuwaruhusu wapiga debe wengi(wakala) kusimama mlangoni jambo ambalo bado linasababisha wizi," anasema.

**WENYE DHAMANA**

Mwenyekiti Umoja wa Wasafrishaji - Akiboa Kanda ya Kaskazini, Hussein Mrindoko, anakiri tatizo wameliona na anaahidi kuchukua hatua ya kulikomesha.

"Tiketi kwa njia ya mtandao zimeanza Septemba Mosi mwaka huu. Tulikuwa na askari hapo stendi na kwa sasa amestaafu, hivyo tunatarajia kukaa na Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Simon Maigwa, kumwomba atupe mwingine. Haya matatizo yataisha," anasema.

Meneja wa Stendi hiyo, Hashim Kilongola, anakili na kufafanua matatizo hayo tayari uongozi wa stendi umeanza kuchukua hatua kuwatoza faini Sh.50,000 kwa atakayebainika kutukana.

"Tumekaa na viongozi wa mawakala na vimewapa maelekezo ya usafi na unadhaifu, hatutasita kuchukua hatua kali kwa atakayebainika. Niendelee kuwataka watu wote wanaofanya kazi katika stendi ya Moshi kufuata sharia, kanuni na taratibu za nchi," anaeleza.

Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa Kilimanjaro, Paul Nyello, katika hilo anasema, ni kosa kumwomba abiria kutoa taarifa wanapo kata tiketi tofauti na gari ilivyo.

"Namba zetu zipo wazi, hakikisha tiketi uliyokatiwa inaendana na hadhi ya gari utakayopanda. Ikiwa ni tofauti wasiliana nasi na tutachukua hatua stahiki, hatutawafumbia macho madereva, wamiliki wa magari wanaoruhusu mawakala kumnyanyasa abiria stendi au vinginevyo," anasema.

BIASHARA

NAIBU WAZIRI AKIIPIGIA DEBE ...

# Vifungashio vyabaki malighafi nyeti ya uzalishaji, lakini ni adimu nchini

## • Wa ughaibuni waonyesha nia kuwekeza

**Na Beatrice Moses**



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara akizungumza na wafanyabiashara wa vifungashio kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee Dar es Salaam, akitumia nafasi hiyo kuwashawishi kuwekeza nchini hapa. **PICHA ZOTE: BEATRECE MOSES.**

Hatua za mfanyabiashara au mjasiriamali kufanikiwa kusonga mbele zinahusisha mambo mengi, mojawapo ni kuwa na bidhaa bora zenye kuvutia, iliyohifadhiwa vyema hivyo inaweza kuchukulika, Naam! Hapo ndipo kifungashio kinahusika.

**KIFUNGASHIO NI NINI?**

Kimsingi, ni kitu kinachotengenezwa maalum kuhifadhi bidhaa husika iwe salama, iweze kuchukuliwa kwa urahisi na wateja au isafirishwe katika mazingira safi na kufikishwa kwenye soko au mteja. Pia, kinatumika kumvutia mteja kulingana na hitaji lake kwenye bidhaa husika.

Kifungashio kinasaidia kuitunza bidhaa isiharibike ama hasa wakati inaposafirishwa kwenda maeneo tofauti. Ni kwenye vifungashio, ndipo maelezo kuhusu bidhaa husika huwekwa kwa lengo la kumshawishi au kumuelimisha mteja kuhusu matumizi ili anaponunua atambue pia na matumizi yake ipasavyo.

Kwa ujumla vipo vya aina tofauti kulingana na bidhaa husika, ikiwamo vya matunda, chakula, sabuni, vinywaji, vinawekwa katika

vipimo vya namna tofauti kulingana na uhitaji wa soko au mzalishaji wa bidhaa husika.

Suala la kifungashio linapiga hatua ya mbali, hata kufika ngazi kwamba ni moja ya vigezo muhimu katika biashara ya kimataifa, nchini zikishuhudiwa sasai kama Shirika la Kuhdumia Viwanda Vidogo (SIDO) ikihimza suala hilo.

**HALI ILIYOKO**

Nchini kwa ujumla, bado kunatajwa ukosefu wa vifungashio nahasa vinavyokidhi viwango vya kimataifa, hatua inayotajwa, hata kusababisha baadhi ya wafanyabishara kukwama katika ushindana kwenye soko la kimataifa.

Mfanyabiashara wa Mvinyo Dickson Mgoha ana simulizi ni kwamba, aliwahi kulazimika kwenda kununua vifuniko vya bidhaa zake nchini Uganda baada ya kuvikosa nchini, vikiwa ni hitaji la vizibo 50,000, kuhudumia kreti za vinywaji vyake, ambapo kila moja ilikuwa na chupa 24.

"Mimi bado ni mfanyabiashara wa hapa ndani ya nchi, lakini lengo ni kukuza biashara yangu. Hivyo, nipo kwenye mchakato wa kutanua soko kuwa la kimataifa. Kuna mengi natakiwa kuyatimiza, Sasa vifungashio ni changamoto kubwa kwangu," anasema.

Wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Bidhaa za Uhandisi, Vyakula, Vifungashio na Uchapaji wiki iliyopita mnamo Septemba 22, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, akatumia nafasi hiyo kufanya kampeni ya kuhamasisha wafanyabiashara hao kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza nchini kwa kujenga viwanda vikiwamo vya kutengeneza vifungashio.

Naibu Waziri Kigahe, anatumia fursa ya kutembelea kwenye mabanda yaliyopangwa bidhaa tofauti ndipo katika mazungumzo na wafanyabiashara, akawakaribisha kuwekeza hapa nchini, wakiwa wametengewa maeneo ya ujenzi viwanda kwenye mikoa tofauti, akihimiza suala la vifungashio .

Anaeleza kuamini ujenzi wa viwanda vingi ikiwamo vya vifungashio vitasaidia kuweka ushindani kwenye uzalishaji, hivyo kuwepo ubora na upatikanaji wake kwa uhakika.

Solail Khan wa Kiwanda cha Kutengeneza Vifungashio cha Cristal Plastic (LLC) kilichopo Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), anasema wameshiriki kwenye maonyesho hayo kwa mara ya kwanza, ili kutangaza bidhaa zao na kutafuta washirika wa kibiashara.

Anasema kuwa, LLC inafikiria pia kuanza kwa kufungua tawi nchini, katika harakati zao za kutafutarisha suluhu za vifungashio, wakiendelea kupata taarifa kuhusu mitindo inayohitajika kwenye soko, ili wazalishe.

Hapo Khan anataja vigezo vingine kuwa ni

gharama nafuu, usalama na mvuto wa vifungashio vinavyokusudiwa.

Anasema LLC pia wana zana za uhandisi, kanuni na michakato, nyenzo za mafunzo, miongozo, taratibu za uendeshaji na vipengele vingine vinavyosaidia kuhakikisha bidhaa zinakidhi mahitaji yote ya wateja na usalama wa afya na chakula.

Kwa mujibu wa Khan, wanafanya utafiti kujua wana soko kiasi gani nchini hapa, iwapo itabainika kuwa kuna soko lenye uhakika, watasaka washirika ili waweze kujenga kiwanda.

**KUTOKA SIDO**

Msimamizi- Kituo cha Vifungashio na ufungashaji kutoka SIDO, Dar es Salaam Antonia Masoy anasema kuwa wanatambua changamoto hiyo ipo na tayari wameanza kuitafutia majibu.

Masoy anasema, mnamo April 21 mwaka huu, walifanya kikao maalum na wazalishaji wa vifungashio na wajasiriamali na wakapata nafasi ya kujadiliana, kuangalia jinsi gani wazalishaji wa vifungashio watamudu kukidhi kiwango cha ubora wa kushindana kwenye soko la kimataifa.

Katika kikao hicho wajasiriamali walipata nafasi ya kutoa maoni yao kwa wazalishaji vifungashio, ikiwamo aina wanazohitaji, kulingana na mahitaji ya soko la bidhaa zao.

Masoy anasema, suala la ukosefu wa vifungashio sahihi umesababisha baadhi ya wajasiriamali kuvitumia vifungashio visivyo na nembo, huku kukielezwa kwamba, kukosekana vifungashio vyenye kiwango hasa vya chupa, inatokana na kuwa na viwanda vichache vya kutengeneza bidhaa hizo.

"Wajasiriamali wanahitaji kuza bidhaa zao katika viwango tofauti, ikiwamo ndani ya nchi na nje ya nchi, vifungashio vinavyokidhi kiwango cha kimataifa ni muhimu," anasema Masoy.

Katika hilo anafafanua kwamba, kwenye vifungashio vya chupa, vinavyopatikana ni vyenye ujazo wa milimita 330, nyingi zikiwa kwenye maumbo yanayofanana, huku wafanyabishara wazalishaji wakihitaji zenye mwonekano tofauti, ili kutofautisha bidhaa zao kwenye soko, hata wakakabiliana na ushindani.

Anatoa mfano wa vifungashio vingine vinavyokosekana ni, vinavyohusisha vipodozi hasa za bidhaa za 'tyubu.'



Baadhi ya vifungashio katika maonyesho ya biashara jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

BIASHARA

## UCHUMI WA BLUU KILWA

# Inaweka rekodi Bara Afrika, pweza kuvuliwa kwa kigezo elektroniki, kutua soko kimataifa

**Na Jenifer Gilla**

HIVI karibuni serikali chini ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo kwa kushirikiana na Shirika la Aqual Farm (AFO) na Umoja wa Ufuatiliaji na Uhalalisho wa Mazao ya Bahari (SALT), iliyofanya kikao na wadau wa samaki pweza, kukusanya maoni ya kuboresha mkakati wa kufuga kwa mfumo wa kielektroniki, wakifuatilia uvuvi wa Pweza katika wilaya ya Kilwa.

Mfumo huo unapokamilika na kuanza utekelezaji, unatarajiwa kuleta mapinduzi ya soko la samaki hao nchini na hata kuingizwa soko la kimataifa mfano shamba la wilayani Kilwa.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Takwimu ya Uvuvi ya mwaka 2019 ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, viumbe bahari huchangia pato la taifa kwa asilimia 1.71.

Taarifa hiyo pia inaonyesha mwaka 2020, sekta hiyo ilitoa ajira za moja kwa moja kwa zaidi ya watu milioni 4.5 katika shughuli za uvuvi ikiwamo wasindikaji, wafanyabiashara wa samaki na wachuuzi wa zana za uvuvi.



Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Mashimba Ndaki (aliyekaa katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilwa, Eston Ngilangwa, (mbele kulia) akiwa na wadau wa samaki pweza katika warsha ya kukusanya maoni kuboresha mkakati wa kufunga mfumo kielektroniki wa ufuatiliaji wa uvuvi wa Pweza katika Halmashauri ya Kilwa, kilichofanyika jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.

**MFUMO ULIVYO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilwa, Eston Ngilangwa, anaiambia Nipashe kuwa ni mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia mnyororo wa thamani wa pweza toka anapovuliwa, hadi anapofika kwa mlaji.

Anasema ufuatiliaji wa mfumo huo ulivyo, mteja anaponunua samaki ana uwezo wa kufahamu historia ya samaki huyo tangu alipovuliwa, kampuni iliyomchakata, kwa kupitia alama maalum zilizokwekwa kwenye bidhaa hiyo (barcode), jambo linalompa uhakika wa usalama wa chakula anachokinunua.

Mkurugenzi Eston anasema, lengo kuu la kuleta mfumo huo ni kuliteka soko la dunia la samaki huyo hasa kwa nchi zinazoendelea, ambazo wanaweka kupaumbele kwenye usalama wa chakula.

"Katika sheria za vyakula hasa nchi zilizoendelea wanazingatia sana usalama wa chakula, ndio maana unaona baadhi ya vitu tunavyovizalisha Afrika haviwezi kuuzwa ughaibuni, hasa nchi zilizoendelea kwa sababu hawana uhakika wa usalama wa vyakula hivyo," anasema.

**KWANINI PWEZA?**

Mkurugenzi huyo anasema, pweza ni samaki anayeonekana kufanya vizuri katika soko la dunia ingawa bado pweza anayevuliwa Kilwa hajafanya vizuri katika soko hilo.

"Tuligundua kuwa samaki huyu hafanyi vizuri katika soko la kimataifa, kwa sababu hakujawa na mfumo wa ufuatiliaji wa mnyororo wa thamani, ukilinganisha na wanaopatikana katika mataifa mengine kama vile Mexico," anafafanua.

Anasema, kwa sasa bidhaa hiyo inauzwa katika nchi za Ubelgiji na Ufaransa, lakini bado hawajafikia kuuza katika masoko makubwa kama vile Japan, kwa sababu nchi hiyo inazingatia kuwapo na mfumo wa ufuatiliaji wa mnyororo wa thamani katika chakula hicho.

Takwimu katika mtandao wa forbes ya mwaka 2019, inaonyesha kuwa, nchi zinazokula zaidi pweza ulimwenguni ni Korea, Japan, na zile za Mediterania kama vile Hispania, Ureno, Ugiriki na Italia.

**NAFASI YA KILWA**

Mkurugenzi huyo anasema, mradi huo una haki ya kuanzia katika halmashauri hiyo, kwa sababu inajulikana kuwa ina hazina ya uchumi wa bahari nchini na kuwakaribisha wadau wengine kuwekeza katika sekta ya uvuvi.

Anasema katika kisiwa cha Songosongo, huwa wanavua takribani tani 100 za pweza kwa mwaka na kwa kushirikiana na wadau wa zao hilo, walianzisha utaratibu wa kufuga mwamba ili wavuvi wavue kwa utaratibu wa kila baada ya miezi mitatu, ili kuhakikisha uvunaji wa samaki huyo unawanufaisha wanaoshiriki.

Akizungumza katika warsha ya ufunguzi wa ukusanyaji wa maoni ya mfumo wa ufuatiliaji mnyororo wa samaki huyo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema serikali imejipanga kuboresha mifumo ya ufuatiliaji wa mazao ya uvuvi, ikiwamo samaki pweza, ili kuyaongezea thamani na kuboresha maisha ya wavuvi na wadau wa zao hilo nchini.

Mwenyekiti wa Wavuvi wa pweza wa Kata ya Songosongo, Juma Mahuhuri, anasema kuwa mfumo huo utawaongezea kipato, kwa sababu pweza hao watakuwa na uwezo wa kuuzwa katika masoko mengi.

Anasema, changamoto wanazokutana nazo katika soko hilo ni wigo kuwa mdogo, kwa sababu hawana watu wengine wa kuwauzia zaidi ya wanaolipia gharama za uvuvi jambo linalowabana katika masoko.

"Yaani hapa kuna mabosi wetu ambao wanakuja kulipia gharama zote za uvuvi, ikiwamo mafuta, mtumbwi halafu sisi tunakwenda kuvua tukirudi samaki wote wanakuwa wa kwake, changamoto hapo huwezi kuongeza bei kwa sababu mnakuwa mmeshakubaliana kabla ya kwenda kuvua," anasema.

Juma ambaye naye pia ni mvuvi maarufu katika eneo, hilo anataja changamoto nyingine ni uwapo wa wavuvi wasio waaminifu wanaoenda kuchokoa pweza katika mwamba uliofungwa, hali inayowarudisha nyuma kimaendeleo na mikakati yao ya kutanua uzalishaji.

Anasema, lengo la kuanzisha mpango wa kufunga mwamba, ni kuwapa nafasi pweza kuzaliana kwa wingi ili kuboresha shughuli za uvuvi huo. "Wakati tunaanza mpango huu, tulielimishwa vizuri na wote tukaelewa na kukubaliana, mara ya kwanza kufungua mwamba tulikuwa tunavua tani 40 kwa siku tatu. Lakini sasa, tunafunga mwamba kwa miezi mitatu na tukifungua hatupati kitu" anasema.

Kiongozi huyo wa wavuvi anasema, ni hali inayowavunja moyo, kwani hata wakiwakamata wezi hao na kuwapeleka polisi, ndani ya muda mfupi huwa wanaachiwa, pasipo kupewa maelezo yoyote au sababu za kutolewa kwao.

**WENYE DHAMANA**

Ofisa wa Uvuvi Kata ya Songosongo, Ulimbuka Mbwile, anasema kuwa mfumo huo mpya wa soko la kisasa ukianza kufanya kazi, unatarajiwa kuboresha maisha ya wavuvi, kwa sababu watakuwa wanauza kwa bei ya juu tofauti na wanavyouza sasa kwa Sh. 5000 kwa kilo moja.

"Kwa sasa mvuvi analazimika kuuza bei ya chini, kwa sababu wanunuzi nao wanalalamika thamani ya samaki huyo ni ndogo, lakini akishapandishwa thamani na soko lake likakua huko juu hata mvuvi naye atapata nguvu ya kupandisha bei," anasema

Mkurugenzi wa Asasi ya AFO, Jerry Mang'ena, anaeleza matarajio yake kwamba, Kilwa itakuwa mfano mzuri katika matumizi ya mfumo huo kwa kuwa Tanzania ni nchi pekee barani Afrika itakayofunga mfumo huo unaotumiwa na nchi tatu pekee duniani.

"Ndio maana tuliandaa kongamano ili kushirikiana na wadau wa samaki huyo katika kutoa mawazo, kupanga, na kutekeleza mikakati mbalimbali itokanayo na mfumo huo ikiwamo usimamizi mzuri wa uvuvi wa pweza na matumizi mazuri ya mifumo ya kielektroniki ili kufikia malengo waliyojiwekea, ili kitakachozalishwa hapa kiwe ni kutokana na matakwa ya wadau wenyewe," anaeleza.

Aidha, Jerry anasema katika kongamano hilo wamewajengea uelewa wadau katika namna ya ufuatiliaji wa kielektroniki na umuhimu wake kwa mazingira, jamii na uchumi.

Vivyo hivyo, ana ufafanuzi kwamba malengo na vipaumbele vitakavyokuwapo katika mfumo huo, ni kwamba ulete tija, kujenga mtandao wa watakaosaidiana kufanikisha kutekeleza mkakati huo na wadau kufahamu jukumu lao katika mpango huo.

Mkuu wa Umoja wa SALT, Jenny Barker, anaeleza furaha yake, pale Tanzania inakuwa sehemu ya kwanza duniani mafunzo ya usimamiaji na kanuni za ufuatiliaji wa mifumo ya kielektroniki kwa mazao ya uvuvi yatakayofanyiwa majaribio na kuleta tija.



Mvuvi akionyesha pweza baada ya kumvua. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Bila shaka Sensa itatupa ufumbuzi kwa walao bure!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

BUNDI ni ndege. Ana maumbile kama ya ndege wengine wakiwamo warukao na wasioruka. Tofauti yake, yeye haruki mara nyingi mchana, ni usiku tu huyo, tabia iliyosababisha binadamu wengine kumtilia shaka.

Shaka yao ni ya kuruka usiku, ambao kwao hususan Waafrika, ni muda wa wachawi au wanga! Fikra hizo zinasababisha bundi kuhusishwa na masuala ya kishirikina.

Kana kwamba haitoshi, wapo waliofikia kuamini kuwa bundi hubashiri kifo cha mtu na kwamba pale aonekanapo kwenye nyumba yenye mgonjwa, basi mara nyingi kama si zote, mgonjwa hupoteza maisha.

Lakini, wenye sayansi yao ya viumbe, wanasema tofauti ni kwamba bundi ni ndege mwenye uwezo mkubwa wa kunusa na hunusa zaidi palipo na mzoga. Hivyo, anaweza kunusa mzoga akiwa umbali mrefu.

Uwezo huo humfanya kupata harufu ya mgonjwa aliye mbali na hasa anapokuwa mahututi, kwani kisayansi, inaaminika kuwa mgonjwa akifikia hali mbaya, kuna sehemu ya seli zake huanza kufa na hivyo kumfanya bundi kunusa harufu hiyo.

Hivyo, kusogea kwake karibu na aliko mgonjwa si ushirikina, bali hisia za kupata mzoga kwa chakula, na ndiyo sababu husubiri eneo jirani ama mtini au kwenye paa la nyumba alimo mgonjwa, akitarajia mzoga huo kupatikana na si vinginevyo.

Bashrafu hii, inanifanya nimwone Kamisaa Mkuu wa Sensa ya 2022, Anne Makinda kujikuta ananusa harufu ya matokeo ya Sensa, hasa anapokuja na kauli kuwa vijana wengi wasomi walimaliza vyuo wanaishi wakila kwa wazazi wao bure!

Mama kasema vijana hao wanakaa bila kujishughulisha vyovyote kujipatia kipato, wakitarajia ajira kutoka serikalini badala ya kuiga wanavyofanya hata ambao hawajasoma! Ni kauli ya kijasiri sana kutolewa katika kipindi hiki cha ukosefu wa ajira unaozaa Panyarodi.

Hajakosea, ni kweli kabisa kwamba vijana wengi hususan wamalizao vyuo vikuu wako mitaani, wakitafuta kazi baada ya kupoteza miaka mingi wakitafuta na kupata elimu, lakini wakishindwa kuitumia hatimaye.

Sasa kwa bahati mbaya sana, lawama zinawalemea wao kana kwamba waliomba kusoma ili kutaabika. Ni hao ambao tumekuwa sisi wazazi, walezi na hata serikali, tukiwahimiza juhudi za kusoma kwa ajili ya mustakabali mwema baadaye.

Leo wanapohitimu masomo yao, tena kwa kufaulu, wanakosa kazi na kuambulia kulaumiwa tena, kana kwamba jitihada zao za kusoma mpaka vyuo vikuu zilikuwa ni za kujitafutia balaa na sasa wanaporudi kwa wazazi wao wanakuwa nongwa kwa kula bure. Wakale wapi?

Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, mara nyingi imekuwa ni kauli yake ya kujaribu kutazama upya mfumo wetu wa elimu na kuacha kutoa watoto majumbani na kuwapeleka hadi vyuo vikuu na kurudishwa kwa wazazi wao wakiwa hawana la kufanya kwa elimu yao.

Inashangaza kulaumu watoto waliosoma vyuo vikuu na kumaliza vizuri, wakati hatujaandaa elimu inayoweza kuwasababisha kujiajiri wenyewe, kwani mara zote tumekuwa tukiwafunza zaidi kinadharia na wakati mwingine kuwakaririsha, ili mradi mwishowe watoke na vyeti.

Hivi sasa lipo wimbi la vijana wanaoona kwenda vyuo vikuu ni kama kupoteza muda na hivyo wanaamua kuishia sekondari na kufanya mambo mengine, badala ya kutumia miaka mingi shuleni na kurudi kuungana na waliofeli darasa la saba kuendesha bodaboda.

Kama vijana wangeambiwa kuwa ukisoma mpaka kupata shahada utarudi kuendesha bodaboda au kufanya umachinga, hakuna hata mmoja angekubali kwenda chuo kikuu. Angejikalia nyumbani na kutafuta maisha mengine ya kulima na kuchunga mifugo.

Kama mfumo wetu wa elimu utabaki huu huu wa kupeleka watoto hadi vyuo vikuu na kurudi majumbani kukaa, huku wazee wanaotakiwa kustaafu waking'ang'ania kazini na wengine kung'ang'anizwa kwa kurudishwa kwa mlango mwingine, sijui mambo yatakuwaje?

Tunashuhudia baadhi ya wazee wakistaafu na kuongezwa muda, huku nafasi hizo zikistahili kuchukuliwa na vijana wanaomaliza elimu ya juu, tena kwa mikopo kwa ufaulu mzuri tu, lakini hakuna kitu kama hicho. Kwani nani alisema bodi za wakurugenzi lazima ziwe na wazee au wastaafu?

Hivi sasa tukubali tukatae, kwa maendeleo ya sasa ya kidigitali, vijana ndio wakati wao na wana uwezo mkubwa wa kushauri wakiwa kwenye bodi za wakurugenzi ambao kwanza wameshaondoka na Ulimwengu wa analogia. Utashauriwa pia analogia wakati digitali imeshika hatamu?

Inaonekana Anne alichokifanya ni hicho hicho cha bundi kunusa harufu tu ya Sensa, kwamba kumbe makarani walipokuwa wanatuhoji walijionea jinsi kundi kubwa la wahitimu wa vyuo vikuu linavyokaa na kula kwa wazazi. Bila shaka matokeo ya Sensa yatatupa ufumbuzi. Alamsiki!

BIASHARA

# Machinga Dodoma wafika mwisho mtaani, kuhamia maisha ya sokoni

## • Jiji lawekeza mradi wa bilioni kadhaa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipomsikiliza aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alipotoa maelezo ya vibanda vya Machinga wakati wa kukagua ujenzi wa Soko la Machinga Complex, Barabara ya Bahi jijini hapo, Machi mwaka huu. **PICHA ZOTE: OFISI YA WAZIRI MKUU.**

INAFAHAMIKA kwamba wafanyabiashara wadogo nchini maarufu Machinga, wamekuwa wakikibiliwa na kero katika utekelezaji majukumu yao ya kila siku kwa miaka mingi na uongozi mbalimbali kitaifa nchini.

Pia, kunatajwa kuwepo jitihada zilizofanywa na serikali kusaka nafuu kwa kundi hilo kutekeleza majukumu yake, pia ikiwa katika mazingira rafiki na wezeshi.

Sehemu ya mazingira ambayo yamekuwa yakifanyiwa kazi na serikali, ni pamoja na kutoa vitambulisho kwa machinga na kuwatambua rasmi, ili wakopesheke na kukuza mitaji yao.

Serikali imetoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa kuwapanga Machinga katika maeneo rasmi, ili kufanya shughuli zao bila ya kubughudhiwa.

Katika kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwapanga machinga katika maeneo rasmi Halmashauri ya jiji Dodoma, imekamilisha ujenzi wa mradi soko la wazi litakalohudumia wafanyabishara zaidi ya 5,000 na kutoa huduma kwa saa 24.

Aidha, kutoka na kukamilika mradi huo uliogharimu Sh. bilioni 9.53 jiji hilo lilitangaza Septemba 23, mwaka huu ndiyo mwisho kwa machinga yeyote kuendelea kubaki mtaani.

**MD DODOMA**

Mkurugenzi Mtendaji wa jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, anatamka kwamba kukamilika mradi huo, ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Rais alitoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa Septemba 13, mwaka 2021 kwa wakuu wa mikoa wote kuwapanga machinga, katika maeneo maalum bila ya kuwasumbua katika ufanyaji wao biashara.

"Mpaka sasa tunakamilisha mradi huu ni kama mwaka mmoja umepita toka agizo hilo kutolewa, kwanza tunamshukuru mheshimiwa Rais kwa kutuvumilia.

"Lakini tulitaka mradi huu ukamilike kabisa, ili machinga wote tuweze kuwapatia eneo sahihi na la kudumu kwa ajili ya biashara zao," anasema Mafuru

Pia, anasema soko hilo lina ukubwa wa mita za mraba 14,235 ndani yake inajumuisha huduma zote muhimu kama vile, eneo maalum la wanawake kunyonyeshea, kituo cha polisi, huduma za kifedha pamoja na maeneo ya vinywaji na vyakula.

"Tunataka mtu akiingia katika soko hili kila kitu akipate hapa. Kama kuna bidhaa kaja kununua, basi huduma za saluni azikute hapa, akitoka arudi nyumbani siyo kwenda eneo jingine tena kutafuta huduma," anasema

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mafuru, katika kiasi cha fedha kilichotumika kukamilisha ujenzi huo wa Sh.bilioni 6.5 ni mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali vya jiji hilo.

"Wakati tunaendelea na mradi huu, Waziri Mkuu alipita na kuona juhudi zetu na kutupa moyo kuwa tupambane kukamilisha ujenzi.

"Rais kupitia waziri wake wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, alitupatia Sh.bilioni tatu zilizotupa nguvu hadi leo hii kukamilisha kwa asilimia 100 mradi huu,"anaeleza Mafuru

Anasema kutokana na kukamilika mradi huo,uamuzi uliopo ni kwamba machinga wote hadi ifikapo Septemba 23 mwaka huu, wanapaswa kuwa wametoka mitaani.

"Hadi Sepetemba 24 (wiki iliyopita) hatutaki kumuona machinga yeyote anazunguka mitaani katika maeneo hatarishi, ikiwemo kupanga bidhaa zao kwenye barabara na maeneo ya watembea kwa miguu," anasema

Mkurugenzi huyo anasema, mradi huo utaliwezesha jiji kupata mapato Sh. Bilioni 1.2 kwa mwaka, kutoka makusanyo ndani ya soko, huku akiorodhesha faida za kukamilika mradi, inayojumuika kuongezeka usafi.

"Faida nyingine ya mradi huu ni usalama wa wafanyabiashara na bidhaa zao, pia wanaweza kukopesheka kwakuwa watatambulika wao na maeneo yao ya kufanya biashara," anasisitiza Mafuru

Vilevile, anasema hali ya Dodoma kuendelea kukua inalifanya jiji liendelee kujenga miradi mingine kwa wafanyabiasahara ndogo, maarufu machinga.

"Katika eneo la Nzuguni jirani na soko la Ndugai, tayari tumetenga kiasi cha Sh. milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa soko kama hili. Pia, kule eneo la mnada mpya kuna eneo tumepanga kutenga kwa ajili ya ujenzi wa soko kama hili," anaeleza.

**WAJASIRIAMALI NAO**

Wajasiriamali mkoa wa Dodoma, wao wameipongeza kwa kufaniksha mradi mkubwa wa kujenga Soko la Wazi la Machinga, litakalosaidia kuondoa adha ya mvua na jua waliyokuwa wakipata muda mrefu.

Katibu wa Wajasiriamali Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, anabainisha kuwa mradi huo wa fedha nyingi, kwao wanaohitaji uongozi wa jiji kuhakikisha watakaopata nafasi katika soko hilo, ni wale wanaostahili na siyo vinginevyo.

"Mradi huu ni mkubwa sana ambao serikali imewekeza fedha zake. Tunauomba uongozi wa jiji kuhakikisha kuwa hakuna upendeleo kwenye kutoa nafasi wanazopata wawe ni Machinga kweli na usifanyike udanganyifu wowote," anasema Dioniz

Aidha, anawataka wamachinga waunge mkono juhudi za serikali inayowataka wafanye biashara katika eneo hilo na kulipa kodi, ili kusadia kupanua wigo wa ukusanyaji mapato jiji la Dodoma.

"Pia soko hili linakwenda kujibu ukakasi uliokuwepo hapo awali, kuwa wafanyabiashara wakubwa wanawatumia machinga kukwepa kulipa kodi ya serikali," anasisitiza Dioniz

Hata hivyo, anaitaka serikali kuweka mfumo thabiti utakaowasaidia kudhibiti upotevu wa mapato na uwekezaji hapa ukubalike zaidi .



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokagua ujenzi wa Soko la Machinga Complex, jijini Dodoma.

UCHUMI

AJIRA PLUS

# Jitihada za NGO Kilolo zinavyoibua mapinduzi kilimo kwa vijana wake

## • Wawekwa darasani, nyenzo... kazini



Timu ya Bridge for Change wakikagua moja ya mashamba yanayolimwa na vikundi vya vijana wilayani Kilolo, mkoani Iringa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

**Na Frank Monyo**

KWA mujibu wa ripoti mbalimbali, Tanzania inahitaji takribani dola milioni 150 sawa na Sh. bilioni 345 kwa mwaka, ili kujijengea uwezo wake wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi huku kilimo kikitajwa kuwa mojawapo ya sekta muhimu yenye uwezo wa kuvutia uwekezaji huo.

Hata hivyo, serikali imeongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 294 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 751 mwaka wa fedha 2022/23, ili kujenga ufanisi wa sekta hiyo kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Jitihada hizo zimeibua taasisi isiyokuwa ya serikali, Bridge for Change (BFC) kuja na programu ya kimkakati iitwayo Ajira Plus.

BFC, kwa kushirikiana na Vi Agroforestry wameweza kutoa fursa kwa vijana kujihusisha na kilimo chenye tija pamoja na kukabiliana moja kwa moja na mabadiliko ya tabianchi.

Programu hiyo ya Ajira Plus, ilianza mwaka 2021 ikiwajumuisha takribani vijana 145 kutoka mitandao minne ya vijana wilayani Kilolo, mkoani Iringa waliowekwa chini ya uangalizi na usimamizi kwenye shughuli za kilimo kwa kupatiwa nyenzo, mafunzo na kuunganishwa na viongozi 47 ngazi ya wilaya.

Sambamba nayo, vijana hao walifundishwa mbinu za kupanda mazao mbalimbali, kutumia mbegu bora,kuhifadhi mazao kwa njia sahihi, misimu mizuri ya kupanda mazao mbalimbali yanayostahimili hali ya hewa, na mbinu nyinginezo za kilimo endelevu pamoja na ufugaji wa mifugo na ufugaji wa nyuki.

UFUGAJI NYUKI

Mojawapo ya shughuli zao za kipato na inayostahimili hali ya hewa, ni ufugaji wa nyuki, biashara yenye faida inayohitaji uangalizi mdogo na haiathiriwi kirahisi na mabadiliko ya hali ya hewa.

Anna Kivamba, mnufaika wa program hiyo, anasema baada ya kupewa elimu na BFC, kikundi chao waliamua kutengeneza jumla ya mizinga 60 ya nyuki na kuwekwa kwenye vyanzo vya maji, ili kurina asali na mazao mengine yanayopatikana kwa nyuki.

"Ufugaji wa nyuki ni wazi unachangia utunzaji wa mazingira na unafaida nyingi kwa mfugaji katika kuongeza kipato, na pia ufugaji huu hauhitaji mambo mengi na pia mtu anaweza kufuga nyuki huku akisubiri msimu wa kilimo kwani nyuki hawana msimu." anasema Kivamba

Anafafanua kuwa, vijana baada ya kupatiwa elimu wamekuwa wakishiriki kikamilifu kwenye ufugaji wa kuku, mazao, ufugaji wa nguruwe na kilimo cha bustani ambao unaongeza rutuba kwenye udongo ambao hupunguza utoaji wa hewa chafu ya kaboni katika mazingira.

Kivamba anasema, Ajira Plus wameshawishi vikundi 16 vya vijana kujikita katika kilimo kupitia ushirikiano na serikali za mitaa na kubadilishana maarifa, huku zaidi ya vijana 70 wamehamasishwa zaidi baada ya kuona tija kwenye sekta hiyo.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Maendeleo, Alito Kipindi anasema kupitia shirika la BFC wamenufaika kwa mafunzo na kwamba elimu waliyoipata wataendelea kuitumia ili kuwaongezea kipato.

Kipindi, anaeleza jinsi mradi huo ulivyomnufaisha, akifafanua: "Kubadilishana maarifa imekuwa nguzo muhimu sana kati yetu. Kuna mengi tunayoweza kufanya sasa hivi baada ya kupata ujuzi zaidi wa kile tunachoweza kukifanya."

Anasema, yeye ni mkulima wa bustani na anakiri kwamba kabla ya mafunzo hayo alikuwa haoni umuhimu wa kufanya shughuli za kilimo kwani hakuwahi kuona mafanikio yoyote kupitia shughuli hizo, lakini kwa sasa anaona mwanga na anatarajia kuona matunda baada ya programu hiyo.

Anasema katika shughuli za kilimo, mabadiliko ya tabianchi ni adui namba moja kwa mkulima, endapo kukikosekana elimu inayohusu kukabiliana na mabadiliko hayo ya kukosa soko kama ilivyokuwa awali kwake na wenzake wengi.

"Ajira Plus wametusaidia kutupa maarifa ya kufanya kilimo chenye manufaa na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, jinsi ya kuongeza rutuba kwenye udongo sambamba na kupanda mazao kwa weledi," anasema Kipindi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kilolo mkoani Iringa, Amasha Kisoma, anapongeza azma ya Ajira Plus kuhamasisha ushirikishwaji wa kilimo hasa kwa vijana wa eneo hilo, akifafanua:

"Tunaona vijana wengi wakijitokeza kila siku. Programu hii ni mwokozi wa maisha yao. Ninaweza tu kuipongeza BFC kwa uthubutu wao mzuri wa kuilinda kesho ya wakulima wadogo."

Anasema kuwa vikundi vingi vya vijana vina mapato ya kila mwezi ya shilingi 1.7 na hadi kima cha chini cha shilingi laki nne na anaeleza kuwa matokeo, yanakuja katika kipindi ambacho serikali imeshazielekeza mamlaka zote za mitaa kutenga ardhi ya kutosha kwa ajili ya vijana, pamoja na taasisi za fedha ili kutoa mitaji inayohitajika.

Ofisa Kilimo Kijiji cha Mdeki wilayani Kilolo, Fred Ngaelo, anasema mradi wa Ajira Plus umeongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za uzalishaji kwa kiasi kikubwa na kutokana na mwitikio huo, ni wazi mafanikio ya kijana mmoja mmoja pamoja na kikundi yataonekana.

"Vijana walikuwa wanafanya shughuli za kilimo, ufugaji na biashara bila ya kuwa na elimu, lakini kufuatia mradi huu (Ajira Plus) tunaamini utaenda kubadilisha fikra za vijana wengi na kufanya shughuli zao kisasa zaidi.'" anasema Ngaelo.

Hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa wito kwa vijana nchini kujishughulisha na kilimo na kueleza kuwa halmashauri zote nchini zimeelekezwa kutenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya programu maalum ya kuwawezesha vijana kushiriki katika sekta hiyo muhimu.

Akaeleza kuwa fursa zinazotokana na sekta ya kilimo ni nyingi, na hivyo kuwataka vijana kuchangamkia fursa hizo na kuwatoa hofu vijana kuhusu upatikanaji wa mitaji na kusema mikopo ipo kwa maelekezo ya serikali kwa benki zote nchini kutenga eneo la mikopo kwa ajili ya wakulima na wajasiriamali.

Utafiti unaonyesha kuwa kuna vijana wengi Kilolo wanaamini kuwa Ajira Plus ni miongoni mwa suluhisho la kukabiliana na matatizo ya ukosefu wa ajira nchini huku jitihada hizi zikienda sawa na kudumisha mikakati ya maendeleo kimataifa na ndani ya nchi.

Katika hilo kuna ufafanuzi unaogusa Mpango wa Miaka Mitano ya Maendelo Awamu ya Tatu, Tanzania na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Umaskini, usawa kijinsia na mabadiliko ya tabia nchi.

BIASHARA

# Bomba la gesi baharini Russia – Ulaya lahujumiwa, nchi EU zachanganyikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI za Ulaya zimeanzisha uchunguzi kuhusu hujuma kwenye njia tatu za bomba kuu la gesi kutoka Russia, jeshi la wanamaji linashika doria katika bahari ya Baltic inayovuja gesi hiyo, huku polisi nayo inaimarisha ulinzi karibu na mitambo ya mafuta na gesi.

Ni nani aliyelipua mistari mitatu ya mita hiyo kwa jina Nord Stream kwa mara moja kwenye pwani ya Denmark na Sweden? Ni swali ambalo halina jibu ila wanadai wana uhakika ni hujuma, wala si bahati mbaya.

Leo ni siku ya tano tangu gesi kuanza kutoka katika mabomba yaliyoharibiwa yalipasuka kwa nguvu sawa kutoka katika kina cha mita 80 hadi juu na kutoa mapovu kwenye eneo kwa kipenyo cha kilomita moja.

Nusu ya gesi inayopatikana kwenye mkondo uliokatika uliojazwa wa Nord Stream. Meli za kivita za Ujerumani na Denmark, hulinda eneo lililofungwa kwa usambazaji ndani ya eneo la maili tano za baharini.

"Mlipuko huo ulikuwa na nguvu sana, kwa hivyo itachukua muda kabla ya kuzama ndani ya maji huko," anasema Waziri wa Ulinzi wa Denmark Morten Bedskov.

"Kwa kweli inaweza kuchukua wiki moja au hata mbili kabla ya kila kitu kutulia hapo na tunaweza kuangalia eneo hilo tu," anasema na kuongeza, imegundulika kuwepo milipuko miwili kwenye mkondo wa kwanza na wa pili wa Nord Streams Jumatatu na sauti iliyofuata gesi ikitoka kwenye bomba.

Anathibitisha hitimisho lililotolewa siku moja kabla na mamlaka ya nchi tatu za pwani kwamba milipuko mitatu kwenye nyuzi mbili za bomba la gesi ilikuwa hujuma. Sababu za asili za ajali hazijajumuishwa.

"Sio bahati mbaya. Kila kitu kilipangwa, kimepangwa kwa uangalifu," anasema Bedskov.



Meli ya kivita ya Denmark ikiwa karibu na kisiwa cha Bornholm, katika doria ya bomba, jirani na eneo la tukio. **PICHA: MTANDAO.**

**HALI IKOJE?**

Russia inatajwa kupoteza bomba kubwa na mpya zaidi la gesi kwenda Ulaya, ambayo hata hivyo, haikupeleka gesi, kwani Ujerumani haikuthibitisha mstari mmoja na Kremlin ilizuia mwingine katika duru iliyofuata ya vita vya gesi dhidi ya EU, ikiwa ni katika jaribio la kutoa shinikizo na kuweka vikwazo kwa shambulio la Ukraine.

"Je, tunavutiwa na hili? Hapana hatupendezwi. Tumepoteza njia za usambazaji wa gesi kwenda Ulaya," anatamka Msemaji Dmitry Peskov, akiyaambia mashirika ya habari ya Russia.

Anakumbuka kuwa Marekani ikiwa inaongoza duniani kwa nishati ya mafuta na gesi, inafaidika kutokana na kupunguzwa usambazaji kwenye soko la Ulaya na kutokana na kupanda kwa bei ya gesi.

"Tunaona faida kubwa kutoka kwa wasambazaji wa gesi ya kimiminika wa Marekani, ambao wamezidisha usambazaji wao katika Bara la Ulaya. Wana nia kubwa ya kupokea faida hizi kubwa," Peskov alinukuliwa na chombo cha habari.

Ulaya imeweka dau kwenye Nord Stream kama chanzo kikuu cha gesi kwa miongo kadhaa, hata hivyo ikapata vikwazo katika vita vya Russia na Ukraine vinavyoendelea.

Awali, Marekani ilikuwa ikipinga mradi kama huo Nord Stream 2. Vikwazo dhidi ya mradi huo viliwekwa na Rais Donald Trump katika zama zake, lakini Rais aliyefuata, Joe Biden, akafuta vikwazo hivyo.


• ***Kwa mujibu wa BBC.***

---

Dondoo: Kulia
3. Binadamu
5. alikuwa Rais mweusi Marekani
6. mwendesha mitambo
10. Mji mkuu wa Mali
14. ng'ata kwa meno
15. sehemu ya kwanza ya Biblia
17. cheti 18. miezi 3 anayokaa mwanamke Muislamu aliyeachika
20. mnyama mjanja katika hadithi
21. aina ya kahawa


Chini:
1. Rabat ni mji mkuu
2. Zamani
3. mpinzani mkuu Afrika Kusini
4. kuwa wa awali kufanya jambo
7. kwa taratibu
8. toka chini na kwenda juu
9. mchezo wa kutumia kipande cha mti baina ya timu mbili
10. karatasi inayotiwa barua
11. omba ruhusa ya kuondoka
12. mboji 13. ndege mwenye mkia mrefu 16. Utaji wa Waislamu kuswali 19. vumbua


CHEMSHABONGO NA -00 1 00-



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| MAZINGIRA | WALI |
| WAMASAI | IRAN |
| KIANGAZI | AGUA |
| ALAMINA | MNAA |
| KANISANI | AZMA |
| MAZIWA | ASALI |
| PASAKA | AKILI |
| MPAKA | ADAA |
| MMEA | AGUA |
| KAMA | GARI |
| KALILI | ALA |
| AMANI | NIA |
| ASISI | GIA |





maoni: 0755429240



## HABARI MBEYA

## Waumini wafanya usafi kwa shughuli za kijamii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAISLAMU jamii ya Waismailia mkoani Mbeya wamejitokeza kufanya usafi wa mazingira, kupanda maua na kuboresha baadhi ya miundombinu ya barabara ikiwa ni sehemu ya kushiriki kazi za kijamii.

Walishiriki kazi hizo juzi ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Ismailia Duniani ambapo walifanya usafi kwenye maeneo yote ya njiapanda za katikati ya Jiji la Mbeya.

Msemaji wa Jumuiya ya Ismailia Mkoa wa Mbeya, Afzal Bhojani, alisema walifanya usafi kwenye minara yote iliyoko katikati ya Jiji la Mbeya na kupaka rangi kwenye maeneo ambayo yalikuwa yamechakaa.

"Tumeamua kufanya tendo hili kwa sababu tumeona mazingira yetu yamechafuka. Tumepanda maua na tutaendelea kuyahudumia mpaka yastawi vizuri," alisema Bhojani.

Baadhi ya viongozi wa serikali wanaosimamia mazingira katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya waliishukuru taasisi hiyo kwa kufanya usafi huo kwa maelezo kuwa wamekuwa ni mfano wa kuigwa na taasisi zingine za kijamii.

Mmoja wa viongozi hao, Nehemia Mwakatobe, ambaye ni Ofisa Mazingira wa Jiji la Mbeya, alisema maeneo hayo yanakabiliwa na hali mbaya kutokana kutofanyiwa usafi kwa muda mrefu na hivyo akawashukuru waumini wa dini hiyo kwa kujitolea.

Alisema taasisi zingine ambazo zinataka kufanya kazi kama hiyo zinakaribishwa kutokana na maeneo mengine ya jiji hilo kuwa na hali mbaya.

Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa, alitoa wito kwa viongozi wa dini kuendelea kudumisha amani ya nchi kwa kusaidia kukemea mambo maovu ili taifa lipate maendeleo kwa haraka.

Alisema nchi yoyote hupata maendeleo endapo kuna hali ya amani na utulivu.

# Mbaroni tuhuma kubomoa nyumba za mwenzao wakimdhania mchawi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wanane wakazi wa kijiji cha Ibula, Kiwira Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kubomoa nyumba ya mwananchi mwenzao wakimtuhumu kuwa ni mchawi.

Wananchi hao walibomoa nyumba za Lucia Kasebele (50) mkazi wa kijiji hicho Septemba 25, mwaka huu, na kubondabonda mifugo yake hali iliyozua taharuki kwa baadhi ya viongozi wa serikali katika wilaya hiyo.

Hali hiyo ilimfanya mama huyo pamoja na familia yake kubaki bila makazi, hivyo Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, kuagiza polisi kuwakamata wahusika na kuwasweka ndani ili kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa maofisa wake wamefanya msako katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo na kuwakamata watu wanane ambao walikuwa vinara kwenye tukio hilo.

Kamanda Kuzaga alisema tukio hilo lililofanywa na wananchi hao lilisababisha hasara ya Sh. milioni 2.5 ambazo ni gharama za nyumba pamoja na mifugo ambayo waliipiga.

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni Lupakisyo Mwanjisi (40) mkazi wa Igogwe, Nelson Mwakyeja (34), Lusekelo Mpangata (24), Maneno Ndabili (31), Semen Lucky (37), Abel Mwaisumo (42), Fanuel Peter (39) na Daves Foni (22) wote wakazi wa kijiji hicho cha Ibula.

Watuhumiwa hao, alisema walikuwa wanamtuhumu mwenzao huyo kuwa ni mchawi ambaye alisababisha kifo cha kijana Elikachi Mwambungu ambaye alifariki dunia Septemba 21, mwaka huu, baada ya kuugua kichwa.

"Watuhumiwa wote tuliwapeleka katika mahabusu ya Tukuyu na tayari tumeshawafikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya hatua za kisheria. Kitendo walichokifanya ni cha kinyama sana na hatuwezi kuwaacha," alisema Kamanda Kuzaga.

Aidha, Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linaendelea kuwasaka viongozi wa kijiji hicho ambao ni Mwenyekiti wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ibula ambao walitoroka na kutokomea kusikojulikana baada ya kutekeleza tukio hilo.

Katika tukio lingine, Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linamshikilia Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Sangambi wilayani Chunya, Joseph Nangale (45), kwa tuhuma za mauaji ya dereva bodaboda, Aaron Mbuba (18) mkazi wa kijiji cha Chalangwa wilayani humo.

Kamanda Kuzaga alisema ofisa mtendaji huyo alimuua kijana huyo kwa kumpiga na kitu butu kichwani akishirikiana na askari mgambo wa kijiji hicho ambao walikuwa kwenye operesheni ya kuwasaka wauza mkaa wasio na vibali.

Alisema ofisa huyo pamoja na mgambo wa kijiji walimkamata kijana huyo akiwa amepakia mkaa kwenye pikipiki na walipomtaka alipe ushuru wa kijiji, aliwajibu kuwa hakuwa na fedha ndipo wakaanza kumshambulia kwa kumpiga sehemu mbalimbali za mwili.

Alisema kijana huyo alishambuliwa Septemba 17 na baada ya hapo walimweka kwenye mahabusu ya kijiji mpaka Septemba 19, ambapo alidhaminiwa na kuruhusiwa kutoka.

"Baada ya kudhaminiwa kijana huyo alipelekwa katika zahanati ya kijiji cha Sangambi kwa ajili ya kupatiwa matibabu na wakati akiendelea na matibabu hayo, Septemba 20 alifariki dunia kutokana na majeraha aliyokuwa amepata kwa kupigwa," alisema.

Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linaendelea kuwasaka mgambo wa kijiji hicho ambao walikimbia baada ya tukio hilo na kwamba ofisa mtendaji anaendelea kushikiliwa.




Mjasiriamali wa dawa za asili aina ya mlonge, akizungumza na wateja wake katika eneo la Sokoine, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafugaji mbwa wana mwamko mdogo chanjo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanaofuga mbwa wana mwamko mdogo wa kuwachanja wanyama hao ili kuwakinga na maambukizi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Hali hiyo imeelezwa kuwa inaufanya ugonjwa huo kuendelea kuambukiza na kuathiri watu.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Benard Mbwele anayefundisha masomo yanayohusu mazingira, afya na magonjwa ya kuambukiza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani.

Alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa watu 60,000 wanafariki dunia kila mwaka kutokana na kichaa cha mbwa jambo ambalo alisema linahitaji jitihada kubwa kukabiliana nalo.

Dk. Mbwele alisema kwa Tanzania tatizo hilo ni kubwa zaidi maeneo ya vijijini ambako wananchi wanaishi na mbwa bila kuwachanja. Alisema hiyo inasababisha mbwa hao kuambukizwa ugonjwa huo na kisha kuendelea kuusambaza kwa binadamu.

"Takwimu zinaonyesha kwamba idadi kubwa ya watoto wanaopata matatizo mbalimbali ya kiafya yakiwamo kichaa au ugonjwa wa akili, hutokana na kichaa cha mbwa. Hali hii inasikitisha sana maana tatizo hilo linaepukika kwa kuchanja wanyama hao," alisema Dk. Mbwele. Alisema ugonjwa wa kichaa cha mbwa hauna tiba isipokuwa unazuilika kwa kuchanja mbwa, hivyo akawataka wananchi kuchanja mbwa wao ili kuepuka madhara hayo.

Vilevile alisema ugonjwa huo kwa bara la Afrika unaathiri zaidi mataifa yaliyoko kusini mwa Jangwa la Sahara ambako Tanzania ni miongoni mwa mataifa hayo.

Chama cha Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi Mbeya (MCHAS), ambao ni wanachama wa Chama cha Mazingira, Wanyama na Binadamu, wamejitosa kutoa elimu kwa wananchi wa mkoa wa Mbeya.

Wanafunzi hao walisema wameamua kutoa elimu kwa wananchi kwa sababu ugonjwa huo umekuwa tishio na unaathiri wananchi kwa kiwango kikubwa.

Mmoja wa wanafunzi hao, Leokadia Michael, alisema chama chao kinafanya kazi kuhakikisha maisha ya binadamu yanakuwa salama kwa kuyaweka mazingira kuwa na afya.

"Sisi tunaamini kwamba binadamu hawezi kuwa salama endapo mazingira yanayomzunguka hayako salama, kwahiyo tumeungana kwa ajili ya kutoa elimu ili wananchi wajuwe tatizo hili na wachukue tahadhari," alisema Michael.

Naye Mariam Mwasumbule alisema ugonjwa huo unaambukiza endapo mbwa mwenye maambukizi atalamba kidonda cha binadamu au kutumia chombo kimoja kula na mbwa mwenye maambukizi.





# Wafugaji wamwagiwa bil. 1.2/- za maendeleo

**Na Renatha Msungu** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imetoa Sh. bilioni 1.2 kwa vikundi vya wafugaji kwa ajili ya ununuzi wa ng'ombe 487 wa maziwa ili kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Biashara Mwandamizi wa TADB, Daniel Mwalyayo, alisema hayo jana kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mikopo wa benki hiyo wakati wa kilele cha Siku ya Maziwa Duniani iliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square, jijini hapa.

Mwalyayo alisema mikopo hiyo itachochea ongezeko la uzalishaji wenye tija wa maziwa nchini kutokana na mradi kuwa na faida.

Akikabidhi mfano wa hundi kwa viongozi wa vyama vya ushirika na ufugaji, alisema mradi huo wa ushirikiano wa wazalishaji na wasindikaji maziwa (TI3P) ulizinduliwa mapema mwaka huu na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

"Tunafurahi kuona mradi huu wa kimkakati unakwenda kuleta mapinduzi yenye manufaa katika jamii yetu ya wafugaji na wasindikaji ikiwamo kuleta maendeleo," alisema Mwalyayo.

Akizungumzia walivyonufaika na mkopo huo, Salehe Lubuva alisema wamepokea ng'ombe bora wenye ubora ambao wanaaamini watawasaidia kuzalisha maziwa kwa wingi huku akiishukuru TADB kutokana na kuwapa fedha hizo ambazo zimenunua ng'ombe wa kisasa.

"Awali tulikuwa hatuna uhakika wa kuzalisha maziwa ya kutosha lakini kwa sasa tutazalisha maziwa ya kutosha," alisema Lubuva.

Naye Edmund Mariki, Ofisa Biashara Mwandamizi katika mradi wa ushirikiano wa wazalishaji na wasindikaji, alisema unywaji maziwa shuleni ni jambo muhimu kwa kuwa maziwa yana virutubisho vingi na muhimu katika ukuaji wa watoto.

Alisema maziwa pia huchangia kuongeza mahudhurio ya wanafunzi kutokana na kupata virutubisho hivyo vya maziwa.

# AG aonya ukosefu maadili mawakili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, ametoa dondoo 10 kwa wanasheria wa serikali kwenye taasisi za umma huku akitoa onyo kuhusu ukosefu wa maadili na mifarakano isiyo na tija.

Dk. Feleshi aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akifungua kikao kazi cha wakurugenzi, mameneja na wakuu wa vitengo vya sheria kwenye taasisi za umma nchini.

Alisema watendaji hao wa sheria wanasimama kwa niaba ya serikali, hivyo mwajiriwa mkereketwa anayetaka kufanikiwa anapaswa kuzingatia dondoo 10 ikiwamo kuzingatia maadili.

Mwanasheria mkuu alisema kama kuna vitu vinavyowashinda ni vyema wakaacha kazi na kuondoka kuliko kuanzisha chokochoko kwenye ofisi za umma.

"Jitathmini umeajiriwa umeingia siku ya kwanza, mfano mwaka 2001 kwa mara ya kwanza niliteuliwa kuongoza ofisi ngazi ya kanda nilikuwa Kanda ya Mwanza. Tulikuwa na mafaili yalikuwa yanakuja yana vumbi hadi yanaota ukoko zaidi ya 1,000. Yalikuwa yakija yanatoka siku hiyo hiyo," alisema.

Mwanasheria huyo alisema alilazimika kujifunza kazi mbalimbali ikiwamo za masjala na kuunda mfumo ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Alisema kuna watu wanaamini wakienda kwao watapata haki, hivyo wawajengee matumaini lakini wengine wanashiriki kuhujumu.

"Sasa wewe unakuwa ni mtu wa mafarakano, utakuwa unajenga au unabomoa? Mengine ninayasema kwa sababu hii kaulimbiu yetu mjue thamani yake kuna watu ambao hawataipenda," alisema makusisitiza uadilifu ili kuwa na nguvu ya utashi ya kuchukua hatua. "Ukiwa ni mla rushwa halafu anamwambia mtu fanya hivyo, si anasema wewe ni wale wale. Lakini kama umesimamia lile neno lako la weledi litasimama. Lakini tumia kipato chako halali," alisema.

Alisema yeye alijenga nyumba yake kwa miaka minane, miaka mitatu alitumia kufyatua matofali kwa kuanzia na mshahara wa Sh.35,000 hadi Sh.50,000.

"Ukijijengea uwezo na kuwa mwadilifu unajiweka sokoni mwenyewe na maandiko yanasema utavuna mema ya nchi na mimi ni miongoni mwa watu waliokula mema ya nchi. Nyumba ya pili nilijenga kwa miezi sita," alisema.

Awali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Shabani Ramadhan Juma, alisema kikao hicho ni muhimu kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Mkutano huu ni muhimu sisi tutajifunza wenzetu mnavyofanya kazi ili na sisi kuiga utendaji wenu mzuri," alisema.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu na Naibu Wakili Mkuu, Dk. Boniphace Luhende, walisema kikao hicho ni muhimu kwa kupanga mikakati ya utekelezaji mzuri wa masuala ya sheria.



Ofisa Elimu Maalum wa Jiji la Dodoma, Issa Kambi (katikati), akizungumza wakati akifungua mafunzo ya afya ya kinywa na meno, kwa ajili ya wazazi wanaoishi na ulemavu jijini humo juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Special Olympics Tanzania, Charles Rays na Mjumbe wa Bodi wa Taasisi hiyo, Muharam Mchume. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Walia kukosa maji kisa umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANANCHI wa vijiji vya Seluka na Wiyenzele wilayani Mpwapwa, wanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya majisafi kutokana na mradi wa maji ulioko kwenye maeneo hayo, kushindwa kutoa maji hali inayohatarisha afya zao.

Wakitoa kilio chao jana kwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alipotembelea vijiji hivyo kukagua upatikanaji wa maji, Mkazi wa Seluka, Yona Kutala, alisema wananchi hao wanakabiliwa na kero ya maji hali inayosababisha kukosa hata ya kupigia mswaki.

"Mheshimiwa Waziri utaona kama vile wananchi wa Seluka wamenuna. Wanashindwa kucheka kwa sababu meno yao hayapo sawa, kupiga meno mswaki kunahitaji maji," alisema.

Mkazi mwingine, Esther Mgonela, alisema wanawake ndio waathirika wakubwa wa tatizo hilo kutokana na kushindwa kupika chakula kwa kukosa maji.

"Mwanamume akija akiuliza chakula kiko wapi unamwambia hakuna kwa sababu ya shida ya maji hakuelewi na unaambulia kipigo," alisema.

Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alisema mradi wa maji Seluka ulikamilika na watu walikuwa na matumaini makubwa lakini huduma haipo kutokana na ukosefu wa umeme.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Aweso, alitoa siku 30 kwa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuhakikisha huduma ya maji inatolewa bila kuwapo kisingizio chochote.

Alisema kama meneja wa RUWASA Mpawapwa atashindwa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwenye eneo hilo, anatakiwa kutafuta kazi ya kufanya.

Awali, Meneja wa RUWASA Mpwapwa, Cyprian Warioba, alisema kutokana na ukosefu wa umeme wa kuendesha mradi huo, wanaomba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kufikisha huduma kwenye eneo hilo.

"Kuhusu changamoto ya huduma ya maji, mtandao uliopo ni mdogo na kijiji kimetanuka, kutokana na ongezeko la watu," alisema.

# Mpango wa afya kwa wote waja

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kwa kushirikiana na mashirika ya maendeleo imekusudia kutengeneza mpango maalumu wa afya ili kuimarisha huduma za afya kwa wote bila ya ubaguzi.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa kujadili mpango wa pamoja baina ya serikali na mashirika ya maendeleo, uliofanyika jana mjini hapo, Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mpango huo unaotengenezwa, umelenga kuwasaidia wananchi wa vipato vyote kumudu gharama za matibabu .

Waziri Mazrui alisema huduma za afya Zanzibar ni bure kama sera inavyoeleza na ikitokea wananchi kachangishwa fedha, wengi hushindwa kumudu gharama hizo na kuamua kutumia dawa za miti shamba.

Alisema jambo hilo huchangia madhara zaidi, hivyo mpango huo endapo utafanikiwa, utawasaidia wananchi kupata huduma bora za afya.

Mazrui alisema wizara itahakikisha kila mwananchi anapata fursa ya matibabu bila usumbufu ili wananchi kunufaika na huduma kama ilivyo azma ya serikali.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kutumia fursa ya kuchanja chanjo zote zilizowekwa na serikali ikiwamo UVIKO-19, ebola, surua na polio ili kujikinga na magonjwa hayo ambayo husababisha madhara.

"Kinga ni bora kuliko tiba, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kujikinga na magonjwa yote hatarishi," alisema. Naye Mkuu wa Sera za Kijamii, Diego Angemi, alisema Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) litaendelea kuiunga mkono Wizara ya Afya katika kuimarisha huduma za jamii ikiwamo afya.

Alisema shirika hilo lina imani na serikali ya Zanzibar katika mikakati yake ya kuimarisha huduma za afya, hivyo litahakikisha lengo la serikali la kuimarisha huduma za afya kwa wote Zanzibar linatimia.

Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Salim Slim, alisema katika mkakati huo wa serikali wa kuboresha huduma za afya, kutakuwapo na bima ya afya ili kila mwananchi kupata huduma hizo kwa urahisi.

# SMZ yaahidi kulinda vyanzo vya maji

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema vyanzo vya maji vilivyoko vijijini vitalindwa ikiwamo kujengewa uzio ili kudhibiti matukio ya uharibifu ikiwamo ujenzi wa nyumba za makazi ya kudumu.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Shaaban Ali Othman, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi na kujibu ripoti za Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza hilo. Alisema vyanzo vingi vya maji viko katika hatari ya kutoweka kutokana na kasi ya harakati za wananchi za ujenzi wa nyumba za kudumu.

Shaaban alivitaja baadhi ya vyanzo vya maji ambavyo viko katika hatari ya kutoweka pamoja chemchemu Maarugu ya Mwanyanya iliyoko Mjini Magharibi, Unguja.

Pia alisema baadhi ya vyanzo muhimu vya majisafi na salama vimekumbwa na changamoto kutokana na kasi ya ujenzi hadi kutoweka ikiwamo Masingini, Unguja.

"Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji, Nishati na Madini inakabiliwa na tishio la vyanzo vya majisafi na salama kutoweka kutokana na kasi ya ujenzi holela wa makazi ya kudumu ya wananchi," alisema.

Kutokana na hatari hiyo, alisema hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ili kulinda vyanzo hivyo ikiwamo kuzungushia uzio vyanzo vyote vya maji na kazi hiyo imeanza kwa upande wa Kiyanga, Unguja.

Alisema kuwapo kwa mabadiliko ya tabianchi ni miongoni mwa sababu za kuwapo kwa uhaba mkubwa wa maji ambao umechangiwa kutoweka kwa vyanzo vya maji.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, kuwapo kwa mabadiliko ya tabianchi, baadhi ya vyanzo vya maji vimekuwa na mchanganyiko wa maji yenye ladha ya chumvi zaidi katika maeneo yanayopakana na bahari.

"Tunakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi ambayo nayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa uhaba wa maji na kutoweka kwa vyanzo hivyo," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rajab Yussuf Mkasaba, akishiriki kuvuna nyanya katika shamba la ushirika wa Kumekucha, Mzuri Makunduchi, wilayani humo juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# DC asema ujasiriamali ndio mpango mzima

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rajab Yussuf Mkasaba, amesema serikali ya Zanzibar itaendelea kuwaunga mkono wajasiriamali wote ili kuhakikisha wanafikia malengo yaliyokusudiwa katika kupambana na umaskini na kujikwamua kiuchumi.

Mkasaba aliyasema hayo jana baada ya kushiriki uvunaji wa nyanya katika shamba la Ushirika wa Kumekucha, Shehia ya Mzuri Makunduchi katika Wilaya ya Kusini Unguja.

Aliwapongeza wanaushirika hao kwa kuzitumia vyema fedha za mkopo wa UVIKO- 19 na kuendeleza kilimo cha mboga ambacho kinawapa tija na kujikwamua kimaisha.

Mkasaba alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuwakumbuka wajasiriamali na kuwawekea fedha nyingi ili kukopa na kuendesha shughuli zao za kimaendeleo.

Alisema ushirika huo umeonyesha mfano mkubwa wa kuthamini fedha za mkopo ambazo wamezifanyia mradi mkubwa wa kilimo cha mboga.


Mkuu huyo wa wilaya pia aliwasisitiza wanaushirika hao kuendelea kushirikiana ili kupata maendeleo makubwa zaidi katika ushirika wao.

Alisema iwapo wataendelea na juhudi zao hizo katika kuimarisha sekta ya kilimo kwa kujikusanya pamoja na kuunda ushirika huo na kuomba mkopo hatimaye kuutumia vizuri, kuna uwezekanao mkubwa wa kupewa kipaumbele pale watakapomaliza mkopo na kuamua kukopa kwa mara nyingine.

Akisoma risala ya ushirika huo, Rehema Issa Ameir ambaye ni miongoni mwa wanakikundi, alisema Juni 6, mwaka huu, walipata mkopo na kuanza kushughulikia kilimo cha mboga. Alisema kutokana na mkopo huo wamekuwa na mafanikio, hivyo kumshukuru Dk. Mwinyi kwa juhudi zake hizo ambazo zimeanza kuleta mabadiliko katika maisha yao.

Kuhusu historia ya ushirika huo, Rehema alisema ulianzishwa Machi 3, 2012 ukiwa na wanachama 20 na ulianza na kilimo cha migomba kwa muda na baadaye wakaona haja ya kuingia katika kilimo cha mboga ambacho wanaendelea nacho.

Alisema changamoto waliyo nayo ni kukosa umeme wa uhakika na usio salama kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za kilimo.





## Wenye ulemavu walalamikia masharti magumu ya mikopo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJASIRIAMALI wenye ulemavu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia uwapo wa masharti katika upatikanaji wa mikopo isiyokuwa na riba.

Moja ya sharti wanalolalamikia ni pamoja na kuwa na leseni ya biashara hali ambayo inawafanya kukosa mikopo hiyo kupitia mjasiriamali mmoja mmoja.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Msaidizi wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) wilayani Kahama, Edward Charles, alipozungumza na Nipashe kuhusu mambo yanayowakwamisha wanapoomba mikopo.

Charles ambaye ni fundi viatu alisema wao hawana shughuli kubwa inayowafanya kuwa na leseni ya biashara na kwamba taasisi za fedha zinakataa kuwakopesha.

Kabla ya kanuni za uchukuaji wa mikopo ya asilimia mbili inayotengwa na halmashauri kupitia mapato yake ya ndani kwa wajasiriamali wenye ulemavu walipata, lakini kwa sasa wanaweza kuchukuku mmoja mmoja kwa sharti la kuwa na shughuli ya kumwingizia kipato.

Alisema wajasiriamali wenye ulemavu wanashindwa kukuza biashara zao kutokana na ukosefu wa mitaji ya asilimia mbili inayotolewa na halmashauri kutokana na masharti magumu katika mikopo hiyo ikiwamo kuwa na leseni ya biashara.

"Bora mwanzo tulivyokuwa tunakusanyika kupitia vikundi tulivyokuwa navyo, tunaomba na tunapata mikopo tunagawana na kuziingiza kwenye shughuli za ujasiriamali, lakini kwa sasa kumekuwa na masharti makubwa hadi mitaji tuliyokuwa nayo tumeanza kupunguza," alisema Charles.

Pia alisema ujasiriamali unawasaidia wengi kutoingia barabarani kuomba omba lakini kazi ya kufanya watarudi huko.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Kahama, Robert Kwela, alisema wamekuwa wakitoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vyote vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hususani wale wenye shughuli ya kuwaingizia kipato.

Alisema mwaka huu wa fedha 2022/23 manispaa imetenga Sh. milioni 147.8 kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wenye ulemavu ili kukuza mitaji yao ili kujikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemezi ndani ya jamii na familia zao.

Aidha, alisema mwaka wa fedha uliopita walifanikiwa kutoa mikopo isiyokuwa na riba kwenye vikundi 20 vya watu wenye ulemavu.

# Madudu yaibuliwa ukusanyaji wa mapato madini ya ujenzi

**Na Richard Makore,** MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Mwanza imebaini madudu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madini ya ujenzi yakiwamo kokoto, mawe na mchanga.

Katika eneo hilo, TAKUKURU imebaini kwamba wakusanya mapato hukaa njiani na kuvizia magari yaliyobeba madini hayo na kuyatoza ushuru, lakini fedha hizo hazifiki serikalini (halmashauri).

Akitoa taarifa ya TAKUKURU hivi karibuni, Mkuu wa taasisi hiyo mkoani Mwanza, Frank Mkilanya, alisema wakusanya ushuru hao wanatumia utaratibu ambao unainyima halmashauri mapato badala yake fedha hizo zinaingia mifukoni mwao.

Pia alisema Mkoa wa Mwanza kuna leseni nyingi zilizotolewa za uchimbaji madini hayo lakini hakuna maeneo maalum yaliyotengwa na halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo.

Alisema hatua hiyo inawafanya watu kuchimba holela madini hayo na hivyo kuharibu mazingira pamoja na kuikosesha serikali mapato yake.

Kuhusu mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, Mkilanya alisema wamebaini urejeshwaji wake ni wa kusuasua tofauti na walivyokubaliana.Alisema uchambuzi wa mifumo ya mikopo inayotolewa na halmashauri imebaini kuna idadi ndogo ya watu wanaorejesha mikopo hiyo ili kutoa fursa kwa watu wengine kukopa.

Mkilanya alitoa mfano kuwa kufikia Juni, mwaka huu, fedha zilizokopeshwa kwa makundi 65 ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ilikuwa Sh. milioni 220 na kati ya hizo, zilizorejeshwa ni Sh. milioni 110 katika Wilaya ya Kwimba.

Aliongeza kuwa licha ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa makundi hayo kufanyiwa marekebisho mwaka 2022, lakini hazifuatwi jambo linalochangia kuwapo ufuatiliaji mdogo katika ukusanyaji.

Kwa hatua nyingine, TAKUKURU mkoani Mwanza imesema imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofikia 22 yenye thamani ya Sh. bilioni 27.

Miradi hiyo ya afya, elimu, barabara, maji, usafi wa mazingira na afya, ilikaguliwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu.

Katika ufuatiliaji huo TAKUKURU ilibaini mapungufu kadhaa katika miradi ya afya, maji na elimu ikiwamo kuchelewa kukamilika kwake kwa mujibu wa mkataba.



Wafanyabiashara wakisaidia kusukuma mkokoteni uliosheheni mikungu ya ndizi, eneo la Kamanga, baada ya kushushwa kwenye meli katika Bandari ya Mwanza ikitokea mkoani Kagera, kwa ajili ya kwenda kuziuza katika masoko mbalimbali jijini humo juzi. Mkungu mmoja wa ndizi unauzwa kwa bei ya 20,000/- hadi 25,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Serikali yawahakikishia ulinzi wazee

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imewahakikisha wazee mkoani humo ulinzi wa maisha yao huku ikiahidi kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaowafanyia vitendo vya kikatili yakiwamo mauaji yanayohusisha imani potofu za kishirikina.

Septemba 20, mwaka huu, katika kijiji cha Kazuni Kata ya Bukene wilayani Shinyanga, kulitokea mauaji ya Sophia Dotto (66) kwa kushambuliwa kichwani na watu wasiojulikana nyumbani kwake majira ya saa 2:00 usiku wakidai mshirikina.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, alibainisha hayo juzi wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani mkoani humo yaliyofanyika Kata ya Mwamalasa wilayani humo.

Alisema serikali itaendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa watu ambao bado wanaendekeza tabia ya kuwanyanyasa wazee, kuwatelekeza pamoja na kuwaua kwa sababu ya imani potofu za kishirikina.

"Serikali itaendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa watu ambao wataendelea kuwanyanyasa wazee wetu kwa namna yoyote ile," alisema Mkude.

Aidha, aliziagiza halmashauri zote mkoani humo kuendelea kuwatambua wazee na kuwapatia kadi za matibabu bure pamoja na kutengwa madirisha ya wazee kwa kila kituo cha afya na zahanati ili kuwapatia huduma za afya.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wilayani Kishapu, Suzana Masebu, akisoma risala yao, aliiomba serikali kuendelea kutatua matatizo yanayowakabili hususani upatikanaji wa matibabu bure pamoja na kuzuia mauaji dhidi yao yatokanayo na imani potofu za kishirikina.

"Tunaishukuru serikali kwa kuendelea kuheshimu na kutambua mchango wa wazee na kukemea vitendo vya unyanyasaji na kuchukua hatua kwa wanaokiuka haki za binadamu. Tunaomba pia elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu Sera ya Taifa ya Wazee, haki na wajibu wa kuwalinda wazee," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

# Maeneo yaliyotekwa Ukraine kuunganishwa rasmi Russia

**MOSCOW, Russia**

RAIS wa Russia, Vladimir Putin atafanya hafla maalum ya utiaji saini ya kuunganisha majimbo manne yanayokaliwa na vikosi vyake nchini Ukraine.

Katika mkutano huo, Rais Putin atatoa hotuba katika Ikulu ya huko Kremlin, kutangaza maeneo hayo manne kama sehemu ya Russia.

Viongozi wanne wanaoungwa mkono na Russia, wamewasili jana mjini Moscow kuhudhuria mkutano huo baada ya siku chache kumtaka Rais Vladimir Putin kuyanyakua rasmi maeneo hayo.

Viongozi hao walioidhinishwa na Russia katika maeneo ya Ukraine ya Lugansk, Donetsk, Kherson na Zaporizhzhia wanadai kuwa raia waliunga mkono hatua hiyo katika kura za maoni zilizoandaliwa haraka na ambazo nchi za Magharibi zinasema zilikuwa za udanganyifu.

Leonid Pasechnik, kiongozi wa eneo la Lugansk ameliambia shirika la habari la serikali TASS kwamba tayari wako nchini Russia kwa ajili ya mkutano huo.

Kiongozi aliyeteuliwa wa eneo la Kherson, Kirill Stremousov, alisema katika kipindi cha redio kinachoiunga mkono Russia kwamba mkutano umepangwa kati yao na Putin lakini kufikia sasa hana habari na hawezi kusema utakuwa wapi ama lini.

Hata hivyo, shirika la habari la Reuters limechapisha picha ya jukwaa lililojengwa katika medani ya Red Square mjini Moscow kama maandalizi kwa ajili ya mkutano wa kuunga mkono kutwaliwa kwa majimbo hayo.

Kulingana na vyombo vya habari vya Russia, mkutano huo unafanyika leo.

Kulingana na picha hizo, tukio hilo litafanyika chini ya kauli mbiu kama inayosema "Donetsk, Lugansk, Zaporozhye, Kherson na Russia pamoja daima." ht: Reuters

Maandalizi ya mkutano yameripotiwa na vyanzo vya shirika la habari la Russia (TASS).

Taarifa kuwa eneo hilo linalofahamika kama Red Square litakuwa limefungwa imethibitishwa na ofisi ya meya wa mji wa Moscow.

Mapema Jumatatu, BBC iliripoti ikinukuu vyanzo vyake kwamba Rais Vladmir huenda akazungumza katika mkutano huo.

Kulingana na taarifa ya gazeti moja, kiongozi huyo wa Russia huenda akakutana na viongozi waliojitangazia utawala kwenye majimbo ya Ukraine yaliyovamiwa na Russia Jumatano.

Kulingana na vyanzo vya habari vya Russia, bunge la taifa l huenda likapiga kura kwa ajili ya kujitenga kwa maeneo yaliyovamiwa Oktoba 3, na Baraza la Shirikisho litaidhinisha uamuazi huo siku moja baadaye.

Mamlaka za nchi hiyo ziliendesha kura ya maoni juu ya maeneo ya Ukraine yaliyo chini yake kujiunga na Russia. Ukraine na washirika wake wa Magharibi wamesema kuwa utaratibu huo uliandaliwa katika hali za kivita na uvamizi hauwezi kuwa halali kisheria.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alitaja kura ya maoni ni sawa na maigizo, ambayo matokeo yake yalikuwa yanajulikana na waandaaji mapema.

Wakati huo huo, Wizara ya mambo ya nje ya Russia, imesema kwamba kupasuka kwa mabomba ya gesi ya Nord Stream ambayo yanasababisha kuvuja kwa gesi katika Pwani za Denmark na Sweden, kumetokea katika eneo lililoko chini ya udhibiti kamili wa taasisi za ujasusi za Marekani.

Katika mahojiano na shirika la habari la mtandaoni linaloiunga mkono Russia, msemaji wa wizara hiyo Maria Zakharova, alisema Marekani ilikuwa na udhibiti kamili katika bahari karibu na Sweden na Denmark mahali uvujaji katika maeneo manne uligunduliwa.

Mabomba yaliyopasuka ni Nord Stream 1 na Nord Stream 2 yanayovuka sakafu ya bahari ya Baltic kati ya Russia na Ujerumani.

Zakharova hata hivyo hakutoa ushahidi wa udhibiti wa Marekani katika eneo hilo.

Russia mara kwa mara hulalamika kuhusu ushawishi na msaada wa kijeshi wa Marekani kwa Ulaya.

*BBC*



Meli ya kivita ya Denmark karibu na eneo la bomba la gesi lililopasuka katika bahari ya Baltic. **PICHA: EPA**

## Wanafunzi waandamana kupinga bunge la Ulaya

**KAMPALA, Uganda**

MAMIA ya wanafunzi wa Uganda wanaandamana kupinga hatua ya bunge la Ulaya, kuzuia ujenzi wa mradi wa mafuta unaoanzia nchini humo hadi Tanzania.

Hivi karibuni wabunge wa Ulaya walipitisha azimio la kuonya kuhusu ukiukaji wa haki za binadamu na hatari za kijamii na mazingira zinazoweza kusababishwa na mradi huo.

Wanafunzi hao waliandamana mjini Kampala kufikisha hoja yao kwa ubalozi wa Ulaya nchini humo.

Maandamano hayo yalionekana kuidhinishwa na taifa hilo, wanafunzi wakitembea huku wakisindikizwa na polisi.

Ujenzi wa bomba hilo la mafuta lenye urefu wa km 1,443 sawa na maili 896 ni kutoka Ziwa Albert magharibi mwa Uganda hadi kwenye bandari ya Tanga nchini Tanzania.

*BBC*

## Truss atetea punguzo la kodi

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza Liz Truss, amevunja ukimya wake kufuatia takriban wiki moja ya misukosuko katika masoko ya fedha iliyosababishwa na mipango yake ya kupunguza kodi.

Truss alisema yuko tayari kuchukua maamuzi magumu kuchochea ukuaji wa uchumi.

Hatua hiyo imekuja siku moja baada ya Benki Kuu ya Uingereza kufufua mpango wake wa ununuzi wa dhamana katika hatua ya dharura ya kulinda mifuko ya pensheni dhidi ya uwezekano wa kuporomoka kwa kiwango fulani.

Kiongozi huyo alisema misukosuko hiyo imetokana na uvamizi wa Russia nchini Ukraine ambao umesababisha mfumuko wa bei ulimwenguni.

Katika mfululizo wa mahojiano na shirika la habari la BBC, Truss alisema kuwa iliwabidi kuchukuwa hatua za haraka kuchochea ukuaji wa uchumi na kufanya Uingereza iendelee na shughuli zake na pia kukabiliana na mfumuko wa bei ambapo analazimika kufanya maamuzi magumu na ya utata

**DW**

## Rais Museveni akataa karantini ya ebola

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amesema hakuna sababu ya kuweka vikwazo katika maeneo yenye maambukizi makubwa ya Ebola, kutokana na kwamba virusi havitokei hewani.

Ebola huenezwa kwa njia ya kugusana na mtu aliyeambukizwa au sehemu zilizoambukizwa na kinyesi cha binadamu.

Chama cha wafanyakazi wa tiba nchini humo kilitoa wito kwa eneo lililoathiriwa kuwekwa karantini ili kukomesha kuenea zaidi kwa homa ya kuvuja damu.

Rais Museveni alisema serikali yake ina uwezo wa kudhibiti janga hilo kutokana na uzoefu wa awali wa milipuko kama hiyo.

Hii ni mara ya nne kwa Ebola kuzuka nchini Uganda. Alisema wataalam wa afya ambao hapo awali walishughulikia milipuko ya Ebola wametumwa katika eneo lililoathiriwa.

Alisema serikali itafungua maabara katika makao makuu ya wilaya ya Mubende, kitovu cha mlipuko huo, ili kuharakisha usindikaji wa sampuli.

Wahudumu sita wa afya waliomtibu mwanamume huyo mwenye umri wa miaka 24 ambaye baadaye alitambuliwa kuwa kisa cha kwanza, wamepimwa na kukutwa na Ebola.

Jumla ya watu 24 wamethibitishwa kuambukizwa na virusi hivyo nchini humo, watano kati yao wamefariki tangu kuzuka kwa ugonjwa huo wiki iliyopita.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LOVENESS D. MLACHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0536-0021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KINDOROKO SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/384840/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na 56/....2022**
**JINA LA MDAI: JOSEPHINE PHILIPO MACHOCHO**
**JINA LA MDAIWA: FESTO ELIFASI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: FESTO ELIFASI WA MTWARA......MDAIWA**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Kuomba kuvunja mahusiano na kupatiwa talaka. Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 04/10/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO:Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28/09/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KIJAKAZI SAID ABDALLAH**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya Pikipiki (t better) yenye namba za usajili **T 736AUG** ,Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi au piga simu namba **0718122326**

**MOR/MOR/RB/384382/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......50/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MSAFIRI A. SHABANI WA TUNGI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA RAMADHANI A. SHABANI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 03Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 09 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS BEFORE THE COMMISSION FOR MEDIATION AND ARBITRATION**
**((Made under Regulation 34(1))**
**Labour Dispute No. CMA/DSM/KIN/257/2022/205/22**
**Between**
**ARLENE CAROLINA GOMES ............Complainant**
**And**
**MINING AGRICULTURE AND CONSTRUCTION SERVICES LIMITED...... Respondent**

**NOTICE TO ATTEND ARBITRATION HEARING**

Take notice that the above mentioned Arbitration has been fixed for hearing on 10th day of October, year **2022** at **09.30 hours**, at
**DAR ES SALAAM ZONE, AKIBA-BIBI TITI ROAD.**
You are required to appear before the Commission in person and or accompanied by an Advocate/Personal representative as instructed, and produce on that day all relevant documents you intend to rely upon in support of your defence. You are further cautioned to remain in attendance until permitted by the Commission
**Given under my hand and seal of the Commission, this 26th day of September year 2022**

**Name: Massawe, Y.**
**Signature: M.Y**
**Arbitrator**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAJOGI (T) CO. LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 245 AMA – ISUZU-MODEL-TXD. Chassis namba 1647031.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/383879/2022**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**SOSTHENES ALON MFUGALE**
Anatangaza kupotelewa kwa vyeti,cheti cha kidato cha nne (2) dunda secondary school (index no **1969-0072-2014**, identity card alfagames,result slip kidato cha sita (alfagames),kitambulisho cha chuo (Tanzania institute accountancy) REG **NO SGD/BHRM/1967828,** kitambulisho cha karani wa sensa/cheti cha kuzaliwa.Na vyote vimepotea pamoja na vyeti vya vifo vya marehemu Aron mfugale na Yosepha Kalinga **DSM/PHQ/RB/386484/2022.**

---

**N THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 104 OF 2022**

In the Matter of the Estate of the Late:
**BATISTA MBALLA NGALALIKWA**

**BY 1. GRACE HENRY ZACHARIA**
All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above -named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 05 day of OCTOBER.........2022
Dated at MOROGO this 23 day of SEPTEMBER...2022

RESIDENT MAGISTRATE
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FAUSTINE HAMIS NYAMSANGYA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA **MARKX** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T862 CVV** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/1593/2022.**

---

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

Mimi **Anthony Amasi Joka** wa **S.L.P 841, Morogoro**. Natangaza kupotelewa na ofa ya kiwanja **Namba 44 Kitalu 'S' Mkundi** -Manispaa ya Morogoro Nimeripoti Polisi tarehe **18/08/2022** Kituo kikuu cha Polisi/Morogoro na kupewa Namba. **MOR/MOR/RB/334124/2022**. Atakayeipata atoe taarifa kituo cha Polisi alicho karibu nacho

---


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# RAPA COOLIO
## AFARIKI DUNIA AKIACHA WATOTO 10

**LOS ANGELES, Marekani**

RAPA wa Marekani Coolio, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 59 bafuni kwa rafiki yake aliyekwenda kumtembelea.

Coolio ambaye jina lake halisi ni Artis Leon Ivey Jr anayefahamika kwa nyimbo zake maarufu zaidi za "C U When U Get There" na "Gangsta's Paradise", amefariki kwa mshituko wa moyo.

Meneja wake wa muda mrefu, Jarez Posey aliviambia vyombo vya habari vya Marekani kuwa msanii huyo alipatikana akiwa hajitambui kwenye sakafu ya bafuni katika nyumba ya rafiki yake huko Los Angeles.

Coolio alianza kufanya muziki miaka ya 1980, lakini aliimarisha nafasi yake katika historia ya hip hop alipotoa wimbo wa Gangsta's Paradise mwaka 1995.

Sababu kamili ya kifo chake siku ya Jumatano bado haijawekwa wazi. Hata hivyo Posey aliiambia TMZ, ambayo iliripoti habari hiyo kwa mara ya kwanza, kwamba wahudumu wa afya waliamini kuwa huenda alipatwa na mshtuko wa moyo.

Coolio alishinda tuzo za Grammy kupitia wimbo wake wa Gangsta's Paradise, ambao ulitumika katika filamu ya Dangerous Minds iliyochezwa na Michelle Pfeiffer.

Wimbo huo unaendelea kusikilizwa na watu wengi na umesikiliwa na zaidi ya watu bilioni moja kwenye Spotify, kwa mujibu wa tovuti hiyo.

Zaidi ya kazi yake iliyochukua miongo minne alirekodi albamu nane na kushinda tuzo ya Muziki za American Music Award na tuzo tatu za Muziki za Video za MTV.

Vibao vyake vingine ni pamoja na Fantastic Voyage, Rollin' With My Homies, 1, 2, 3, 4 (Sumpin' New), na Too Hot.

Coolio amefariki akiwa ameaacha watoto 10, sita kati ya hao alizaa na mke wake Josefa Salinas aliyefunga nae ndoa mwaka 1996 na wakatalikiana mwaka 2000.

# MOBETO HATAKI WANAUME WATANZANIA

MWANAMITINDO muigizaji na muimbaji wa muziki wa Bongofleva, Hamisa Mobeto amesema anachukizwa na tabia za wanaume wa Kitanzania.

Hamisa anasema kuwa, anachukizwa na tabia zao za kuwatumia wanawake na kuwatelekeza baada ya kumaliza shida zao.

"Sitaki wanaume wa hapa Tanzania kwa sasa," anasema Hamisa ambaye ni mama wa watoto wawili; mmoja amezaa na Majizzo na mwingine amezaa na Diamond Platnumz.

Hayo yanakuja miezi kadhaa baada ya Hamisa kudaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Rapa wa Marekani, Rick Ross.

Kumbukumbu zinaonesha kwamba, Hamisa ameshawahi kutoka na wanaume kadhaa Watanzania ingawa kwa sasa haijulikani anatoka na nani.



# WEMA, WHOZU PENZI MOTOMOTO

IKIWA ni saa chache baada ya kuvujisha video yao ya mahaba mazito, nyota wa bongo muvi Wema Sepetu ameweka wazi penzi lake la msanii wa Bongofleva, Whozu.

Video inayotrend mjini kwa sasa, inamuonesha Miss Tanzania huyo wa mwaka 2006 akibusiana na Whozu huku wakiwa kwenye hafla fupi ya kusherekea siku ya kuzaliwa na Wema.

Kupitia ukurasa wake, msanii Whozu aliposti video hiyo na kuandika: "Nina furaha sana kuona Chi Mama akiwa na furaha. Kwa sababu muda wake mwingi anatumia kufurahi. "Hapendi kukosa raha, hapendi kukosa amani. Asante Mungu hata kwa hili nimeiongeza furaha yake siku yake ya kuzaliwa. Angalia alivyo na furaha. Unajua namna ninavyokupenda. Furahia siku yako."

Nae Wema alijibu kupitia instagram yake kwa kuandika; "Umekuwa faraja yangu kubwa sana Chibaba wangu. Umenipa amani ya moyo sijapata kwa muda mrefu mnooo. Wewe ndo furaha yangu kwa sasa. Umegusa maisha yangu kwa namna ambayo sijawahi hata kudhani.

"Tokea nakujua kama rafiki mpaka dakika hii nakuita "My Baby". Hata sijui tumefikaje fikaje hapa tulipo ila nachoweza sema ni kwamba najiona ni miongoni mwa wanawake wenye furaha sana duniani. Alhamdulillahfor you.

"Asante kwa kunipenda na mara zote kuwa hapa kwa ajili yangu. Mungu aendelee kukuweka sana kwa ajili yangu."



# SHANTA GOLD MINING YAPONGEZWA KWA UKARABATI WA UWANJA WA LITI

**Na Mwandishi Wetu**

UWANJA wa Mpira wa Liti zamani Namfua ulioko Singida uko tayari kutumika.

Kampuni ya Shanta Gold Mining ambayo ilijitosa kusaidia ukarabati wa Uwanja wa Liti zamani Namfua, Singida ambao kwa sasa umekuwa kivutio, inastahili pongezi kwa mujibu wa Meneja wake, Simba Hassan.

Akizungumza na gazeti hili, Meneja wa Uwanja huo, Hassan alisema kuwa Kampuni ya Shanta Gold Mining inastahili pongezi na wadau wote wa michezo nchini.

"Hadi sasa marekebisho ya uwanja huu yamefikia asilimia 90, tunatarajia kukamilika ukarabati huu wa maboresho ya awali mwaka huu kutoka kwa mkandarasi aliyepewa jukumu la kuukarabati ukiwa tayari kutumika," alisema Hassan.

Hassan aliishukuru Kampuni ya Shanta Gold Mining kwa kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu ambaye aliagiza viwanja vya michezo kufufuliwa.

"Tunawanashukuru kwa ujio wao Kampuni ya Shanta na imekuwa ikijitoa kwa vipaumbele vingi vya Singida. Tunaamini kusaidia ukarabati huo kutakuza mapato na kukuza michezo hapa, si Singida tuu bali kwa nchini nzima," alisema.

Uwanja huo kwa sasa upo katika hali nzuri na kuvutia na katika eneo la kuchezea kiwango chake ni kizuri na nyasi zikivutia tofauti na ilivyokuwa awali, huku jukwaa kuu ambalo lilikiwa halina paa, limeezekwa na vyumba vyote vimekarabatiwa.

Kwa upande wake, mkandarasi wa ujenzi huo, Hassan Rajab Tati alisema katika vipaumbele vyao walihakikisha ukarabati katika maeneo hayo unakuwa tayari mapema.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya KCB Tanzania, Christine Manyenye, akizungumza katika uzinduzi wa mashindano ya ngumi ya Mo Boxing yanayohusisha mataifa sita. Kulia ni Alan Pina kutoka Mexico atakayepigana, Mkurugenzi Mkuu wa MeTL Bajaj Tanzania, Ashish Josh, Ibrahim Class (kushoto) na Yahya Poli ambaye ni Katibu wa Baraza la Mchezo wa Ngumi za Kulipwa (TPBRC). Pambano hilo litafanyika leo katika ukumbi wa Mlimani City. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# JKU yajipanga kuisambaratisha Black Sailor

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu ya Zanzibar mzunguko wa tano inaendelea leo Ijumaa kwa kupigwa michezo miwili katika viwanja tofauti.

Katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 11:00 timu ya Maafande wa JKU itakawaribisha Black Sailor, wakati saa 2:00 usiku KMKM watawakaribisha Dulla Boys kutoka Kusini Unguja.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Timu ya JKU, Sheha Khamis alisema mchezo huo anatarajia utakuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao wanasaka matokeo.

Alisema wapinzani wao hawakufanya vizuri michezo yote waliyocheza hivyo watataka kuutumia mchezo huo kuhakikisha wanapata alama tatu.

Alisema wanawafahamu Black Sailor msimu huu wamesajili wachezaji vijana hivyo kutofanya vizuri katika michezo iliyopita kutawapa kasi ya kucheza kwani wanapata matokeo mazuri.

"Tunashuka dimbani kuwakabili Black Sailor najua utakuwa mchezo mgumu na wenye kasi, wenzetu hawakufanya vizuri michezo yote minne hivyo watakuja na mbinu ya kupata alama tatu, lazima tuwe makini sana," alisema.

Aidha, aliwataka mashabiki wa JKU kujitokeza kwa wingi uwanjani kama walivyofanya katika michezo iliyopita ili kuwapa hamasa wachezaji.

Timu ya JKU ipo nafasi ya nne ikiwa na alama saba huku wapinzani wao Black Sailor wanaburuza mkia wakiwa na alama moja katika msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar yenye timu 16.

## Kocha Singida Big Stars aitisha Azam

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Singida Big Stars, Mathias Lule, amesema wanaendelea na maandalizi kufanyia kazi ubora wa Azam FC kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Singida Big Stars inaendelea kujifua katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiweka sawa kabla ya kuivaa Azam Oktoba 3, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema kikosi kipo imara na wanaendelea kuimarisha timu yao kwa kufanyia kazi ubora wa wapinzani wao ili kupata matokeo mazuri ugenini.

Alisema ligi ina ushindani mkubwa kikubwa wanafanyia kazi mapungufu ya kikosi chao na kuingia katika mchezo huo kwa tahadhari kubwa kupata matokeo chanya.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya wapinzani wetu wako nyumbani, tunaandaa timu kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri na tunatarajia kuwafuatilia katika mechi ijayo wapinzani wetu wakicheza," alisema.

## DRFA kuisaidia serikali kukuza vipaji

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam(DRFA), umeeleza utaendelea kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kukuza vipaji, ili viweze kupata ajira kupitia michezo.

Kauli hiyo, imetolewa jijini hapo, juzi, na Kaimu Katibu Mkuu wa DRFA, Ramadhan Missiru, wakati akimuaga Shafii Lumambo ambaye amepata nafasi ya kujiunga na timu ya Tuzlaspor ya Tuzla mjini Istanbull nchini Uturuki.

"Unajua sera ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia ni kuhakikisha inatengeneza ajira nyingi kupitia michezo, hivyo kijana Shafii nenda ukajitume na umtanguliza Mungu kwanza kisha Tanzania, ukawe balozi wa nchi kwa kufanya mambo mazuri na kuitangaza nchi," alisema.

Missiru alisema kuwa wataendelea kushirikiana na serikali ili lengo hilo liweze kutimia kwa vijana wengi kupata ajira kupitia mchezo huo pendwa.

Akizungumza na gazeti hili, Shafii Lumambo, alisema anashukuru Mungu kupata nafasi hiyo ya kwenda kujiunga na timu ya Tuzlaspor na kuahidi kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania.

Mchezaji huyo alipata nafasi hiyo, baada ya kampuni ya Africa Youth Empowerment kuwachukua wachezaji wanane ambapo nyota hao wote, wamepata timu za kuzichezea za nje ya nchi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI KURUDI BARCA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, huenda akarejea Barcelona, kwa mujibu wa makamu wa rais wa uchumi, Eduard Romenu, ambaye alikiambia kituo cha redio cha El Mati de Catalunya kwamba, uhamisho wa mshambuliaji huyo wa Argentina "unawezekana." ***(The Sun)***

### BELLINGHAM AWINDWA CHELSEA

CHELSEA wamejiunga na kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa England na Borussia Dortmund, Jude Bellingham - bei ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, inakadiriwa kuwa pauni milioni 130, huku Liverpool na Real Madrid pia wakimtaka. ***(Telegraph)***

### SILVA NA MKATABA

KLABU ya Manchester City inapanga kufanya mazungumza na kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva kubaini ikiwa atajaribu kuondoka klabuni hapo mwisho wa msimu huu, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuonyesha hamu ya kuondoka kwa misimu miwili iliyopita. ***(Mail)***

### GUNDOGAN ATAKIWA BARCELONA

BARCELONA wanavutiwa na kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 akiwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake. (Sport)

### OSARIO ANYATIWA WOLVES

KLABU ya Wolves imeripotiwa kumsajili kiungo wa Chile Dario Osario kutoka Universidad de Chile kwa ada ya pauni milioni 5.5, huku Real Madrid na Manchester City hapo awali zikihusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18. ***(Express)***

### LUIZ KUMRITHI PARTEY

ARSENAL bado wanataka kumsajili Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 24 kutoka Aston Villa kuchukua nafasi ya kiungo wa kati wa Ghana anayeuguza jeraha, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 29. Kocha wa washikabunduki hao, Mikel Arteta alishindwa kumpata Luiz msimu uliopita, lakini yuko tayari kuwasilisha dau la tatu la kumnunua kiungo huyo wa Brazil, baada ya ofa mbili kukataliwa siku ya mwisho ya uhamisho. ***(The Sun)***

### OBLAK ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wanamnyatia mlinda mlango wa Atletico Madrid na Slovenia, Jan Oblak mwenye umri wa miaka 29, kama mbadala wa muda mrefu wa kipa wa Ufaransa, Hugo Lloris mwenye miaka 35. ***(Evening Standard)***.

### KULUSEVSKI KUBAKI

KLABU ya Tottenham Hotspur inatazamia kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 22 kwa mkataba wa kudumu wakati mkopo wake kutoka Juventus utakapoisha. ***(Fabrizio Romano***

### DE GEA ATAKIWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Manchester United, David de Gea huku mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 31 unakamilika mwishoni mwa msimu huu. ***( 90min)***

### ABRAHAM KURUDI CHELSEA

CHELSEA wanaweza kumsajili tena mshambuliaji wa England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 24 kutoka AS Roma kupitia kifungu cha kumnunua tena kwa pauni milioni 67. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA SASA YATAKA KUMSAJILI MESSI BURE

**Mtaalamu wao wa uchumi asema kwa sasa bajeti yao haiwezi kumudu, kwani inahitaji miaka miwili...**

**BARCELONA, Hispania**

MAKAMU wa Rais wa Uchumi wa Barcelona, Eduard Romeu, amethibitisha kuwa kumsajili tena Lionel Messi hakujapangwa kwa sasa katika bajeti ya klabu hiyo na kunaweza tu kuwa na manufaa iwapo mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or na nyota wa Camp Nou atapatikana kama mchezaji huru.

Messi alijiunga na Paris Saint-Germain kama mchezaji huru wakati mkataba wake na Barca ulipokamilika mwaka wa 2021.

Alikuwa amekubali kuongezewa muda, ingawa alikuwa ameomba kuondoka mwaka 2020, lakini hali mbaya ya kifedha ya klabu hiyo ikamlazimu kuondoka kutokana na kutomudu mshahara wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, hivi majuzi alikiri kwamba alitatizika katika mwaka wake wa kwanza pale Paris, lakini sasa 'anahisi tofauti', jambo ambalo linaonekana kuwa ameimarika zaidi.

Bado Barca wana nia ya kuungana nae tena na rais wa klabu, Joan Laporta alisema kwa ujasiri wakati wa majira ya joto kuwa sura ya Messi 'haijaisha' Barcelona na ripoti ya ndani mwishoni mwa juma lililopita ilipendekeza kuwa klabu hiyo imeanza kutafuta chaguzi za kujaribu kutimiza ndoto hiyo.

Romeu, akizungumza kwenye Redio Catalunya, ametoa zaidi katika habari hiyo.

"Kama atarudi, itakuwa bure, kwani kwenye bajeti yangu ni ngumu," alisema.

"Yeye ni ishara ya klabu, hapa patakuwa ni nyumbani kwake daima, lakini utakuwa uamuzi wa kiufundi."


Mkataba wa Messi na PSG unamalizika mwisho wa msimu huu, ingawa masharti ya mkataba huo yanajumuisha chaguo la kuongezwa kwa miezi 12 hadi 2024.

Romeu aliongeza kuwa ingawa hali ya kifedha ya Barcelona sasa iko katika hali nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa, bado hawana uwezo wa kufanya usajili mkubwa na inaweza kuchukua miaka miwili kabla ya mambo kurejea katika kiwango cha kawaida zaidi kwa klabu.

"Tumeiokoa Barca, lakini bado hatujasuluhisha," alielezea. "Hatuna afya; inahusisha ukali mwingi, ukali mwingi na kuna kazi nyingi ya kufanya. Msimu wa 2024/25 tutakuwa katika kiwango kinacholingana na sisi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,034,9
MECHI KALI
TANZANIA PRISONS
VERSUS
AZAM
1 | 3.55
X | 2.75
2 | 2.30
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BENZEMA AREJEA MAZOEZINI REAL MADRID




**MADRID, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Karim Benzema, alirejea mazoezini Jumatano baada ya kukosa wiki chache zilizopita kutokana na jeraha na anatarajia kurejea uwanjani wakati Los Blancos watakapowakaribisha Osasuna kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumapili.

Benzema alifunga mabao manne katika mechi zake sita za kwanza msimu huu, lakini hajaonekana tangu alipotoka katika kipindi cha kwanza cha ushindi wa Real kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Celtic mapema mwezi huu.

Mchezaji huyo mkongwe pia alikosa mechi ya kimataifa ya Ufaransa dhidi ya Austria na Denmark kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa wiki hii iliyopita.

Benzema amekiri kuwa hakufanya kazi yoyote ya mpira kabla ya kurejea uwanjani siku ya Jumatano, ingawa amekuwa akifanya kazi kwa bidii kwenye uwanja wa mazoezi, nyumbani na amefanya vyema programu ya mazoezi.

"Nimefanya kazi nyingi za kimwili. Sijagusa mpira. Leo(juzi) yalikuwa mazoezi yangu ya kwanza," alisema akiiambia RealMadrid.com.

"Nilifanya mazoezi ya nguvu nyumbani, nilichelewa kutoka likizo na sikuwa na muda mwingi wa kufanya maandalizi mazuri ya msimu, ndio maana nimefanya sasa na ninajisikia vizuri sana.

"Nina furaha kurejea na timu. Muda umepita na nimepata muda wa kufanya maandalizi ya msimu mpya. Najisikia vizuri sana. Nataka kucheza Jumapili."

Licha ya kutokuwapo kwa Benzema, Real wamedumisha mwanzo mzuri wa msimu huu.

Kikosi hicho cha Kocha Carlo Ancelotti kimeshinda kila mchezo ambao kimecheza hadi sasa, kikiwa na tofauti ya pointi mbili dhidi ya Barcelona kwenye LaLiga, na kuanza vyema hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Chelsea yajitosa kumwania Bellingham

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, kwa mujibu wa Telegraph.

Bellingham anavutia mashabiki wengi kutokana na uchezaji wake wa kuvutia akiwa na Borussia Dortmund na England.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 19 alijiunga na Dortmund kutoka Birmingham City mwaka 2020.

Chelsea ndio klabu ya hivi punde zaidi kujiunga na mbio za kumsajili kiungo huyo.



Mwandishi wa habari za usajili wa Italia, Fabrizio Romano amedai kuwa Liverpool, Manchester City, Real Madrid na Manchester United pamoja na Blues hao wanatafuta mpango wa kumnunua mchezaji huyo.

Romano ameripoti kuwa Dortmund bado haiko kwenye mazungumzo na klabu yoyote, badala yake wameahirisha majadiliano na uamuzi wowote kuhusu bei hadi baada ya Kombe la Dunia.

Gazeti la Telegraph limedai kuwa Bellingham atagharimu takriban pauni milioni 130.

905,195/-

# MKULIMA WA RUVUMA ALAMBA MIL. 6/- ZA JACKPOT BONUS

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Kijiji cha Liganga Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Bernard Benedict Oliver ameibuka na kitita cha Sh. 6,047,295 kwenye Jackpot ya katikati ya wiki baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 zilizochezwa wiki iliyopita.

Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi ya kitita hicho, Bernard alisema alianza kucheza na Sportpesa Julai, 2022 baada ya kusikia matangazo ya washindi mbali mbali kupitia televisheni.

"Kwa zaidi ya miaka kama minne au mitatu kurudi nyuma nilikuwa naona washindi mbali mbali wa Sportpesa wakitangazwa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii," alisema.

Benedict pia anajishughulisha na kilimo cha mahindi amesema kitendo hicho cha kuwa anaona washindi wakitangazwa mara kwa mara kupitia vyombo vya habari kilifanya aanze kufuatilia kimya kimya kuhusu Sportpesa.

"Unajua haikuwa rahisi kwa mimi kuchukua uamuzi wa kucheza michezo hii ya kubashiri kwa namna ambavyo inachukuliwa katika jamii kwa baadhi ya watu."

Benedict anasisitiza kuwa mwezi mmoja baada ya kuanza kucheza yaani mwezi wa nane alipata bahati ya kushinda kupitia Supa Jackpot kiasi cha shilingi laki 8.

"Ushindi huo ulinipa moyo sana na kuniongezea ari ya kucheza zaidi. Nimekuwa na kawaida ya kucheza sana Jackpot za Sportpesa kwa kuwa ndio nilikuwa nawaona washindi wengi wakitangazwa kushinda bonus na Jackpot yenyewe hasa hasa ile ya bilioni moja iliyoliwa mwaka huu.

Akiongelea mkeka wake wa Jackpot ulioshinda shilingi Tsh 6,047,295, Benedict anasema yeye huwa na kawaida ya kufuatilia mechi za Jackpot kuanzia Jumatatu kama zimetoka.

"Inapofika Jumatatu mara nyingi huwa naingia kwenye Sportpesa kuona kama mechi za Jackpot za wiki husika zimeshawekwa. Baada ya hapo husubiri mpaka usiku ndipo hutulia na kuchambua timu na kisha kuweka mikeka.

Mkeka huu ulioshinda niliweka mikeka mitano. Kati ya hiyo mitano mmoja ndio uliotoa Jackpot bonus ya shilingi Tsh 6,047,295 na visenti kadhaa. Baada ya kuweka mkeka wangu sikufuatilia matokeo".

Akimpongeza mshindi, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni ya Sportpesa, Sabrina Msuya alimpa kongole Benedict kwa kushinda Jackpot bonus na kumtaka kuendelea kucheza ili aweze kushinda pesa nono zaidi.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Bernald Oliver kutoka Ruvuma akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 6,047,295 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. Jackpot kubwa ya SportPesa kwa wiki hii ni Sh. 1,034,905,195. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Nabi: Kisinda yuko kwenye mipango yangu

INATOKA UK. 32

mazuri," alisema Nabi.

Yanga inawafuatilia Al Hilal katika michezo yao ikiwemo safari ya kikosi cha timu hiyo kuelekea nchini DR Congo kwa ajili ya kuweka kambi ya muda mfupi kabla ya kucheza mchezo wa Ligi ya Mabingwa Barani Afrika dhidi ya Yanga.

Kikosi hicho kikiwa nchini Congo kitacheza mechi mbili za kirafiki ya kwanza itakuwa dhidi ya TP Mazembe na As Vita na baada ya mchezo hiyo itakuja Tanzania tayari kuivaa Yanga.

## Simba yamjia juu Dejan

INATOKA UK. 32

mmoja wa mastraika waliochukua nafasi za walioonyeshwa mlango wa kutokea, Mkongomani Chris Mugalu na Mnyarwanda Meddie Kagere.

Wakati huo huo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amesema kuwa, hakuna mapungufu yeyote yatakayojitokeza kuondoka kwa Dejan, kwani Simba imesajili wachezaji zaidi ya 25. Dejan ambaye alitua Simba Agosti 7 mwaka huu na kufanikiwa kufunga bao moja Ligi Kuu Bara, Agosti 20 dhidi ya Kagera Sugar, ameamua kuvunja mkataba na klabu hiyo na kutimka.

Akizungumza na Nipashe, Mgunda amesema kuwa, hakutakuwa na tofauti yeyote ndani ya kikosi chake hicho baada ya kuondoka Dejan kwa kuwa ana kikosi kikubwa na kudai kuwa atakaa na uongozi ili kupata ripoti kamili juu ya mchezaji huyo.

"Simba tumesajili wachezaji zaidi ya 25, hivyo kwa sasa nazungumzia zaidi kikosi nilichokuwa nacho na walivyocheza jana 'juzi' dhidi ya Kipanga," alisema.

"Simba ina wachezaji wa kutosha na watacheza ligi na mashindano ya kimataifa, hivyo kutokuwepo kwake hakuna shida.

"Lakini suala lolote linalohusiana na mchezaji huyo uongozi ndio unaohusika na kutoa ufafanuzi, nitazungumza na uongozi nitakachoambiwa ndio nitaweza kuzungumza zaidi, kwa sasa nipo narudi kutoka Zanzibar kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu wa Jumapili dhidi ya Dodoma Jiji," alisema Mgunda.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/10/22 | 17:00 | Coventry vs Middlesbrough | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 02. 01/10/22 | 17:00 | Fulham vs Newcastle | 3.04 | 3.39 | 2.27 |
| 03. 01/10/22 | 17:00 | Rotherham vs Wigan | 2.33 | 3.19 | 3.09 |
| 04. 01/10/22 | 17:15 | Getafe vs Valladolid | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 05. 01/10/22 | 18:00 | Strasbourg vs Rennes | 2.92 | 3.36 | 2.32 |
| 06. 01/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 07. 01/10/22 | 19:30 | Werder Bremen vs Borussia Monchengladbach | 2.58 | 3.57 | 2.48 |
| 08. 02/10/22 | 14:00 | Lorient vs Lille | 2.92 | 3.42 | 2.30 |
| 09. 02/10/22 | 14:00 | Stoke City vs Watford | 2.38 | 3.18 | 3.03 |
| 10. 02/10/22 | 15:00 | Espanyol vs Valencia | 2.73 | 3.22 | 2.58 |
| 11. 02/10/22 | 16:00 | AJ Auxerre vs Brest | 2.67 | 3.36 | 2.52 |
| 12. 02/10/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.47 | 3.36 | 2.72 |
| 13. 02/10/22 | 16:00 | Sampdoria vs AC Monza Brianz | 2.31 | 3.29 | 3.04 |
| 14. 02/10/22 | 16:30 | Hertha BSC vs Hoffenheim | 2.97 | 3.56 | 2.21 |
| 15. 02/10/22 | 17:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 16. 02/10/22 | 18:30 | Leeds vs Aston Villa | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 17. 02/10/22 | 19:30 | Girona vs Real Sociedad | 3.19 | 3.14 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 30/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2078 | Tanzania Prisons vs Azam | 3.55 | 2.75 | 2.30 |
| 17:00 | 3038 | Avenir Rjich vs AS Slimane | 2.27 | 2.62 | 3.60 |
| 17:00 | 5174 | Olympique de Beja vs US Monastir | 2.74 | 2.55 | 2.92 |
| 18:00 | 2052 | ZR Temouchent vs RC Kouba | 1.46 | 3.68 | 6.88 |
| 18:00 | 2068 | ASM Oran vs MC Saida | 1.77 | 3.19 | 4.52 |
| 18:00 | 3284 | Novi Pazar vs Mladost Lucani | 1.40 | 4.31 | 6.47 |
| 18:00 | 3557 | RC Arbaa vs El Bayadh | 2.33 | 2.95 | 3.00 |
| 18:00 | 3595 | Ben Aknoun vs MCB Oued Sly | 2.00 | 3.09 | 3.63 |
| 18:00 | 3812 | Sabayil vs Gabala | 4.41 | 3.38 | 1.73 |
| 18:00 | 4429 | FAR Rabat vs Difaa El Jadidi | 1.44 | 4.03 | 6.29 |
| 18:00 | 5196 | MO Constantine vs JSM Skikda | 1.54 | 3.63 | 5.69 |
| 18:00 | 5836 | Ramtha Club vs Moghayer AL Sarhan | 1.64 | 3.60 | 5.20 |
| 18:30 | 4337 | Ararat Yerevan vs Urartu | 2.50 | 3.09 | 2.65 |
| 19:00 | 3335 | Radomiak Radom vs Cracovia | 2.30 | 3.05 | 2.95 |
| 19:00 | 3575 | Vsnk Varazdin vs Istra | 1.90 | 3.39 | 3.58 |
| 19:10 | 3923 | Vorwarts Steyr vs SV Horn | 2.89 | 3.39 | 2.18 |
| 19:10 | 4152 | First Vienna vs Kapfenberg | 1.35 | 4.71 | 6.68 |
| 19:10 | 5781 | Dornbirn vs Austria Vienna II | 2.31 | 3.38 | 2.69 |
| 19:30 | 5578 | Hvidovre IF vs Vejle BK | 2.62 | 3.40 | 2.36 |
| 19:30 | 5754 | Paderborn vs SV Darmstadt | 2.26 | 3.55 | 2.80 |
| 19:30 | 5848 | Hannover vs Hamburger SV | 3.20 | 3.50 | 2.08 |
| 20:00 | 3133 | Motala Aif vs IF Sylvia | 2.25 | 3.50 | 2.71 |
| 20:00 | 5308 | Gomel vs Vitebsk | 1.72 | 3.58 | 4.21 |
| 20:00 | 5822 | Aalborg vs Odense | 2.09 | 3.51 | 3.21 |
| 20:30 | 4613 | Nancy vs Cholet | 1.77 | 3.63 | 4.08 |
| 20:30 | 5600 | Yverdon-Sport FC vs FC Aarau | 2.60 | 3.58 | 2.29 |
| 21:00 | 1394 | Sporting Lisbon vs Gil Vicente | 1.29 | 5.22 | 9.03 |
| 21:00 | 2157 | De Graafschap vs Jong AZ Alkmaar | 1.50 | 4.28 | 5.38 |
| 21:00 | 2644 | Universitatea Craiova vs Voluntari | 1.54 | 3.78 | 5.97 |
| 21:00 | 4131 | Telstar vs Jong Utrecht | 1.91 | 3.53 | 3.58 |
| 21:00 | 4971 | US Biskra vs MC Magra | 2.13 | 2.95 | 3.44 |
| 21:15 | 4986 | FC Thun vs Neuchatel Xamax | 1.60 | 3.93 | 4.52 |
| 21:15 | 5877 | Lausanne vs Sport-FC Wil | 1.69 | 3.87 | 4.02 |
| 21:30 | 2783 | Chojnice vs Wisla Krakow | 3.39 | 3.29 | 1.99 |
| 21:30 | 3465 | Bayern Munchen vs Bayer Leverkusen | 1.32 | 5.78 | 6.78 |
| 21:30 | 4402 | SKN St Polten vs Amstetten | 2.09 | 3.34 | 3.10 |
| 21:30 | 5071 | Cosenza vs Como | 2.47 | 3.21 | 2.76 |
| 21:45 | 1578 | Mansfield vs Hartlepool | 1.42 | 4.28 | 6.97 |
| 21:45 | 3013 | Bohemians FC vs UCD Dublin | 1.32 | 4.61 | 7.84 |
| 21:45 | 3663 | Airbus UK Broughton vs Bala Town | 5.10 | 4.22 | 1.50 |
| 21:45 | 3703 | St Patricks vs Derry City | 2.74 | 3.18 | 2.38 |
| 21:45 | 3780 | The New Saints vs Newtown AFC | 1.19 | 5.91 | 10.84 |
| 21:45 | 4526 | Dundalk FC vs Drogheda Utd | 1.38 | 4.32 | 7.07 |
| 21:45 | 5364 | Standard Liege vs RFC Seraing | 1.56 | 4.12 | 5.23 |
| 22:00 | 1212 | Finn Harps vs Shelbourne | 2.74 | 3.13 | 2.41 |
| 22:00 | 2069 | Hull City vs Luton Town | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 22:00 | 4707 | Athletic Bilbao vs Almeria | 1.39 | 4.65 | 7.49 |
| 22:00 | 5909 | Tenerife vs Sporting Gijon | 2.24 | 3.04 | 3.29 |
| 22:00 | 5994 | Angers vs Marseille | 3.92 | 3.71 | 1.82 |
| 23:15 | 1631 | Porto vs Sporting Braga | 1.72 | 3.82 | 4.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Septemba 30, 2022

Nipashe


UKURASA 30




## Benzema arejea mazoezini Real Madrid




Wachezaji wa timu ya Singida Big Stars, Peu Dacruz (kushoto) na, Miguel Escobar, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YAMJIA JUU MZUNGU

●●● Kocha Mgunda asema kuondoka kwake hakuna pengo kwa kuwa Simba imesajili...

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

BAADA ya straika wa Simba raia wa Serbia, Dejan Georgijevic kuamua kuondoka kwenye kambi ya timu hiyo iliyokuwa Zanzibar siku ya Jumanne na kuandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuwa mkataba wake na klabu hiyo umevunjika kwa kile alichokiita kukiukwa, klabu hiyo nayo imemjia juu mchezaji huyo, ikidai haijaridhishwa na alichokifanya na kukitafsiri kama utovu wa nidhamu.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo iliyosainiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez imesema kuwa imepokea taarifa hiyo kwa masikitiko makubwa, kwani ametangaza kuvunja mkataba bila kufuata taratibu, badala yake ametumia mitandao ya kijamii.

"Uongozi wa klabu ya Simba umepokea taarifa ya mchezaji Dejan Georgijevic ya kuvunja mkataba na klabu yetu. Hata hivyo, tumesikitishwa na kitendo cha Dejan kuandika taarifa ya kuvunja mkataba kupitia mitandao ya kijamii bila hata ya kufanya mazungumzo na waajiri wake.

"Uongozi utachukua hatua stahiki juu ya mchezaji huyo kufuatia kuvunja mkataba bila kufuata utaratibu," ilisema taarifa iliyosainiwa na Barbara .

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema wao kama Simba hawafahamu kitu gani ambacho straika huyo alikuwa anakihitaji na hajatekelezewa, hivyo kwa namna alivyotangaza kuwa amevunja mkataba, basi watachukua hatua stahiki ili kila mmoja apate haki yake.

"Yeye ndiyo yupo kwenye nafasi nzuri ya kusema kitu gani hajatekelezewa, na kusababisha kuvunja mkataba, sisi kama Simba tunaona ametoa taarifa ya kuvunja mkataba kwa njia ambazo sisi hazituridhishi, kuna namna ya kuvunja mkataba, siyo kwa namna aliyovunja yeye, sisi msimamo wetu ni kwamba tunakwenda kuchukua njia stahiki ili kila mmoja apate haki yake," alisema.

Ahmed alipingana na dhana kuwa ameamua kufanya hivyo kutokana na kocha aliyemleta, Zoran Maki kuondoka kwenye klabu hiyo.

"Hakuna ukweli kuhusu hilo kwamba aliyemleta kaondoka hivyo na yeye anaondoka, kwanza Zoran hakumleta, huyu tulimsajili wenyewe," alisema.

Dejan alisajiliwa msimu huu, akiwa

INAENDELEA UK. 31

## Nabi: Kisinda yuko kwenye mipango yangu

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikijiimarisha kwa ajili ya mechi zao mbili ya Ligi Kuu Tanzania na Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesredine Nabi ameweka wazi amemuingiza winga, Tuisila Kisinda katika mipango yake na yuko fiti kutumika dhidi ya Ruvu Shooting.

Kisinda huenda akaanza kuonekana uwanjani Oktoba 3 kwenye mchezo wa ligi kuu dhidi ya Ruvu ambao ratiba inaonesha utapigwa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga ilimsajili Kisinda Augosti 31 wakitumia vema dakika za lala salama za dirisha la usajili kwa kumnasa nyota huyo mwenye kasi ya kimbunga akitokea klabu ya RS Berkane ya Morocco.

Kulikuwa na sintofahamu kuhusu uhakika wa Kisinda kuitumikia Yanga, lakini jambo hilo lilipatiwa ufumbuzi na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, wakimuidhinisha kuitumikia Yanga baada ya kukamilisha taratibu zote za usajili wake pamoja na kupata ITC kwa wakati.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema tangu aliposajiliwa na Yanga, Kisinda alikuwa akifanya mazoezi chini ya uangalizi maalum na sasa wamejiridhisha yuko tayari kuitumikia Yanga.

Alisema Kisinda ametua nchini alikuwa na mazoezi maalum chini ya kocha wa viungo na utimamu wa mwili na yuko fiti kucheza mechi yeyote ya Ligi Kuu iliyopo mbele yao.

"Nyota huyo yuko fiti sana suala la kumtumia au kutokumtumia itategemea na mpango wangu siku hiyo, ni mchezaji wa Yanga amesajiliwa ili kuitumikia timu hivyo ni lazima atapangwa," alisema Nabi.

Alisema wakati wa maandalizi ya michezo hiyo miwili, leo watacheza mechi ya kirafiki ya ndani kwa kuendelea kukisuka kikosi chake hasa baada ya kuona ubora na madhaifu ya Al Hilal.

"Tumewafuatilia wapinzani wetu, tumepanga mechi za hivi karibuni walizocheza huko Sudan na kuna taarifa zao za kucheza mechi mbili za kirafiki nchini Congo, zote hizo tunazifuatilia kikubwa ni kutafuta matokeo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >